


**LUGHA KATIKA KATIBA YA KENYA: UJITOKEZAJI WAKE KATIKA
UTANGAZAJI WA JANGA LA UVIKO-19**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili
katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.**

AGOSTI 2022

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawaasilishwa kwa mahitaji ya Shahada katika Chuo kingine chochote kile.


Sahihi.....  Tarehe:05/08/2022

Gladys Mogoi Mauti

C50/85194/2016


(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

Sahihi.....  Tarehe 25-11-2022

Dkt. Ayub Mukhwana

(Msimamizi)

Sahihi  Tarehe 21- 11- 2022

Prof. Iribe Mwangi

(Msimamizi)

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu Bw. Daniel Mauti Onchiri na Bi. Josephine Nyaboke Daniel ambao wamekuwa nguzo muhimu katika masomo yangu kuanzia shule ya msingi hadi uzamili.

SHUKRANI

Safari ya kukamilisha utafiti huu ilikuwa na changamoto si haba, ila nashukuru kwa ushauri, maelekezo na mawazo ya watu mbalimbali. Mchango wao mkubwa ulipunguza changamoto ambazo zilihusiana na utafiti huu. Natoa shukrani zangu kwa Mungu kwa neema yake katika kipindi hiki cha shahada ya uzamili na kuniwezesha kuikamilisha. Kwa neema ya Mungu tuliweza kuikamilisha tasnifu hii.

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu, Dkt. Mukhwana na Prof. Iribe Mwangi kwa kujitolea kwao kusoma na kunipa marekebisho yaliyonifaa si haba katika kukamilisha kazi hii. Walijitolea kwa hali na mali kunielekeza ipasavyo. Walinihudumia kila nilipowahitaji ingawa walikuwa na majukumu si haba chuoni na katika familia zao. Nawashukuru kwa mawaidha na maelekezo yao ya kitaaluma ambayo yalinifaa. Mungu awabariki na awaongezee hekima.

Nawashukuru watoto wangu, Javan Miruka, Nethanel Nyangoto na Shanzah Sarange kwa kunivumilia kipindi cha utafiti wangu. Nililazimika kushughulikia utafiti wangu na kuwanyima nafasi ya kutangamana nao hata wakati wa usiku.

Nawashukuru ndugu zangu kwa kusimama nami katika kipindi cha utafiti huu. Vile, siwezi kuwasahau rafiki zangu kama vile Ruth Binyanya na Dorca Getonto kwa kunipa moyo hata wakati nilikuwa nimekosa tumaini la kukamilisha tasnifu yangu. Mungu awabariki. Siwezi kuwasahau pia Hellen Bitutu, Ben Nyang'ate, Vanesa Nyang'arisa, Diana Bosibori, Nixon Ntabo na Yvonne sarange kwa msaada wao. Nawatakia maisha mema.

MAELEZO YA DHANA MUHIMU

Katika utafiti huu zipo dhana za kimsingi ambazo tutaeleza maana yake katika sehemu hii. Baadhi ya dhana zitakuwa na maana mahsusi na wala sio kama inavyozoeleka katika matumizi ya kawaida. Dhana hizo ni:

Uhusiano wa pragmatiki na isimujamii: pragmatiki ni fasili itokanayo na kilichosemwa kutegemea muktadha, hadhira, uhusiano wa wazungumzaji na masiala mengine ya kijamii. kwa upande mwingine isimujamii hujihusisha na uhusiano uliopo kati ya lugha na jamii inayotumia lugha husika. Kutokana na fasili hizi, pragmatiki na isimujamii ni matawi ya isimu yaliyo na mwingiliano mkubwa kwa kuwa yanashughulikia namna jamii hutumia lugha kwa mujibu wa muktadha wa matumizi. Hivi kwamba maana ya usemi fulani hutegemea msemaji, msemewa na sababu ya mazungumzo hayo.

Sera za lugha: haya ni maamuzi ambayo hufanywa na serikali kuhusu majukumu ya lugha katika taifa. Matumizi ya lugha fulani hupaswa kutekelezwa na viongozi na wananchi wa taifa husika. Sera za lugha hutokana na upangaji lugha.

Upangaji lugha: hii ni hali ya kuitathmini lugha na kuamua majukumu yatakayopewa lugha fulani. Upangaji lugha huwa shughuli ya kijamii ambayo huonyesha lugha fulani itatumiwa wapi, na nani, na itatumiwa lini. Upangaji lugha basi huhitaji hatua kuchukuliwa na kuundwa kwa sera ambazo zitahusu matumizi ya lugha katika taifa.

UVIKO-19: huu ni ugonjwa ambao husababishwa na virusi vya korona. Virusi hivi husambaa kwa haraka kutokana na mate na kamasi ya mwathiriwa. Mtu binafsi ana jukumu la kuhakikisha kuwa amejikinga na kuwakinga wengine ili kupunguza maambukizi zaidi kwa kudumisha usafi, kuvaa barakoa na pia kukaa umbali wa mita moja au zaidi na watu wengine.

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kubaini lugha katika katiba ya Kenya na ujitokezaji wake katika utangazaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya virusi vya korona. Virusi vya korona vilizuka nchini Uchina mwaka wa 2019 na kusambaa kwa haraka katika mataifa mengi ulimwenguni. Kutokana na kusambaa kwa haraka, serikali mbalimbali zilichukua jukumu la kuhamasisha raia wake dhidi yake. Serikali ya Kenya kupitia kwa Wizara ya Afya ilikuwa na jukumu la kuhamasisha Wakenya kwa kueleza chanzo, msambao na athari za virusi vya korona. Kwa hivyo, viongozi walitumia lugha kuwasilisha hotuba zao za uhamasishaji dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19. Ni kwa misingi hii ambapo tulitaka kujua iwapo viongozi walizingatia lugha kama inavyojitokeza katika katiba ya Kenya katika uhamasishaji wa Wakenya. Katika utafiti huu, tuliongozwa na malengo matatu ambayo ni: Kubaini athari za lugha ya utangazaji na uhamasishaji wa wananchi wa Kenya kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 kwa kurejelea vibadala mbalimbali vya kijamii, kujadili nafasi ya Kiswahili, Kiingereza, lugha za asili, lugha ishara na Sheng' katika utangazaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la UVIKO-19 na kubaini changamoto za kijamii na zile za kimatibabu ambazo hudhihirika baada ya kupuuza lugha kama zilivyoenezwa katika katiba ya Kenya katika kuwahamasisha raia wake kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19. Kwa kushughulikia malengo haya, tuliongozwa na nadharia ya uhusiano ya Wilson (1995) na ile ya utekelezaji iliyoasisiwa na Spencer (1971). Katika utafiti huu, tulibaini kuwa viongozi wengi walipuuza lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya na hili liliwafanya baadhi ya Wakenya kupuuza kanuni zilizowekwa na Wizara ya Afya kwa nia ya kupunguza maambukizi zaidi ya virusi vya korona. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa ni muhimu kuzingatia lugha ambazo zimepewa hadhi mbalimbali kikatiba hasa katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga fulani na hili litapelekea hatua mwafaka kuchukuliwa.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU	ii
SHUKRANI	iv
MAELEZO YA DHANA MUHIMU	v
IKISIRI	vi
YALIOMO	vii
SURA YA KWANZA	1
1.1 Usuli wa Mada ya Utafiti	1
1.2 Tatizo la Utafiti	3
1.3 Maswali ya Utafiti	4
1.4 Malengo ya Utafiti	4
1.5 Sababu za kuchagua Mada	5
1.6 Upeo na Mipaka	6
1.7 Msingi wa Kinadharia	7
1.7.1 Nadharia ya Uhusiano	7
1.7.2 Nadharia ya Utekelezaji	9
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada	12
1.8.1 Sera ya Lugha na Utekelezaji wake	12
1.8.2 Sera ya Lugha na Vyombo Vya Habari	19
1.9 Mbinu za Utafiti	21
1.9.1 Walengwa	21
1.9.2 Sampuli Kielelezo	22
1.9.3 Ala za Ukusanyaji Data	22
1.9.4 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data	22
1.9.5 Maadili katika Utafiti	23

SURA YA PILI.....	24
MAJUKUMU YA LUGHA MBALIMBALI KULINGANA NA KATIBA	24
2.1 Utangulizi	24
2.1.1 Majukumu ya Lugha kwa Mujibu wa Katiba ya Kenya.....	24
2.2 Kiswahili	25
2.3 Lugha Ishara.....	30
2.4 Katiba ya 2010 na Lugha za Kiasili	32
2.5 Lugha Vipindi ya Sheng’	35
2.6 Kiingereza na Lugha za Kigeni	37
2.7 Uhamasishaji na Utangazaji Kuhusiana na COVID-19 Kenya.....	40
2.8 Hitimisho.....	41
SURA YA TATU.....	43
LUGHA YA UTANGAZIAJI NA UHAMASISHAJI DHIDI YA COVID-19.....	43
3.1 Utangulizi	43
3.2 Tathmini Ya Lugha Ya Utangazaji Na Uhamasishaji Dhidi Ya COVID-19.....	43
3.2.1 Kufasiri Ujumbe Visivyo.....	44
3.2.2 Athari Chanya Za Lugha Ya Utangazaji Katika Uhamasishaji Wa COVID-19	56
3.2.3 Kuongeza Maarifa	56
3.3 Hitimisho.....	61
SURA YA NNE	63
NAFASI YA KISWAHILI KATIKA UHAMASISHAJI WA WAKENYA DHIDI COVID-19.....	63
4.1 Utangulizi	63
4.2 Kiswahili Kama Chombo Imara Cha Uhamasishaji Dhidi Ya COVID-19.....	63
4.3 Kiswahili Kama Kitambulisho na Kiunganishi Cha Wakenya	64
4.4 Kujenga Na Kuendeleza Mtindo Mpya Wa Maisha	68

4.5 Kujenga Elimu Bora.....	75
4.6 Kiswahili Kama Lugha Ya Uhamasishaji Dhidi Ya Janga La Korona Kupitia Kwa Muziki	79
4.7 Hitimisho.....	82
SURA YA TANO	84
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI	84
5.1 Utangulizi	84
5.2 Muhtasari.....	84
5.3 Mahitimisho Ya Utafiti	85
5.3.1 Athari Za lugha Ya Utangazaji Na Uhamasishaji Wa Wananchi Wa Kenya Kuhusu Ugonjwa Wa COVID-19.....	85
5.3.2 Nafasi Ya Kiswahili, Kiingereza, Lugha Za Asili, Lugha Ishara Na Sheng’ Katika Utangazaji Na Uhamasishaji Wa Umma Dhidi Ya Janga La COVID-19	86
5.3.3. Changamoto Za Kijamii Na Zile Za Kimatibabu Ambazo Hudhahirika Baada Ya Kupuuza Sera Ya Lugha Za Kenya Katika Kuwahasisha Raia Wake Kuhusu Ugonjwa Wa COVID-19	87
5.4 Changamoto za Utafiti	87
5.5 Mapendekezo	87
MAREJELEO	89
DATA YA UCHANGANUZI.....	93

SURA YA KWANZA

1.1 Usuli wa Mada ya Utafiti

Lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya hutokana na maamuzi ya serikali kupanga matumizi ya lugha fulani kwa lengo la kimawasiliano. Kwa mujibu wa Johnson (2013) upangaji wa lugha ni shughuli ya serikali kupitia bunge au korti kubaini matumizi ya lugha fulani kwa viongozi na wananchi wengine. Lugha yaweza kuteuliwa kuwa rasmi au ya taifa. Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanasema kuwa sera ya lugha ni mpango wa utekelezaji wa masuala ya lugha ambazo zimepewa majukumu mbalimbali katika taifa. Wanaendelea kusema kuwa sera ya lugha hulenga kutoa mwongozo kuhusu utaratibu wa matumizi mema ya lugha. Waandishi hawa wanaeleza kuwa sera ya lugha ni utaratibu wa matumizi ya lugha fulani ambayo imepewa hadhi ya kuwa aidha lugha ya taifa au lugha rasmi. Haya ndio tunayoyarejelea kama lugha katika katiba ya Kenya.

Utekelezaji wa matumizi yoyote ya lugha hutegemea upangaji lugha. Ngugi na Chacha (2004) wanazungumzia aina mbili za upangaji lugha ambazo ni upangaji lugha wa kikongoo na upangaji lugha wa kihadhi. Upangaji lugha wa kikongoo hushughulikia muundo wa lugha katika vipengele vya othografia, msamiati, hijai na vile vile maendelezo ya sarufi. Kwa upande mwingine upangaji lugha wa kihadhi huhusu uamuzi unaozingatia majukumu ya lugha fulani kimaeneo kukiwemo kitaifa. Lugha ya Kiswahili imefanywa kuwa lugha ya taifa na vile vile lugha rasmi kupitia upangaji lugha wa kihadhi. Hivyo tunatarajia kuwa viongozi hawatakiuka sera ya lugha ya Kiswahili kuwahamasisha Wakenya dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Nchi ya Kenya, katiba imeorodhesha lugha ambazo hutumiwa katika kufanikisha mawasiliano ya kitaifa. Nchini Kenya, Kiswahili ni lugha ya taifa na vilevile lugha ya kwanza rasmi kwa mujibu wa Katiba ya mwaka wa 2010. Kwa mujibu wa Mathooko (2007) lugha ya taifa huwa na jukumu la kuwaunganisha watu na kuondoa utabaka miongoni mwa watu wote katika taifa husika. Hii inaonyesha kuwa lugha ya taifa ni muhimu katika mawasiliano baina ya wananchi kwa kuwa ndio huwaunganisha watu wa matabaka na makabila mbalimbali. Lugha ya taifa inakuwa muhimu kutumika katika

mawasiliano yanayowahusisha watu wengi katika taifa. Lugha ya taifa inakuwa lugha mwafaka katika uhamasishaji wa wananchi wa Kenya kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19.

Ugonjwa wa UVIKO-19 husababishwa na virusi vya korona. Virusi hivi husambaa kwa haraka na ugonjwa huu umeathiri mataifa mbalimbali kukiwemo mataifa yenye nguvu kiuchumi. Ugonjwa huu ulianza mji wa Wuhan nchini Uchina mwishoni mwa mwaka wa 2019. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (W.H.O), ugonjwa huu husambaa kupitia mate au kamasi wakati ambapo mtu aliyeathirika anakohoa au kupiga chafya na kisha kumfikia mtu mwingine. Shirika hili la W.H.O linadai kuwa ugonjwa huu hauna chanjo kufikia sasa. Wanasayansi ulimwenguni wamejitokeza kujaribu kuuelewa ugonjwa huu na kupata chanjo ila hawajafanikiwa. Mathalan Profesa Turner S. anasema kuwa ni muhimu kujua asili ya ugonjwa huu ambao unaaminika kuwa ulitoka kwa wanyama ili kupata suluhisho lake. Msambao wa ugonjwa huu unaogofya na ndiposa mataifa mbalimbali ulimwenguni yanachukua hatua ya kuwahamasisha raia zake ili kupunguza maambukizi ya virusi vya corona.

Ugonjwa wa UVIKO-19 umeratibiwa kuwa janga la kimataifa. Ni kwa misingi hii mataifa mbalimbali yanaweka mikakati kuhakikisha kuwa wananchi wake wako salama na wamezuia maambukizi zaidi. Mataifa ya Afrika Mashariki hayajasazwa kutokana na janga hili. Serikali za Afrika Mashariki zimekuwa mbioni kuwahamasisha watu wake kuhusu ugonjwa huu kuanzia kwa namna ya kuupata na kuzuia maambukizi zaidi. Taifa la Kenya limejizatiti kuhakikisha kuwa linapigana na janga hili. Taifa la Kenya lina makabila zaidi ya 42 ingawa hivyo, Kiswahili na Kiingereza ndizo lugha ambazo zimetumiwa na viongozi kuwahamasisha Wakenya.

Tangu kuripotiwa kwa kisa cha kwanza katika taifa la Kenya uhamasishaji umekuwa ukifanywa ili kukabiliana na virusi vya corona kwa kuzuia msambao zaidi. Viongozi wa taifa la Kenya wamekuwa mstari wa mbele kuwahamasisha wananchi kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 ili kuzuia maambukizi zaidi. Viongozi wakiwemo rais na mawaziri wa wizara husika kama vile wizara ya Afya na ile ya usalama wamekuwa wakihutubia wananchi kuhusu janga hili kupitia vyombo mbalimbali vya habari ambavyo vimekuwa vikiwahamasisha watazamaji, wasomaji na wasikilizaji kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19. Ugonjwa huu ni tishio kwa taifa na ndio sababu shughuli nyingi zimesitishwa kukiwemo

usafiri wa abiria kutoka au kuingia miji ya Mombasa na Nairobi, taasisi za elimu kufungwa kwa muda usiojulikana na viwanda kupunguza waajiriwa wake. Wanaokufa kutokana na ugonjwa huu wamezikwa bila kuzingatia tamaduni za jamii husika. Suala hili la janga la UVIKO-19 limewafanya watu kubadilisha mazoea yao na kukumbatia ushauri wa serikali ili kupunguza maambukizi na hatimaye kukomesha ugonjwa huu. Hata hivyo, suala ambalo utafiti wa sasa unaangazia ni uteuzi na ufaafu wa aina ya lugha inayotumika katika kuutangazia ugonjwa huu katika taifa la Kenya. Utafiti huu utaangazia namna taifa la Kenya limefaulu kuwahamasisha raia wake dhidi ya virusi vya korona kwa kufuata au kukiuka lugha ambazo zimepewa hadhi katika katiba ya Kenya.

1.2 Tatizo la Utafiti

Utekelezaji wa matumizi ya lugha ambazo zimepewa majukumu mbalimbali kikatiba nchini Kenya hutokana na upangaji lugha ambapo lugha hupewa majukumu maalum katika jamii. Kulingana na katiba ya Kenya ya 2010, Kiswahili na Kiingereza ni lugha rasmi nchini Kenya. Kiswahili kimetajwa mwanzo katika kupewa jukumu la kuwa lugha rasmi. Kutajwa mwanzo ina maana kuwa Kiswahili ni lugha rasmi ya kwanza Kenya huku Kiingereza kikiwa lugha rasmi ya pili. Lugha ishara pia ni lugha ya taifa kwa watu walio na ulemavu wa kusikia na hata kuongea na vile vile ni lugha rasmi. Katiba ya Kenya pia inasisitiza suala la utamaduni na namna ambavyo Wakenya wana uhuru wa kujihusisha na utamaduni wanaoupendelea ikikumbukwa kwamba utamaduni na lugha ni vitu vilivyo na mafungamano makubwa na hatuwezi kuvitenganisha. Hii ndio sababu lugha za asili Kenya zinasisitizwa katika katiba ya Kenya ya 2010 na hivyo basi zafaa kulindwa na kutumiwa katika shughuli muhimu kama vile uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la UVIKO-19.

Lugha vipindi ya Sheng' ni muhimu pia katika uhamasishaji wa vijana dhidi ya janga hili. Je, hivi ndivyo hali ilivyo katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la UVIKO-19 nchini Kenya? Swali hili ndilo linaloshughulikiwa katika utafiti wetu nia ikiwa ni kuweka bayana lugha inayotumiwa katika utangaziaji na athari zake kwa umma kuhusu Janga la UVIKO-19. Njia mojawapo ya kuuthibiti ugonjwa huu ni kufuata kanuni zilizowekwa na wizara ya afya kama zinavyotangazwa. Kanuni hizi ni kudumisha usafi kila wakati na kuvaa maski. Je, viongozi hawa wanazingatia majukumu ya lugha

mbalimbali kikatiba au la? Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu utafanywa ili kubaini athari za ukiukaji wa katiba ya Kenya kwa kuzingatia majukumu yake ya lugha mbalimbali katika kuwahamasisha raia kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19. Utafiti huu pia una nia ya kubaini namna lugha ya utangaziaji na uhamasishaji kuhusu virusi vya korona inavyopokelewa na Wakenya.

1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na maswali yafuatayo ya utafiti:

1. Je, lugha ya utangaziaji na uhamasishaji wa wananchi wa Kenya kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 ina athari gani kwa wananchi kwa kuzingatia vibadala mbalimbali vya kijamii?
2. Je, nafasi ya Kiswahili, Kiingereza, lugha za asili, lugha ishara na Sheng' katika utangaziaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la UVIKO-19 ni ipi nchini Kenya?
3. Je, ni changamoto zipi za kijamii na za kimatibabu hudhihirika baada ya kupuuza matumizi ya lugha ambazo zimepewa hadhi kwa mujibu wa katiba ya Kenya wakati wa kuwahamasisha raia wake kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na malengo matatu. Malengo hayo ni:

1. Kubaini athari za lugha ya utangaziaji na uhamasishaji wa wananchi wa Kenya kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 kwa kurejelea vibadala mbalimbali vya kijamii.
2. Kujadili nafasi ya Kiswahili, Kiingereza, lugha za asili, lugha ishara na Sheng' katika utangaziaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la UVIKO-19.
3. Kubaini changamoto za kijamii na zile za kimatibabu ambazo hudhihirika baada ya kupuuza lugha ambazo zimepewa hadhi katika katiba ya Kenya wakati wa kuwahamasisha raia wake kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19.

1.5 Sababu za kuchagua Mada

Mataifa mbalimbali huwa na jukumu la kuwahamasisha na kuwaokoa wananchi wake kila panapozuka janga ambalo huenea kwa haraka. Serikali huwahamasisha raia wake ili kuzuia kuenea kwa janga ambalo linaweza kuwaathiri watu wengi. Uhamasishaji wa raia dhidi ya virusi vya korona unafanywa kwa kutumia lugha fulani. Vyombo vya habari hupeperusha matangazo yao kwa kutumia lugha walioichagua. Vipo vyombo vya habari ambavyo hupeperusha matangazo yao kwa kutumia lugha za asili, Kiswahili, Kiingereza na Sheng'. Lugha ishara pia hujitokeza kwa matangazo hasa ya televisheni. Ni muhimu kukumbuka kuwa lugha za asili kama vile Ekegusii na Kiluhya hazijasanifishwa. Hali hii inazua changamoto kwa kuwa mantiki inayotumiwa kuchagua lahaja ya utangazaji haijitokezi bayana. Kwa hivyo upo uwezekano wa watu wengine nchini Kenya kutoelewa yanayosemwa hasa katika maeneo ya mashinani. Matumizi ya lugha kikatiba katika hali hii inajitokeza kuwa na nyufa kwa kuwa haijaweka wazi lahaja inayopaswa kuzingatiwa katika lugha mbalimbali za asili ambazo hazijasanifishwa.

Kwa mujibu wa shirika la W.H.O janga hili limesambaa kwa haraka kwenye mataifa mengine ambapo limewaathiri maelfu ya watu na kusababisha vifo vya maelfu ya watu. Ni kwa sababu hii mataifa mbalimbali yameweka mikakati ya kupunguza kusambaa kwa virusi vya korona. Nchini Kenya kisa cha kwanza kiliripotiwa tarehe 13-3-2020. Viongozi, akiwemo rais na waziri wa Afya na wahusika wengine kwenye sekta ya afya waliwahutubia watu kupitia vyombo vya habari na kuwataka Wakenya kuwa waangalifu zaidi. Tangu kupatikana kwa kisa cha kwanza nchini Kenya viongozi wamechukua jukumu la kuwahamasisha watu kuhusu ugonjwa huu ili kupunguza msambao zaidi. Lugha ambayo inatumiwa na viongozi ni muhimu katika kutoa athari inayokusudiwa na kupelekea wananchi kuchukua hatua zifaazo kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona.

Katiba ya Kenya inaonyesha kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile kuwa lugha rasmi pamoja na lugha ya Kiingereza, lugha ishara pia ni lugha ya taifa na rasmi kwa watu walio na ulemavu wa kutosikia na kuongea. Lugha za asili vile vile zimesisitizwa na kuashiria kuwa lugha hizi zinatambuliwa katika katiba ya Kenya. Ni muhimu kuangazia lahaja ya lugha fulani ya asili inayotumiwa kwenye redio na televisheni, lahaja

mbalimbali huzua changamoto hasa katika uhamasishaji wa janga hili. Hii ina maana kwamba Kiswahili kinapaswa kutumika katika kiwango sawa na Kiingereza. Ingawa hivyo, matangazo na hotuba zinazotolewa na viongozi wa Kenya kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 hufanywa kwa Kiingereza zaidi. Kiingereza ni lugha rasmi nchini Kenya na inachukuliwa kuwa lugha ya waliosoma.

Janga hili halibagui kabila wala hali ya kiuchumi ya mtu. Ni kwa sababu hii ambapo viongozi wanapaswa kuzingatia matumizi ya lugha kikatiba wanapowahamasisha watu dhidi ya janga la korona na hatimaye kukabiliana nalo vilivyo kabla ya kusababisha maambukizi zaidi. Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu utataka kubaini athari ya lugha ya matangazo ya uhamasisho dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 nchini Kenya na kuelezea athari zake kwa Wakenya. Janga la virusi vya korona ni jipya na kwa hivyo hakuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kulihusu hasa katika mahusiko ya lugha inayotumika kulikabili. Kwa hali hii, utafiti huu ni muhimu katika ulimwengu wa taaluma ya Kiswahili kwa kuwa utakuwa moja katika tafiti za mwanzo kufanywa kuhusu lugha katika katiba ya Kenya na ujitokezaji wake katika utangazaji wa janga la virusi vya korona.

1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu unahusu janga la virusi vya korona ambavyo ni vipya kwa walimwengu na vimeathiri maelfu ya watu kote ulimwenguni. Wanasayansi kote ulimwenguni wanajizatiti kupata chanjo ya virusi hivi. Viongozi wa Kenya wako msitari wa mbele kuwahamasisha watu kwa kuwaeleza namna ugonjwa wa UVIKO-19 husambaa na njia za kujikinga na kuwakinga wengine ili kusitisha maambukizi zaidi. Utafiti huu utajikita kwenye lugha katika katiba ya Kenya katika utangazaji wa janga la virusi vya korona na athari za lugha ya uhamasisho wa raia wa taifa la Kenya.

Tutazingatia lugha ya matangazo yanayohusu ugonjwa wa UVIKO-19 nchini Kenya. Lugha hii itakuwa ya mazungumzo, ya maandishi na ishara, kipragmatiki na kiimplikecha. Tutajikita kwa lugha katika katiba ya Kenya na kisha kushughulikia athari za lugha zitumiwazo kutangazia na kuwahamasisha raia wake dhidi ya virusi vya korona. Tutatumia mtandao kupata data ya utafiti huu na vile vile kuwahoji Wakenya ili kupata maoni yao kuhusu lugha ya utangazaji wa ugonjwa wa UVIKO-19. Tutawahoji

Wakenya wa eneo la Utawala katika mitaa kama vile Airways, Kincar na Githunguri. Vile vile tutawazingatia Wakenya wa eneo la Ruai. Tutaeleza lugha kama chombo cha mawasiliano katika misingi ya Isimujamii. Kwa hali hii, tutazingatia vipengele vya kimawasiliano vinavyokwenda na lugha zungumzwa, lugha ishara na hata lugha kiimplikecha. Pragmantiki pia itajitokeza kwa kuwa sio rahisi kuitenganisha na isimujamii.

1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu utashughulikia majukumu ya lugha mbalimbali kwa mujibu wa katiba ya Kenya na ujitokezaji wake katika utangazaji na uhamasishaji wa raia dhidi ya virusi vya korona. Utafiti huu utajikita kwenye msingi wa kinadharia ili kutimiza malengo yetu ya utafiti. Tutaongozwa na nadharia mbili kwa sababu tutaangazia mada yetu kwa njia ya kiisimujamii na vile vile kipragmantiki. Nadharia za utekelezaji na ile ya uhusiano zitatowezesha kutimiza malengo yetu katika kushughulikia lugha katika katiba ya Kenya na utangazaji wake kuhusu janga la virusi vya korona.

1.7.1 Nadharia ya Uhusiano

Nadharia ya uhusiano inafuata mkabala wa kipragmantiki. Nadharia hii imeasisiwa na Sperber, D. na Wilson, D. (1995). Sperber na Wilson pia waliikuza nadharia hii katika mwaka wa 2002 na kisha mwaka huo huo Carston pia aliikuza nadharia hii. Lengo kuu la nadharia ya uhusiano ni kuonyesha namna usemi hufasiriwa na wasikilizaji. Ufasiri wa usemi fulani hutokana na muktadha wa mazungumzo au hata maandishi. Nadharia ya uhusiano hushughulikia namna msikilizaji huelewa usemi kutegemea ithibati mbalimbali.

Carston (2002) anadai kuwa, kulingana na nadharia ya uhusiano, mawasiliano huongozwa na kanuni moja tu, kanuni ya uhusiano. Anasema kuwa kanuni ya uhusiano huchuja habari kwa kuangalia kiasi cha uhusiano wake. Ni kwa misingi hii ambapo waasisi wa nadharia hii wanasema kuwa usemi huwa na aidha uhusiano wa juu au uhusiano wa chini. Carston anasema kuwa mtu hutumia gharama kidogo anapofasiri usemi ulio na uhusiano wa juu huku akitumia gharama kubwa kufasiri usemi ulio na uhusiano wa chini. Hii ina maana kwamba ni rahisi kufasiri usemi ulio na uhusiano wa juu kuliko ule wa uhusiano wa chini. Hii inaonyesha kuwa iwapo uhusiano baina ya

wazungumzaji ni wa juu, basi msemewa ataelewa kwa haraka anachomaanisha mzungumzaji.

Uhusiano ni kipengele muhimu katika masharti ya matumizi ya lugha katika jamii. Uhusiano hufanya watu kuweza kufasiri taarifa. Iwapo wazungumzaji wana uhusiano wa juu, basi msemewa ataelewa yale ambayo yanasemwa kama ni kinaya, ni jambo la kutadarukiwa au ni kejeli. Kanuni hii ya uhusiano husaidiwa na kuwepo kwa jambo la kuwasilisha yaani kipengele cha taarifa na sababu ya kutoa usemi huo. Sababu ya kutoa taarifa humfanya mtu kuzungumza kwa namna ambayo itamwezesha kufikisha ujumbe kwa namna aliyokusudia. Ujumbe unaotolewa humfanya mzungumzaji kutumia lugha itakayomfanya aweze kufikisha ujumbe kwa namna anayokusudia na kuwezesha wasikilizaji kuchukua hatua faafu. Ni kwa sababu hii ambapo tutachunguza sera za lugha nchini Kenya na utangazaji wake kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19. Nia yetu ikiwa ni kujua iwapo viongozi wanaotangaza na kuhamasisha umma dhidi ya virusi vya korona wanazingatia matumizi ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya au wanaikiuka. Tutataka kujua iwapo vyombo vya habari na viongozi wa Kenya wanazingatia lugha kikatiba ikizingatiwa kuwa mipango ya lugha ya nchi huhusishwa zaidi na siasa.

Nadharia ya uhusiano itatufaa katika kushughulikia matumizi ya lugha kikatiba na utangazaji wake kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19. Viongozi wa Kenya wamekuwa wakiwahamasisha umma dhidi ya janga hili ili kuzuia maambukizi zaidi. Katika hali hii, lugha imekuwa kipengele muhimu cha kufikisha ujumbe kwa raia wote. Mathalan, rais Uhuru Kenyatta na waziri wa afya Mutahi Kagwe wamekuwa wakiwapa wananchi ripoti na mikakati waliyoweka kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19. Viongozi hawa wamekuwa wakiwasiliana na wananchi kwa kutumia lugha ambayo wanaamini kuwa itaeleweka. Viongozi wanapaswa kutumia lugha ambayo itaeleweka na raia wote ili ujumbe uwafikie wote kwa maana ugonjwa huu haubagui kabila, umri au hata jinsia. Bila kutumia lugha itakayoeleweka basi kunakuwa na changamoto na hivyo basi hatua zifaazo za kuzuia maambukizi zaidi nchini huenda ikawa hazitafuatwa na wananchi ambao pengine hawaelewi lugha ya Kiingereza. Kwa mujibu wa nadharia ya uhusiano, viongozi wanapaswa kutoa usemi ambao utaeleweka na wananchi na iwapo sivyo, basi afadhali wasiseme lolote.

Hii ni kwa sababu iwapo usemi unaotolewa hautaeleweka na wanaoambiwa basi hawataweza kufasiri maana kama ilivyokusudiwa na wazungumzaji na kuchukua hatua zifaazo. Ni kwa misingi hii ambapo Wilson na Sperber (2002) wanasema kuwa ni vizuri kwa mwenye kutoa usemi kuhakikisha kuwa ameeleweka kwa urahisi ili hatua zifaazo zichukuliwe.

Wilson na Sperber (2002) wanasema kuwa mtoa usemi anapozungumza anaweza kutumia lugha ya upole na ikiwa hawezi basi abane taarifa au adanganye kwa nia ya kutimiza malengo yake. Katika kushughulikia janga la UVIKO-19, watoa ujumbe wana haja ya kutaka kila mtu apate ujumbe huo kwa mpigo fulani ili angalau watii maagizo yanayotolewa ya kupunguza maambukizi zaidi. Wanaotangaza wanaweza kubana taarifa fulani kama vile kusema wazi majina ya waathiriwa ili kupunguza unyanyapaa baada ya kupona. Ingawa hivyo, zipo taarifa ambazo zinasemwa wazi ili kuathiri umma na hatimaye kupunguza msambao wa ugonjwa huu. Ni kwa misingi hii ambapo tutafanya utafiti huu ili kuonyesha namna viongozi na washika dau wengine wa Kenya wanavyotangaza kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 kwa lengo la kuwahamasisha umma ili wajikinge na kuwakinga wengine.

Utafiti huu utaongozwa na mihimili ifuatayo ya nadharia ya uhusiano:

- a. Kwamba muktadha ni muhimu katika kufasiri usemi fulani.
- b. Kwamba kwa kutoa usemi ambao unahitaji kutadarukiwa wazungumzaji wanapaswa kutumia lugha wazi kwa kukadiria usemi wake ili kila mmoja ajue kama atatoa maelezo zaidi au atabana maelezo mengine.
- c. Kwamba usemi fiche hauhitaji maelezo kwa kuwa msemaji anapaswa kutaja kauli pekee bila kutoa maelezo zaidi.
- d. Kwamba uhusiano wa wazungumzaji na wazungumziwa husaidia katika kufasiri taarifa kwa namna fulani.

1.7.2 Nadharia ya Utekelezaji

Nadharia ya uhusiano haingeweza kushughulikia malengo yetu yote kwa pamoja hasa ikizingatiwa kuwa ni nadharia inayoegemea pragmantiki. Nadharia ya utekelezaji ni ya kiisimujamii na itatuwezesha kuangazia nafasi za lugha mbalimbali zinazozungumziwa

katika katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010. Nadharia hii ya utekelezaji itatuwezesha kuangazia sera ya lugha na ujitokezaji wake katika matangazo yanayohusu janga la virusi vya korona. Nadharia ya utekelezaji iliasisiwa na Spencer (1971). Nadharia hii hujumuisha mfumo na viasilia vyake. Viasilia vina majukumu ya kuupa mfumo uhai ili uendelee kutekeleza majukumu yake. Spencer anaendelea kusema kuwa iwapo viasilia vitatenganishwa na mfumo, basi itakuwa vigumu majukumu kutekelezwa kama ilivyokusudiwa. Mfumo hutokana na muungano wa viasilia ambavyo huzua umbo fulani linaloonekana. Ni kwa misingi hii ambapo Spencer anasema kuwa ni vigumu na hatari kugawa vipande ambavyo hutokana na kitu kimoja.

Nadharia ya utekelezaji inaashiria kuwa ni vigumu kutenganisha vitu ambavyo vimefumbatwa pamoja. Jamii huwa na muundo wa viasilia ambavyo vina uhusiano na mfungamano wa kipekee. Watu katika jamii huwakilisha viasilia na lugha wanayoitumia. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa ni vigumu na hatari kutenganisha jamii na lugha. Na iwapo jamii na lugha vitatenganishwa basi mambo hayatakuwa sawa hivi kwamba majukumu mengine yatakwama.

Kutokana na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa, katiba ya Kenya ya 2010 inatambua lugha ya Kiingereza na Kiswahili kama lugha rasmi nchini. Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi kwa mujibu wa katiba hii. Lugha ishara ni lugha rasmi na ya taifa kwa watu walio na ulemavu wa kutoongea na kutosikia. Katiba hiyo pia inatambua lugha asili za Kenya. Ingawa hivyo, matangazo kuhusu janga la UVIKO-19 yanajitokeza kinyume na katiba hii. Kiswahili kinapaswa kupewa nafasi sawa na ile ya Kiingereza. Lugha za asili pia zinatambuliwa katika katiba. Zipo stesheni za redio na zile za televisheni ambazo hupeperusha matangazo yao kwa lugha za asili. Ni muhimu kukumbuka kuwa zipo lugha za asili ambazo hazijasanifishwa licha ya kuwa na lahaja nyingi. Je, vyombo vya habari ambavyo hupeperusha matangazo yake kwa lugha za asili hutumia mantiki ipi kuteua lahaja ya lugha husika? Kwa mfano, kwa mujibu wa Etakwa, Akida na Mukhwana, kibaluhya kina lahaja zaidi ya 18. Stesheni za redio ambazo hupeperusha matangazo yake kwa kibaluhya hutumia lahaja ya Kimaragoli. Kwa mujibu wa wasomi hawa, Kimaragoli ambacho kinatumiwa katika stesheni za redio sio asili. Hali hii inazua vikwazo vya utangazaji kuhusu janga la virusi vya korona kwa kuwa wapo wabaluhya ambao

hawataelewa lahaja ya Kimaragoli. Ni kwa misingi hii ambapo tunajiuliza ni mantiki ipi ilitumiwa na vyombo vya habari kuchagua kutumia lahaja ya Kimaragoli na wala sio Kibukusu au lahaja nyingine ya Kibaluhia hasa ikizingatiwa kuwa Kibaluhya hakijasanifishwa.

Hali tulioizungumzia katika aya ya hapo juu inaonyesha namna vitu vilivyofumbatwa vinatenganishwa jambo ambalo ni hatari kwa mujibu wa Spencer (1971). Mapuuza ya lugha zingine za asili na matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa kubabaisha tu yanaashiria utengano wa viasilia unaojitokeza katika uhamasishaji wa raia wa Kenya dhidi ya virusi vya korona. Hatari iliopo ni baadhi ya raia kutofuata masharti yaliyowekwa na wizara kwa kutengwa katika uhamasishaji kilugha. Tutaongozwa na mihimili ya nadharia hii kama ilivyojadiliwa na Ngigge (2014) kama ifuatavyo:

1. Utambuzi wa pamoja kuhusu uamilifu wa kila kiasilia kinachounda umbo fulani.
2. Uzingativu wa uhusiano baina ya mahitaji, uwezo na mazingira yanayooana na mkabala husika.
3. Uzoefu wa ufungamano wa viasilia katika mfumo wa jamii.

Mihimili hii itatuwekea msingi wa kushughulikia lugha katika katiba ya Kenya na ujitokezaji wake katika matangazo yanayohusu janga la UVIKO-19. Nia ya utafiti wa sasa ikiwa ni kuonyesha nafasi ya Kiingereza, Kiswahili, lugha za asili, lugha ishara na lugha vipindi ya Sheng' katika uhamasishaji wa raia dhidi ya virusi vya korona. Hii ni kwa sababu ugonjwa wa UVIKO-19 husambaa kwa haraka na huweza kusababisha madhara makubwa. Hii ndio sababu serikali inachukua jukumu la kuhamasisha raia wake dhidi ya virusi vya korona ili kupunguza maambukizi zaidi. Lugha ambayo itatumiwa na namna ya kuitumia lugha hiyo itawezesha aidha raia kufuata au kutofuata masharti kutegemea namna serikali itahamasisha raia wake kwa kutumia lugha fulani mwafaka. Ni kwa sababu hii tunasema kuwa ni vigumu kutenga jamii na lugha na vile vile, ili kutimiza nia za uhamasishaji wa raia dhidi ya virusi vya korona, serikali inapaswa kuzingatia katiba na kwa hali hii kila lugha itatekeleza majukumu kama yalivyopakiliwa kwenye katiba ya mwaka wa 2010.

Uhamasishaji dhidi ya janga la virusi vya korona haufai kubagua maana ugonjwa huu haubagui watu kwa misingi yoyote ile. Hii ndio sababu hata vijana wa mitaa duni ya vijiji

vya Kenya wanafaa kuhamasishwa kwa lugha na ishara ambazo wanazielewa. Vijana hawa kama wanavyosema Osinde na Abdulaziz (1997) hutumia Sheng' kuwasiliana. Hii inaashiria kuwa katika uhamasishaji wa janga la kitaifa na hata ulimwengu kwa jumla, uhamasishaji unafaa kuzingatia jamii husika bila kuitenganisha na lugha wanayoipendelea. Ni hali hii inayotufanya kusema kuwa serikali ya Kenya inafaa kuweka mikakati ya kutumia lugha vipindi kama vile Sheng' hasa katika uhamasishaji dhidi ya majanga yasiyobagua kwa misingi ya kiuchumi wala kielimu. Lugha ni chombo muhimu katika uhamasishaji na ni muhimu kuteua lugha mwafaka kwa kujikita kwenye viamuzi vya lugha kama vile, mazingira, hali na tabaka na malezi.

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Sehemu hii inaangazia kazi mbalimbali zinazohusiana na malengo na tatizo la utafiti wetu. Tutawaangazia waandishi mbalimbali ambao watatuwekea msingi kwa utafiti wetu. Watafiti mbalimbali wameshughulikia suala la sera ya lugha ila hakuna utafiti ambao umejihusisha na ugonjwa wa UVIKO-19. Matumizi ya lugha kikatiba huongoza shughuli kama vile za kielimu, kiutawala na katika vyombo vya habari. Tutashughulikia vipengele vifuatavyo katika sehemu hii: Matumizi ya lugha kikatiba na utekelezaji wake pamoja na vyombo vya habari.

1.8.1 Matumizi ya Lugha Kikatiba na Utekelezaji wake

Matumizi ya lugha kikatiba hutokana na maamuzi ambayo hufanywa na serikali kuhusu majukumu ya lugha ambayo huteuliwa kuwa na hadhi maalum katika nchi fulani. Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanasema kuwa sera ya lugha huambatana na kuchukuana na mahitaji ya kisiasa, kiutawala, kiuchumi na kijamii ya wakati fulani husika. Viongozi nchini Kenya wamekuwa na jukumu la kutangaza na kuwahamasisha umma dhidi ya virusi vya korona. Viongozi hawa wamekuwa wakitumia lugha fulani wanapozungumzia janga hili aidha kwa kuzingatia au kutozingatia sera ya lugha ya Kenya ambayo inakitambua Kiswahili kama lugha ya taifa na vile vile lugha ya kwanza rasmi nchini, lugha ishara kuwa ya taifa na rasmi kwa walio na ulemavu wa kutosikia na kutoongea, Kiingereza kama lugha rasmi na vile vile katiba inazitambua lugha za asili nchini Kenya. Ni kwa misingi hii ambapo tutafanya utafiti huu kubaini nafasi ya

Kiswahili, Kiingereza, Sheng', lugha za asili na lugha ishara katika utangazaji kuhusu virusi vya korona.

Ogola (1990) anasema kuwa Wakenya wengi waliosoma hupendelea kutumia lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili katika miktadha rasmi. Alishughulikia mielekeo ya wasomi kuhusu lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Kulingana na Ogola, wasomi wengi wanaichukulia lugha ya Kiswahili kuwa ya watu ambao hawajasoma. Maoni ya Ogola yanaashiria kuwa lugha ya Kiingereza inachukuliwa kuwa lugha ya waliosoma huku ile ya Kiswahili ikipewa nafasi fedhehi na wasomi hawa hawa na kuiona kama lugha ya watu wasiosoma. Mwelekeo wa wasomi hawa ni hasi na inaonyesha ukiukaji wa sera ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010 ambayo imekiweka Kiswahili kuwa lugha ya kwanza rasmi na vile vile ni lugha ya taifa.

Utafiti wa Ogola unatofautiana na utafiti wa sasa kwa kuwa sisi tunashughulikia matumizi ya lugha kikatiba nchini Kenya katika uhamasishaji wa wananchi wake dhidi ya virusi vya korona. Ingawa hivyo, utafiti wake utakuwa muhimu kwetu kwa kuwa wapo wasomi ambao wanatumia kuhamasisha jamii ya Wakenya dhidi ya virusi vya korona. Wasomi hawa hutumia lugha fulani kwa nia ya kutaka kufikisha ujumbe kwa njia maalum na kisha kuibua taswira inayokusudiwa ili kupunguza msambao wa virusi vya korona. Hii ndio sababu utafiti huu ni muhimu kwa kuwa tutashughulikia namna viongozi hutumia lugha kuhamasisha raia dhidi ya UVIKO-19 na kubaini iwapo wanakienzi Kiingereza kama asemavyo Ogola, badala ya kujikita kwa katiba ya nchi.

Mbaabu (1996) alitafiti kuhusu sera ya lugha katika mataifa ya Afrika Mashariki. Aligundua kuwa kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki- Inter Territorial Language (Swahili) Committee ilisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki. Kiswahili kilienziwa wakati wa kamati hii. Ingawa hivyo wakati wa ukoloni mabadiliko kuhusu sera ya lugha Afrika Mashariki yalishuhudiwa. Kiswahili kilidunishwa na Kiingereza kikakwezwa. Umaarufu wa Kiswahili ulianza kufifia wakati wa ukoloni kwa kuwa wakoloni walizua sera zilizokidunisha kwa kukipa majukumu fedhehi. Mbaabu alitoa mfano wa matumizi ya Kiingereza kuwaadhibu wanafunzi waliozungumza Kiswahili na lugha za asili. Utafiti wa Mbaabu unaonyesha namna wakoloni walivyochangia katika kukidunisha Kiingereza. Ni kwa misingi hii ambapo watu

walikihusisha Kiingereza na walio na elimu huku Kiswahili kikichukuliwa kuwa lugha ya wale ambao hawajasoma. Hali hii itaangaziwa katika utafiti wa sasa kwa kuwa tunataka kubaini lugha tumizi katika matangazo kuhusu janga la virusi vya korona kutegemea sera ya lugha Kenya. Mbaabu alijikita kwenye sera ya lugha Afrika Mashariki huku sisi tukishughulikia sera ya lugha Kenya kwa kuangazia nafasi ya lugha mbalimbali katika utangazaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya virusi vya korona. Mbaabu anaonyesha kuwa watu waliosoma hukupendelea Kiingereza na kukidunisha Kiswahili ila ikumbukwe kuwa janga la korona linaathiri hata wale ambao hawajasoma. Kwa sababu hii basi, viongozi wanapaswa kuzingatia lugha ambazo zitafikisha ujumbe kwa Wakenya wote ili kupambana na janga pamoja. Hivyo basi, utafiti huu wa sasa unanui kuonyesha lugha za utangazaji na uhamasishaji dhidi ya UVIKO-19.

Tafiti zingine ambazo ni muhimu kwa utafiti huu wa sasa ni zile za Fink (2005) na Githinji (2008). Fink na Githinji walichunguza mielekeo ya watu wa jiji la Nairobi kuhusu lugha. Fink alitumia mbinu ya hojaji kwa wanafunzi wa chuo kikuu cha Daystar kukusanya data huku Githinji akiwahoji watafitiwa wake ambao ni vijana wa jiji la Nairobi kuhusu lugha wanayoipendelea katika kuwasiliana. Wasomi hawa walipata kuwa watu wa jiji la Nairobi huwasiliana kutumia lugha mbalimbali ingawa ipo mielekeo anuai kuhusu lugha hizo. Fink aligundua kuwa watu waliosoma hupendelea kutumia lugha ya Kiingereza huku Kiswahili kikitumiwa zaidi katika mazungumzo ya watu walio katika makundi mbalimbali ya kijamii. Naye Githinji aligundua kuwa vijana wa jiji la Nairobi hutambulishwa kwa msimbo wao wa Sheng'. Vijana hawa hutumia Sheng' katika mazungumzo yao ila walikuwa na mwelekeo hasi kuhusu msimbo wao wa Sheng'. Hii ni kwa sababu wanasema kuwa hakuna usanifu katika msimbo wao wa Sheng' kama zilivyo lugha kama vile za Kiswahili na Kiingereza. Hii inaonyesha kuwa watu huweza kutumia lugha fulani katika mazungumzo yao huku wakiwa na mielekeo hasi kuihusu.

Tafiti hizi ni muhimu kwetu kwani tunashughulikiwa lugha ambazo zimepewa hadhi na taifa la Kenya. Katika uhamasishaji wa Wakenya kuhusu virusi vya korona, lugha ya taifa inafaa kutumiwa kwa kuwa inachukuliwa kuwa inajulikana na Wakenya wengi. Hivyo basi, lugha ya Kiswahili ingekuwa mwafaka katika uhamasishaji wa Wakenya kwa kuwa ndio lugha itumiwayo kwa mapana nchini. Utafiti wa Fink na ule wa Githinji

unaonyesha kuwa vijana wanapendelea kutumia msimbo wao wa Sheng'. Ni kwa hali hii basi tunaonelea kuwa viongozi wanapaswa kutumia lugha ambazo zimetajwa katika katiba wanapowahamasisha Wakenya dhidi ya virusi vya korona ili ujumbe umfikie kila Mkenya. Ni kwa misingi hii ambapo tutajikita kwa Kiingereza, Kiswahili, lugha ishara, lugha za asili na Sheng'. Tafiti hizi ni muhimu kwa utafiti wa sasa ila zitatofautiana na zetu kwa misingi ya watafitiwa na pia kwamba sisi tutajikita kwa lugha kikatiba nchini Kenya na wala sio lugha yoyote ile kama walivyofanya.

Mathooko (2007) anasema kuwa sera za lugha zinahusu mpango wa utekelezaji. Kuwa sera za lugha hutekeleza mambo kama vile kutambua mahitaji ya kilugha ya taifa kwa kuzingatia jamii na makundi mbalimbali kitamaduni na kutambua jukumu la lugha kwa jumla na pia lugha mbalimbali katika maisha ya wananchi wa taifa linalohusika. Maoni haya ya Mathooko yanaonyesha kuwa watawala wanapopanga lugha huwa na jukumu la kuhakikisha kuwa wametilia maanani mahitaji ya wananchi wake. Lugha itakayoteuliwa na kupewa hadhi ya kuwa lugha ya taifa inapaswa kuwa ile ambayo imevuka mipaka ya kikabila na iwe inajulikana na watu wengi. Mahitaji ya wananchi huzingatiwa ili kuweza kupunguza vikwazo vya kimawasiliano baina ya watawala na raia. Maoni ya Mathooko ni muhimu kwa utafiti huu wa sasa kwa kuwa watawala wa Kenya wana jukumu la kuwahamasisha watu dhidi ya virusi vya korona ambavyo vinasambaa kwa haraka. Watawala hawa wanapaswa kutumia lugha itakayoeleweka na raia wa nchi husika ili hatua faafu zichukuliwe nao. Hii ina maana kwamba iwapo watawala watakiuka sera ya lugha katika nchi yeyote ile basi inawezekana pakawa na vikwazo vya kimawasiliano kama asemavyo Mathooko. Kwa upande wetu, tunachukulia pia kuwa lugha ni kiungo muhimu katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Hivyo basi ni muhimu kwa viongozi kutumia lugha mbalimbali katika uhamasishaji huu ili kupiga vita gong'wa la UVIKO-19 kwa pamoja.

Lugha ya Kiingereza imekuwa ikitumiwa na wale waliosoma huku wakikichukulia Kiswahili kuwa lugha ya watu ambao hawajasoma. Mukhwana (2008) alishughulikia mielekeo ya kilugha katika miji ya Kenya. Katika utafiti wake alipata kuwa Wakenya wanakipendelea Kiingereza. Aligundua kuwa watu wanakipendelea Kiingereza kwa kuwa kilinasibishwa na elimu bora nyakati za ukoloni na iliwezesha watu kupata ajira

nzuri. Ni kwa hali hii ambapo Wakenya wengi wanapendelea kutumia Kiingereza ili kujinasibisha na wasomi. Utafiti wa Mukhwana ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwa kuwa mielekeo ya wasomi kuhusu lugha ya Kiingereza na ile ya Kiswahili huwafanya kutumia lugha ambayo wanaipendelea na kuienzi. Ni katika hali hii ambapo huenda Wakenya wakapuuzwa sera ya lugha Kenya hasa wanapotangaza kuhusu janga la UVIKO-19. Ingawa hivyo, utafiti wetu utatofautiana na ule wa Mukhwana kwa misingi ya mwelekeo wa utafiti kwani yeye alichunguza mielekeo ya lugha katika miji mitatu ya Kenya nasi tutashughulikia majukumu ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya na namna inavyojitokeza katika utangazaji kuhusu virusi vya korona.

Mtafiti mwingine aliyeangazia Kiswahili kama lugha rasmi ni Ali (2011). Alishughulikia changamoto walizokumbana nazo watu waliokitumia Kiswahili ofisini. Alijikita katika ofisi mbili jijini Nairobi na akapata kuwa Kiswahili kilitumiwa kwa nadra sana katika ofisi za jiji la Nairobi. Aliwahoji watafitiwa wake na wakamweleza kuwa Kiswahili ni lugha ya watu wa tabaka la chini na wale ambao hawajasoma. Utafiti huu unaonyesha hadhi ya Kiswahili kwa mujibu wa watu waliosoma na kufanya kazi ofisini. Huu ni utafiti mwingine ambao unaashiria nafasi fedhehi ya Kiswahili ingawa ni lugha rasmi ya kwanza katika katiba ya nchi ya Kenya. Utafiti wetu unanua kuonyesha iwapo viongozi wanazingatia yaliyomo kwenye katiba kuhusu hadhi ya lugha mbalimbali na ufaafu wa matumizi ya lugha hizo katika kuwahamasisha raia dhidi ya UVIKO-19.

Shitemi (2011) anashikilia kuwa tangazo la Kiswahili kuwa lugha ya kwanza rasmi na lugha ya taifa linahitaji kuwekwa katika vitendo vya kimitaala, kiutendaji, kiuwezesaji na pia katika asasi zote za kutumia lugha. Hii inaashiria kuwa Kiswahili hakijakita mizizi katika hadhi yake ya kuwa lugha ya kwanza rasmi nchini Kenya. Wakenya wengi bado wanakipuuza na kukiona kama lugha duni ambayo hutumiwa na wale ambao hawajasoma. Hali hii imeshuhudiwa katika utangazaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la UVIKO-19. Viongozi wamepuuzwa lugha kikatiba ambayo inatambua pia lugha za asili za Kenya na katika hali hii basi huenda wananchi wengine wakakosa kupata ujumbe kwa namna inayofaa. Utafiti wa sasa utatofautiana na ule wa Shitemi kwa kuwa alishughulikia tu sera ya lugha ya Kiswahili ilhali sisi tutaangazia nafasi ya Kiswahili,

Kiingereza, Sheng', lugha ishara na vile vile lugha za asili katika utangazaji kuhusu janga la virusi vya korona.

Mekacha (2011) anaiona sera ya lugha kama kipengele kimojawapo cha mpango-lugha. Mekacha anaelezea aina mbili ya sera. Kwanza ni sera halisi ambazo anasema kuwa ni zile za jumla tu zitumiwazo katika matamko huku sera za kiishara zikiwa ni kauli na nyaraka ambazo hutumiwa tu kama ishara ya kukidhi matakwa ya kisiasa. Hii ina maana kwamba mataifa mbalimbali huweka sera za lugha ambazo ni vigumu kuzitekeleza. Kwa upande mwingine, sisi tutataka kubaini iwapo matumizi ya lugha kikatiba nchini Kenya ni halisi au ya kiishara kutegemea namna viongozi wanatumia lugha katika uhamasishaji wa raia dhidi ya janga la korona. Iwapo viongozi hawatafuata sera ya lugha kulingana na katiba ya nchi, huenda pakawa na vikwazo katika vita dhidi ya janga la korona. Hii ndio sababu tunasema kuwa ni muhimu kuzingatia matumizi ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya katika uhamasishaji wa raia dhidi ya UVIKO-19 ili kuweza kupunguza maambukizi yake. Tunapinga namna viongozi hutumia lugha wanayoipendelea katika kuwahamasisha raia wake dhidi ya janga la UVIKO-19 bila kuzingatia mahitaji ya kimawasiliano ya umma wakati ambao janga linaathiri waliosoma na wale hawakusoma.

Amolloh (2012) alikusudia kubaini namna mikakati iliyowekwa na serikali ya Kenya ilivyofanikisha utekelezaji wa sera ya Katiba ya mwaka 2010 iliyokifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza nchini Kenya. Alijikita kwenye shule za msingi kuchunguza changamoto zilizokumba shughuli ya utekelezaji wa sera hii katika kufundishia wanafunzi. Utafiti wake ulibaini kuwa kufikia wakati huo serikali haikuwa imechukua hatua yoyote kuidhinisha matumizi rasmi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi. Kwa upande mwingine, utafiti wetu wa awali unaonyesha kuwa viongozi hawazingatii sera ya lugha ya Kenya katika kuhamasisha umma dhidi ya janga la korona. Amolloh alikusanya data yake kupitia mbinu ya mahojiano ya ana kwa ana na washika dau mbalimbali wa elimu huku akiongozwa na nadharia jumuishi ya utambulisho ya Giles ya mwaka wa 1979. Utafiti huu wa Amolloh utatofautiana na wetu kwa kuwa malengo yetu ya utafiti ni tofauti na yake na pia tutaongozwa na nadharia ya uhusiano ambayo ni tofauti na yake. Pia sisi tutaangazia namna viongozi na vyombo vya habari vya Kenya vinavyotumia lugha kutangaza na

kuwahamasisha raia dhidi ya janga ambalo limetemesha ulimwengu mzima. Ingawa hivyo, utafiti wake ni muhimu kwetu kwa kuwa sote tunajikita kwa utekelezaji wa lugha kikatiba ila kwa mawanda tofauti.

Mirianga (2014) alichunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu majukumu yaliyotengewa lugha za Kiswahili, Kiingereza na za asili kwa mujibu wa katiba ya mwaka wa 2010. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa walimu wa shule za msingi walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu sera ya lugha Kenya kama ilivyojitokeza kwenye katiba. Katiba inatambua lugha ya Kiswahili, Kiingereza, lugha za asili na lugha ishara. Walimu hawa waliridhishwa na kukipa Kiswahili majukumu zaidi ya kuwa lugha rasmi na ya taifa Kenya. Utafiti wetu unanuia kubaini kama viongozi na vyombo vya habari vinazingatia sera hii ya lugha ya Kenya katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga ambalo lina athari nyingi hasi. Mirianga aligundua kuwa mwelekeo chanya wa walimu wa shule za msingi unaonyesha kuwa ni rahisi kubadilisha mtazamo wa raia kuhusu Kiswahili. Kwa upande wetu, tunaona kuwa viongozi na vyombo vya habari vina jukumu kubwa la kubadilisha mtazamo wa raia kwa kuwa wao hufikia wananchi wengi ikilinganishwa na walimu wa shule za msingi.

Utafiti wa Mirianga utakuwa wa manufaa katika utafiti wa sasa kwa kuwa tunaangazia suala la lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya kama alivyofanya. Ingawa hivyo, utafiti wake utatofautiana na huu wa sasa kwa kuwa tunachunguza lugha kikatiba na ujitokezeaji wake katika matangazo kuhusu janga la UVIKO-19 kinyume na Mirianga aliyeangazia mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu majukumu ya lugha mbalimbali zinazoangaziwa katika katiba ya Kenya.

Kiio (2017) alitaka kujua utayari wa Wakenya katika utekelezaji wa katiba kwa kujikita kwa lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi tofauti na tulivyozoea Kiingereza kama lugha rasmi nchini Kenya. Alipata kuwa utekelezaji wa sera hii ya lugha ulikumbwa na changamoto kama vile hadhi ambayo lugha hii imepewa na manufaa ya lugha ya Kiswahili. Akiongozwa na nadharia ya Utekelezaji ya Spencer (1971) aligundua kuwa lugha ya Kiswahili ilitumiwa sana na idara ya polisi huku Kiingereza kikitumiwa zaidi na vyombo vya habari. Ni kwa misingi hii ambapo tunadai kuwa vyombo vya habari havizingatii sera ya lugha ya Kenya ingawa ndivyo hutumika katika utangaziaji wa janga

la korona. Kiiro alitumia mbinu ya hojaji na mahojiano ilhali sisi tutawasikiliza viongozi wanapozungumzia janga la korona katika vyombo vya habari na vile vile tutawahoji Wakenya. Utafiti huu, kama ulivyo wa Amolloh (2012) unatofautiana na huu wa sasa kwa masuala ya malengo ya utafiti, upeo wa utafiti na hata nadharia ya utafiti. Hata hivyo, kazi hii ni muhimu kwa kuwa inachangia suala zima la lugha kikatiba katika kufanikisha maazimio ya serikali.

1.8.2 Lugha Kikatiba na Vyombo Vya Habari

Vyombo vya habari ni dola muhimu katika kupasha, kuhamasisha, kuonya na pia kueleza hali ya mambo katika nchi ya Kenya. Lugha itakayotumiwa katika utangazaji ni muhimu katika kuzua athari inayokusudiwa kutegemea kinachotangazwa. Ni kwa misingi hii ambapo vyombo vya habari vimekuwa vikitungaza na kuhamasisha umma dhidi ya janga la UVIKO-19. Kupitia kwa vyombo vya habari kama vile redio, runinga na magazeti wananchi wamepata kuuelewa ugonjwa wa UVIKO-19. Redio huwasilisha ujumbe kutumia lugha mbalimbali kukiwemo lugha za asili za Kenya. Redio ndicho chombo cha habari ambacho hutumiwa na watu hata mashinani ambapo hakuna sitima. Magazeti hununuliwa na watu ambao wengi wao huenda kazini huku runinga ikiwa kwa watu walio na nguvu za umeme. Kwa hali hii, redio ndicho chombo cha mawasiliano ambacho huwafikishia watu mbalimbali ujumbe. Wataalamu mbalimbali wamezungumzia lugha kikatiba na matumizi yake katika vyombo vya habari.

Mohochi (2002) alishughulikia mchango wa vyombo vya habari katika kukikiza Kiswahili Afrika Mashariki. Aliangazia vyombo kama vile runinga, redio na magazeti. Anaelezea kuwa vyombo vya habari vimekuwa msitari wa mbele kukitumia Kiswahili kwa nia ya kukikiza katika ukanda wa Afrika Mashariki. Ingawa hivyo, alipata kuwa stesheni nyingi hupendelea Kiingereza wakati mwingi wanapokuwa wakitungaza habari zao. Anatoa mfano wa Kenya ambapo magazeti mengi huchapishwa kwa lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na yale yanayotumia Kiswahili. Utafiti wa Mohochi unaonyesha wazi kuwa vyombo vya habari vinakitumia Kiswahili kwa muda mfupi ikilinganishwa na Kiingereza jambo ambalo linakiuka majukumu ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya. Ni muhimu kutaja hapa kuwa vyombo vya habari ni muhimu katika kuendeleza na kukuza lugha fulani. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa vyombo

vya habari havijaweza kutekeleza sera ya lugha ya Kenya ambayo inakitambua Kiswahili kama lugha ya kwanza rasmi nchini Kenya. Utafiti wa Mohochi utakuwa muhimu kwa utafiti wa sasa ila utatofautiana kwa kuwa sisi tuanashughulikia nafasi ya lugha katika utangazaji wa janga la korona kutegemea nafasi ya lugha hizi katika katiba ya nchi ya Kenya.

Amolloh (2012) alishughulikia suala la sera ya lugha na matumizi yake katika vyombo vya habari nchini Kenya baada ya Kiswahili kutangazwa kuwa lugha rasmi nchini. Amolloh aligundua kuwa lugha tawala katika vyombo vya habari ni Kiingereza. Alipata kuwa taarifa ya habari na mijadala mingi katika vyombo vya habari huendelezwa kwa Kiingereza kwa wakati mwingi. Alitoa mfano wa taarifa za habari za televisheni nchini Kenya ambapo taarifa kwa lugha ya Kiswahili hutangazwa saa moja hadi saa moja na nusu jioni huku habari za saa saba mchana hadi saa nane mchana na saa tatu hadi saa nne usiku zikiwa za Kiingereza. Hii inaonyesha kuwa televisheni kwa wakati mwingi huwasilisha matangazo yake kwa kutumia Kiingereza. Anazungumzia magazeti pia ambapo anasema kuwa magazeti mengi humu nchini huchapisha taarifa zake kwa Kiingereza. Hali hii inaonyesha kuwa vyombo vya habari vimekipa Kiswahili hadhi duni sana. Vyombo vya habari kama tulivyosema awali ni wazi kwamba ndivyo vina jukumu kubwa la kuwafikishia wananchi taarifa za habari.

Nchini Kenya rais, waziri wa afya na viongozi wengine huwasilisha ujumbe kuhusu UVIKO-19 wakati wa mchana. Wakenya hupata yaliojiri siku hiyo kuhusu virusi vya korona kutoka kwa vyombo vya habari. Hii ndio sababu tunaamini kuwa itakuwa rahisi kupambana na janga la korona kama Wakenya iwapo vyombo vya habari na viongozi watazingatia sera ya lugha ya Kenya. Utafiti wa Amolloh ni tofauti na wetu kwa kuwa alishughulikia utekelezaji wa sera ya katiba ya mwaka wa 2010 nchini Kenya huku utafiti wa sasa ukishughulikia sera ya lugha Kenya na ujitokezaji wake kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19. Ingawa hivyo utafiti huu utatufaa kwani sote tumejikita kwenye matumizi ya lugha kulingana na katiba ya Kenya huku tukihusisha vyombo vya habari.

Ngige (2014) alitaka kubaini utayari wa Wakenya katika kutekeleza mabadiliko ya sera ya lugha Kenya ipasavyo kwa kuangazia vyombo vya habari na shughuli za kiutawala ambazo ni viungo muhimu katika kuangazia sera ya lugha. Ngige alibaini kuwa vyombo

vya habari hupendelea Kiingereza kuliko Kiswahili. Alibaini kuwa mijadala mingi ambayo hufanywa kwenye vyombo vya habari hufanywa kwa Kiingereza. Hii ina maana kwamba watawala wenyewe hawakienzi Kiswahili na ndio maana wao hutumia Kiingereza wakati mwingi kama vile tumebaini katika utafiti wetu wa awali. Hali hii inarudisha juhudi za kupambana na janga la korona nyuma. Utafiti wa Ngige utakuwa muhimu kwa utafiti wa sasa ila utatofautiana na huu wetu kwa kuwa alijikita katika sera ya lugha katika vyombo vya habari nchini Kenya. Tofauti ni kuwa utafiti wa sasa unaangazia nafasi ya lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza, Sheng', lugha ishara na lugha za asili katika utangazaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la virusi vya korona. Hali ambayo itadhihirisha nafasi na ufaafu wa lugha mbalimbali kama zinavyotumiwa katika uhamasishaji wa Wakenya wakati wa janga fulani.

1.9 Mbinu za Utafiti

Kwa mujibu wa vyombo vya habari nchini Kenya, kama vile runinga ya Citizen, virusi vya korona vilianza kushuhudiwa Disemba, 2019 katika nchi ya Uchina. Inasemekana kuwa virusi hivi vilitoka kwa wanyama na kuwaambukiza watu mwanzo katika mji wa Wuhan nchini Uchina. Virusi hivi vimeathiri mataifa mengi ulimwenguni na wanasayansi wanajizatiti kutafuta chanjo ya virusi hivi. Utafiti huu utashughulikia lugha katika katiba ya Kenya na ujitokezaji wake katika utangazaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya virusi vya korona. Tutashughulikia namna viongozi wamekuwa wakitangaza na kuhamasisha umma dhidi ya virusi vya korona kupitia kwa vyombo vya habari kama vile redio, u-tube, runinga, magazeti na vipeperushi. Sehemu hii imegawanywa katika makundi matano ambayo ni walengwa, sampuli kielelezo, ala za ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data na maadili katika utafiti.

1.9.1 Walengwa

Walengwa wa utafiti huu ni watu wa taifa la Kenya hasa viongozi wanaotangaza kuhusu janga la UVIKO-19. Vile vile tutawatafiti Wakenya ili kujua namna wanavyoupokea ujumbe unaohusu uhamasishaji dhidi ya janga la korona. Tutakusanya data kwa kujikita kwenye katiba ya Kenya inayoshughulikia lugha kikatiba na kuonyesha nafasi za lugha mbalimbali nchini. Nia ya utafiti huu ikiwa ni kubaini nafasi ya Kiswahili, Kiingereza, Sheng', lugha ishara na lugha za asili katika utangazaji kuhusu virusi vya korona.

1.9.2 Sampuli Kielelezo

Utafiti wetu utakuwa wa uchambuzi ubora. Tutazingatia lugha inayotumiwa katika matangazo kuhusu virusi vya korona kwenye vyombo vya habari. Pia, tutapata kujua namna raia huupokea ujumbe kuhusu virusi vya korona kwa kuteua sampuli ya kimaksudi. Tutatumia idadi ya kimaksudi kwa nia ya kupata data itakayotuwezesha kutimiza malengo ya utafiti wetu. Tutaangazia lugha tumizi katika uhamasisho kuhusu kusambaa na kupunguza maambukizi ya virusi vya korona kwa misingi ya umuhimu na athari zinazojitokeza kutokana na matumizi ya lugha husika.

1.9.3 Ala za Ukusanyaji Data

Tangu kisa cha kwanza cha ugonjwa wa UVIKO-19 kuthibitishwa nchini Kenya, viongozi wameweka mikakati ya kuwakinga raia dhidi ya maambukizi zaidi ya virusi vya korona. Viongozi wamekuwa msitari wa mbele kuwahamasisha raia huku wakitumia mbinu mbalimbali kuhakikisha kuwa raia wanaelewa uzito wa janga hili. Matangazo mengi kwenye vyombo vya habari yanahusu janga la virusi vya korona.

Lugha inayotumiwa ni muhimu katika kuleta athari inayokusudiwa. Mitandao ya kijamii pia imejaa mazungumzo kuhusu janga hili. Ni kwa misingi hii ambapo tutatumia mitandao ya kijamii kama vile u-tube na twitter kupata data itakayotuwezesha kutimiza malengo yetu mbali na kunukuu hotuba za viongozi redioni, kwenye televisheni, magazetini na kwenye vipeperushi. Tutawahoji raia pia kwa kutumia maswali ya kimaksudi ili kupata mtazamo wao kuhusu hamasisho dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19. Tutawahoji watu kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni lugha iliyo na hadhi ya kuwa lugha ya taifa nchini Kenya. Kwa hali hii, kinasauiti cha kunasa taarifa za kila siku zitolewazo na viongozi mbalimbali wa serikali wakiongozwa na rais na waziri wa afya, tutahitaji karatasi na kalamu za kunukuu yale yatakayosemwa ili kupata kihali halisi kile kitakachokuwa kinasemwa na viongozi kuhusu suala la lugha na ugonjwa wa UVIKO-19.

1.9.4 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Baada ya kupata data kwa kusikiliza vyombo vya habari pamoja na teknolojia ya kisasa tutaiandika kwa daftari na hatimaye tutaichanganua data hiyo kwa lugha ya kinathari.

Tutashughulikia kila lengo la utafiti huu katika sura yake kwa kuzingatia mambo yaliyozungumzwa na viongozi wa nchi ya Kenya na pia matangazo ya vyombo vya habari kuhusu virusi vya korona. Tutarejelea mazungumzo ambayo yatawezesha kutimiza malengo ya utafiti wetu pekee yake. Data itakayokuwa imepatikana itapangwa kisura kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu na kuwasilishwa kinathari na kwa viambata lugha kama vile grafu, na paichati. Tutawarejelea viongozi kwa kutumia vyeo na majina yao kama vile, Waziri wa Afya, Kagwe na Watafitiwa wengine tutakaowahoji tutatumia M1 kwa maana ya Mtu wa Kwanza.

1.9.5 Maadili katika Utafiti

Utafiti huu unahusu lugha kikatiba na ujitokezaji wake katika utangazaji kuhusu virusi vya korona ambavyo vinasambaa kwa haraka. Tutatumia taarifa kutoka kwa vyombo vya habari na vipeperushi. Ni kwa hali hii ambapo tutalazimika kufuata maadili ya utafiti ipasavyo. Kwanza tutapata idhini kutoka kwa chuo kikuu cha Nairobi. Idhini hiyo itatuwezesha kufanya utafiti huo kwa kutumia vyombo mbalimbali vya utangazaji na vipeperushi. Tutatafuta idhini ya kunukuu matangazo ya viongozi kuhusu virusi vya korona kutoka kwa vyombo mbalimbali vya utangazaji na vipeperushi vingine. Pia tutatumia mahojiano yasiyo ya moja kwa moja na kwa hali hii tutawaeleza wahojiwa wetu maazimio yetu na kwamba watakatoyasema yatatumiwa tu katika utafiti wetu na wala si mahali pengine pale. Kwa hali hii tutakuwa tumeshughulikia masuala yao ya kiusalama.

SURA YA PILI

MAJUKUMU YA LUGHA MBALIMBALI KULINGANA NA KATIBA

2.1 Utangulizi

Nchi zenye wingilugha hupaswa kuteua lugha ambazo zitatumiwa katika mawasiliano yao yaliyo rasmi na yale yanayohusisha umma mkubwa. Kenya ni nchi iliyo na makabila zaidi ya 42 na yenye kuzungumza lugha zaidi ya 42 zikiwemo za kiasili na za kigeni. Hii ndio sababu ni muhimu kwa taifa hili kuteua na kuzipa hadhi lugha ambazo zinapaswa kutumiwa katika mawasiliano ya miktadha mbalimbali. Uteuzi wa lugha itakayotumiwa katika mambo rasmi ya serikali na ya mihadhara ambayo huwahusisha watu kutoka jamiilugha mbalimbali ni suala la serikali. Serikali ya Kenya imeangazia majukumu ya lugha hizi zake katika katiba ya mwaka wa 2010.

Kiisimu, lugha zote ni sawa na wala hakuna iliyo duni ikilinganishwa na nyingine. Hii ni kwa sababu kila lugha hutosheleza mahitaji yake ya kimawasiliano ya jamii husika. Ingawa hivyo, inakuwa muhimu kuteua lugha ambazo zitawasawazisha Wakenya wote katika hali na miktadha iliyo ya wote. Katika sura hii, tunashughulikia lugha mbalimbali kama zinavyojitokeza katika katiba ya Kenya huku suala la ufaafu likizingatiwa. Tunashughulikia lugha rasmi, za taifa na lugha za asili. Vile vile, tunaangazia lugha vipindi ya Sheng'. Hii ni kwa sababu uhamasishaji wa kuwahamasisha Wakenya dhidi ya janga la korona likiwa ndilo lengo lake kuu. Uhamasishaji wa umma huhitaji kufanywa kwa kutumia lugha ambayo itaeleweka na walengwa wote. Hili litafanikisha lengo la uhamasishaji huo dhidi ya gonjwa la korona. Ni kwa sababu hii pia tutaangazia uhamasishaji na utangazaji katika vyombo vya habari ili kuchunguza iwapo sera ya lugha nchini Kenya inatekelezwa wakati huu wa janga la korona.

2.1.1 Majukumu ya Lugha kwa Mujibu wa Katiba ya Kenya

Lugha mbalimbali huwa na majukumu tofauti nchini Kenya. Katiba ya Kenya imekuwa ikipitia marekebisho kuanzia enzi za ukoloni kufikia mwaka wa 2010 ambapo Kenya ilipata katiba mpya. Kulingana na Kibui (2014) serikali ya KANU kupitia kwa Wizara ya Elimu ilikuwa ikibadilisha hadhi ya lugha mbalimbali kikatiba baada ya Kenya kupata uhuru. Kulingana naye, hii ndio ilichangia hali ya lugha iliopo sasa nchini. Anaendelea

kusema kuwa Kiingereza kimepewa hadhi zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Anaendelea kusema kuwa Kiswahili kinatumika na Wakenya wengi ikilinganishwa na Kiingereza. Kibui anasema pia kuwa lugha za asili hutumika zaidi katika maeneo ya mashinani. Kulingana naye, lugha asili ni muhimu kwa kuwa hutumiwa na wenyeji katika mazungumzo yasiyo rasmi. Hii ndio maana sera ya lugha ya Kenya ya sasa inashughulikia pia lugha asili kama njia mojawapo ya kuendeleza utamaduni. Kwa mujibu wa katiba ya mwaka wa 2010 kifungu cha 7 kuhusu lugha ya taifa, lugha rasmi na lugha zingine ni kama ifuatavyo:

1. Lugha za taifa ni Kiswahili na lugha ishara.
2. Lugha rasmi Kenya ni Kiswahili, Kiingereza na lugha ishara.
3. Taifa linapaswa:
 - a. Kukuza na kulinda utofauti wa lugha ya watu wa Kenya.
 - b. Kukuza maendeleo na matumizi ya lugha za asili, lugha ya ishara ya Kenya, breli na miundo mingine ya mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu au waliozawadiwa lugha kwa njia tofauti.

Kifungu hiki cha 7 cha katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010 kinaonyesha kuwa taifa hili linazitambua lugha mbalimbali kwa kuangazia majukumu tofauti tofauti yanayotekelezwa na lugha hizi husika. Kiswahili kimepewa hadhi ya kuwa lugha rasmi na vile vile ya taifa nchini Kenya. Kiswahili na Kiingereza zimepewa hadhi ya kuwa lugha rasmi nchini Kenya. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa Kiswahili kimepewa hadhi maalum na hii ndio sababu tutakishughulikia katika kishemu kifuatacho kabla ya kuziangazia lugha zingine za nchini Kenya.

2.2 Kiswahili

Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile ni lugha rasmi kulingana na katiba ya Kenya ya 2010. Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi kwa mujibu wa katiba hii ya Kenya na hili limetajwa katika kifungu cha 7. Hii ina maana kuwa Kiswahili ndio lugha inayopaswa kutumiwa zaidi katika mawasiliano yoyote yale ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza. Kutajwa kwanza katika katiba ya Kenya ya 2010 kuna maana kuwa Kiswahili ndio lugha yenye hadhi zaidi ikilinganishwa na Kiingereza. Kwa hali hii basi, Kiswahili kinapaswa kutawala mawasiliano hata ya viongozi wanapozungumza na Wakenya wengine. Ingawa

hivyo, hali hii ni tofauti hasa katika kipindi hiki cha janga la korona ambapo viongozi wanatumia Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Hatimaye kidogo, sura zijazo za tasnifu hii zitasaili ni kwa nini hali iko hivi ilivyo nchini Kenya.

Lugha iliyoteuliwa kuwa rasmi huwa na majukumu ambayo inafaa kutekeleza katika taifa husika. Wardhaugh (1986) anaelezea majukumu ya lugha rasmi na kusema kuwa ndio lugha itumiwayo katika kuendesha shughuli zote za serikali, kufundishia katika shule za msingi hadi vyyuo vikuu na hutumika katika hati zote za serikali. Maoni haya ya Wardhaugh yanaonyesha kuwa lugha rasmi inapaswa kutumika kwingi katika mawasiliano rasmi katika nchi husika. Kwa hivyo basi, Kiswahili kinapaswa kutawala katika mawasiliano ya viongozi hasa wakati wa kuhamasisha umma dhidi ya janga la korona ambalo mbali na kuwa la kitaifa ni la kimataifa vile vile. Hii inaashiria kuwa majukumu ya lugha mbalimbali kikatiba nchini Kenya hayajaweza kutekelezwa kikamilifu. Hali hii inajitokeza pia katika elimu ambapo Kiingereza kinatumiwa katika kufundishia na katika utahini katika masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili pekee huku Kiswahili kikipuuzwa katika masomo mengine. Utekelezaji wa lugha kikatiba ya Kenya ya 2010 ni dhaifu na ndio maana viongozi wengi wanapendelea kutumia Kiingereza wanapozungumza na umma.

Kiswahili ni lugha ya taifa. Lugha ya taifa hutumiwa katika mawasiliano mapana ya nchi husika. Hii ni lugha iliyovuka mipaka ya kikabila na hivyo huwa lugha unganishi (Mathooko, 2007). Ni kutokana na ukweli huu ambapo Kiswahili ni lugha sambazi nchini Kenya. Hii inaonyesha kuwa Kiswahili ndio lugha inayotumiwa na Wakenya wengi ikilinganishwa na Kiingereza masuala ya kitaifa yanapoangaziwa. Kwa hali hii basi, Kiswahili kinakuwa lugha mwafaka ya uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona.

Kibui (2014) anasema kuwa Kiswahili ni lugha sambazi nchini Kenya. Hii ni kwa sababu, Wakenya wengi wanatumia Kiswahili ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza. Anasema kuwa usanifishaji wa lugha ya Kiswahili wa mwaka wa 1930 ulikiwezesha kukwea. Ingawa hivyo, wasomi hukidunisha Kiswahili jambo ambalo linakiuka majukumu ya lugha ya kikatiba. Anaonyesha namna Kiswahili kimepewa vipindi vichache shuleni ikilinganishwa na Kiingereza. Kiingereza pia kinatumika katika utahini

wa mitihani katika masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili. Hii inaonyesha kuwa wasomi wanakienzi Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili na hili ni jambo ambalo linafanya Wakenya kukipa Kiswahili hadhi fedhehi. Hali hii pia inadhihirika katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona ambapo viongozi wanatumia Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Hali hii inasababisha athari hasi kiasi cha kuwafanya Wakenya kupuuza ujumbe unaohusu janga la korona.

Kinoti (2019) anasema kuwa Kiswahili ni lugha ambayo inafaa kutumiwa katika uhamasishaji wa wananchi katika masuala yote yanayowahusu. Hii ni kwa sababu Kiswahili kinaeleweka na watu wa tabaka zote nchini Kenya. Anasema pia kuwa matangazo kuhusiana na masuala mbalimbali ya kimazingira yanaweza kutolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya Wakenya. Haya yanaweza kutokea kupitia kwa maandishi na michoro katika mavazi mbalimbali, vitabu na hata mabango. Kutokana na mtazamo wa Kinoti, tunaweza kusema kuwa uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya ugonjwa wa korona unapaswa kufanywa kwa kutumia Kiswahili zaidi kuliko Kiingereza. Mabango, mavazi na hata michoro mingine ya kuhamasisha raia dhidi ya korona basi inawasilishwa kwa kutumia Kiswahili. Hali ambayo ni kinyume kama tulivyobaini katika utafiti wetu wa kimbele zetu ambapo tuligundua kuwa Kiingereza kilitumika zaidi ikilinganishwa na Kiswahili.

Kwa mujibu wa Kinoti, Kiswahili ni chombo imara cha kuelimisha umma wa Wakenya kuhusu jambo fulani la kitaifa. Hii ni kwa sababu ni lugha ya taifa na sambazi katika taifa la Kenya. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa Kiswahili ni mwafaka katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la korona. Viongozi wa Kenya wanapaswa kutumia Kiswahili zaidi katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Hata hivyo, tuligundua kuwa mambo ni tofauti kwa kuwa viongozi wakiongozwa na Rais na Waziri wa Afya walitumia Kiingereza walipokuwa wakihutubia Wakenya kuhusu hali ya virusi vya korona nchini. Tuligundua kuwa viongozi wa taifa hili walitumia Kiswahili kwa nadra sana katika hotuba zao kama tutakavyoonyesha katika uchambuzi wetu katika sura zitakazofuata. Hali hii inakiuka lugha kikatiba na zaidi inakiukwa na viongozi wa taifa la Kenya wenyewe ambao wana jukumu la kuunda sheria za nchi. Pia, viongozi

hawa wanakosa hata kutilia maanani ukweli kuwa Wakenya wengi wanaelewa Kiswahili zaidi ikilinganishwa na Kiingereza.

Vyombo vya habari ni muhimu katika usambazaji wa taarifa zinazowahusu Wakenya kama watu wa taifa moja. Hivyo basi, vyombo hivi vinakuwa muhimu katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la korona. Lugha kikatiba itatekelezwa kikamilifu iwapo vyombo vya habari Kenya vitakuwa mstari wa mbele kuitekeleza. Vyombo vya habari nchini Kenya pia vinapaswa kutumia Kiswahili zaidi katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga korona. Ingawa hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa hali ni tofauti kwa kuwa Kiingereza kilitumika zaidi ikilinganishwa na Kiswahili katika matangazo kuhusu janga la korona. Kama inavyoweza kuthibitishwa na Youtube, Waziri alitumia Kiingereza kila alipoongea kwenye vyombo vya habari kuelezea hali ya janga la korona nchini Kenya. Maelezo kuhusu virusi vya korona kwenye runinga yaliandikwa kwa Kiingereza. Jambo hili linakiuka yale yaliyo kwenye katiba ya mwaka 2010 ambayo imekipa Kiswahili hadhi ya kuwa lugha ya kwanza rasmi nchini Kenya na vile vile kuwa lugha ya taifa Kenya.

Matumizi ya lugha kikatiba nchini Kenya inaashiria kuwa Kiswahili ndio lugha iliyopewa majukumu mawili: lugha rasmi na ya taifa. Ni kwa sababu hii ambapo tunasema kuwa Kiswahili kinafaa kutumiwa zaidi na viongozi na vyombo vya habari katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga hili la korona. Ontieri (2017) anasema kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Kenya na kwa hali hii basi hii ndio lugha ambayo inafaa kuwa inaeleweka na kutumiwa na Wakenya wengi kwa ajili ya mawasiliano ya kila siku kukiwemo uhamasishwaji dhidi ya korona. Hata hivyo anasema pia kuwa lugha hii ya Kiswahili imekuwa ikipuuzwa na Wakenya na kuchukuliwa kama lugha ya watu wasio na elimu ya kisasa. Kupuuzwa huku na kudunishwa kwa Kiswahili kumejitokeza wazi katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya virusi vya korona. Hii inaonyesha kuwa watu waliosoma na kupata vyeo mbalimbali nchini Kenya hukiona Kiswahili kama lugha duni na kwa sababu hii basi wao huepuka kukitumia.

Hali ya kuupuza na kukidunisha Kiswahili ni jambo ambalo linakiuka sera ya lugha ya taifa la Kenya. Ukiukaji wa sera ya lugha Kenya una maana kuwa lengo la uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya UVIKO-19 halitatimizwa kutokana na kuwa ujumbe

utawafikia watu ambao wamesoma na kukijua Kiingereza. Ikumbukwe kuwa, virusi vya korona havibagui watu kwa misingi ya kabila lao, kiwango chao cha elimu wala hali zao za kiuchumi. Hii ndio maana tunasema kuwa uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya UVIKO-19 unapaswa kufanywa kwa kutumia Kiswahili, ambacho ni lugha rasmi ya kwanza nchini Kenya na lugha ya taifa na hivyo kitaeleweka na wengi nchini humo. Kwa njia hii basi, ujumbe utawafikia Wakenya wengi na hivyo kufuata kanuni za Wizara ya Afya na hatimaye kupunguza maambukizi zaidi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Kiswahili kinaonekana kuwa lugha ambayo huwaunganisha watu wa taifa la Kenya. Kwa hivyo basi, hii ndio lugha ambayo viongozi wa Kenya wanapaswa kutumia katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Hii ndio lugha unganishi nchini Kenya. Kama wasemavyo Habwe na wenzake (2010) lugha ya taifa huwa na majukumu kama vile kuwaunganisha watu wote nchini, kuondoa umatabaka miongoni mwa wananchi kwa kutumia lugha moja na kupata nguvu ya pamoja kama taifa. Nguvu ya pamoja inafaa zaidi katika vita dhidi ya janga la kitaifa kama lilivyo la korona nchini Kenya. Vita dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 vitafaulu iwapo Wakenya wote watahusishwa kikamilifu na serikali. Wakenya watahusishwa tu iwapo lugha tumizi itakuwa ile ambayo ni unganishi na inayoeleweka na watu wengi nchini Kenya ambayo ni Kiswahili.

Jukumu kuu la lugha yoyote ile ni kukidhi haja ya mawasiliano. Wakati huu wa janga la korona, mawasiliano kutoka kwa serikali ni muhimu ili kuzuia maambukizi zaidi ya virusi vya korona. Viongozi wamekuwa wakiwahamasisha umma na kuwaelezea namna ya kuzuia maambukizi zaidi kwa kutumia lugha. Kwa hali hii lugha tumizi inakuwa kiungo muhimu katika kufanikisha au kukwamiza mawasiliano. Hapa utekelezaji wa katiba kuhusu majukumu ya lugha mbalimbali unajitokeza wazi. Majukumu ya lugha kikatiba nchini Kenya inaelekea kuwa inapuuza na viongozi wenyewe kama inavyodhihirika katika matumizi yao ya lugha hasa wanapozungumza na umma katika miktadha mbalimbali ya kitaifa ikiwemo ya kisiasa na hata ya kimatibabu kama huu tunaazungumzia wa janga la korona.

Kama tulivyokwisha kutaja, Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi na vile vile ya taifa nchini Kenya. Kwa hali hii basi, Kiswahili ni chombo muhimu cha mawasiliano baina ya

watu wa jamiilugha mbalimbali nchini humo. Kwa mujibu wa Kiango (2002), nchini Kenya, Kiswahili kinatumiwa na watu zaidi ya asilimia 80 huku Kiingereza kikitumiwa na watu wasiozidi asilimia 20. Maoni ya Kiango yanaonyesha kuwa Kiswahili ni lugha sambazi nchini Kenya na ambayo haifai kupuuzwa kama chombo cha mawasiliano. Kiswahili kinatumiwa na watu wengi ikilinganishwa na Kiingereza. Hali hii inaashiria kuwa idadi kubwa ya Wakenya hutumia Kiswahili katika mawasiliano yao ikilinganishwa na wale wanaotumia Kiingereza. Hivyo basi, Kiswahili kinakuwa lugha mwafaka katika shughuli ya uhamasishaji dhidi ya janga la korona. Kiswahili kinaonekana kuwa lugha bora katika mawasiliano yanayohusu watu wote nchini humo. Ni kwa sababu hii ambapo tunasema kuwa Kiswahili kinapaswa kutumiwa zaidi katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la UVIKO-19.

Nchini Kenya, wapo watu walio na ulemavu wa kusikia na kuongea. Taarifa za serikali kuhusu virusi vya korona pia ni muhimu kwa watu hawa. Hii ni kwa sababu wao pia wako katika hatari ya kuambukizwa virusi hivi. Lugha pekee wanayoielewa ni ile ya ishara na ni kwa sababu hii basi ni muhimu kwa serikali kutilia maanani upekee wao. Kisehemu kifuatacho kinashughulikia lugha ishara.

2.3 Lugha Ishara

Kwa mujibu wa katiba, lugha ishara ni ile ambayo hutumiwa na watu walio na ulemavu wa kusikia na kuongea. Katiba ya Kenya ya mwaka 2010 pia inaitambua lugha ishara kama lugha rasmi na lugha ya taifa la Kenya kwa Wakenya walio na ulemavu wa kusikia na kuongea. Katika sura ya 4, kifungu cha 54, katiba ya Kenya ya 2010 inasema kuwa watu walio na ulemavu wana haki ya kupata taarifa zozote muhimu kwa kutumia lugha ishara. Seneti ni asasi ambayo huwa viongozi ambao huunda kanuni za nchi ya Kenya. Maseneta, wa Kenya nao wamewahi kuzungumzia suala la lugha ishara. Kwa mujibu wa bili ya Bunge la Seneti (2019), serikali inapaswa kuzingatia lugha ishara kwa kuwa ni muhimu kwa watu walio na ulemavu wa kusikia na kuongea. Bili hii inaitaka serikali kuzingatia mambo kadhaa kuhusu walemavu wa kusikia na kuongea. Serikali ya Kenya inapaswa:

1. Kuhakikisha kuwa watu walio na ulemavu wa kusikia wanajumuishwa katika jamii.

2. Kuwatambua wanaotoa huduma za ukalimani wa lugha ishara.
3. Kuhakikisha kuwa walemavu hawa wanapata huduma zote za umma.

Hii ina maana kwamba viongozi wanapaswa kuhakikisha kuwa Wakenya walio na ulemavu wa kusikia na kuongea wamefikiwa na taarifa zote muhimu. Vipengele hivi vya bili ya seneti ya Kenya vinaonyesha kuwa walemavu hawa wamejumuishwa katika jamii kupitia kupata taarifa zote, muhimu na wanazozistahili. Walemavu hawa wanapaswa kujua hali ya janga la korona nchini Kenya. Hili litawawezesha wao pia kujua chanzo na namna virusi hivi husambaa. Kwa hali hii basi, walemavu hawa wanaweza kujikinga na kuwakinga watu wengine nchini Kenya.

Njia ya kimsingi ya kupata taarifa muhimu walemavu wa kusikia na kuongea ni kupitia kwa lugha ishara ya Kenya. Ni kwa sababu hii tunasema kuwa serikali ya Kenya inapaswa kuweka mikakati mwafaka ya kuhakikisha kuwa walemavu pia wamepata taarifa za kutosha kuhusu virusi vya korona. Serikali ya Kenya inafaa kuhakikisha kuwa kuna mkalimani wakati wanatoa taarifa zinazohusu virusi vya korona. Pia walemavu wana haki ya kupata huduma zote za umma kama Wakenya wengine. Hii ina maana kuwa kila asasi inayotoa huduma nchini Kenya kwa umma inapaswa kuwa na mkalimani ili walemavu wa kusikia na kuongea waweze kuhudumiwa ipasavyo pia.

Kutokana na yale tuliyoyajadili katika sehemu hii ni kuwa walemavu wana haki ya kilugha kama Wakenya wengine. Hii ndio sababu katiba pia ina vipengele vinavyoshughulikia haki za walemavu hasa kuhusiana na kupata huduma muhimu na taarifa kutoka kwa serikali. Bunge la Seneti pia lina bili inayoitaka serikali ya kitaifa na ile ya kaunti nchini Kenya kutilia maanani matumizi ya lugha ishara hasa katika kutoa huduma za serikali. Vile vile, wanaserikali wanatakiwa kuhakikisha kuwa yupo mkalimani wa lugha ishara kila wanapotoa hotuba. Hii ina maana kuwa serikali kuu na ile ya kaunti inapaswa kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa walemavu wa kusikia na kuongea wanafikiwa na taarifa pia. Hali hii pia inapaswa kushuhudiwa wakati wa kuhamasisha raia dhidi ya janga la korona nchini Kenya.

Wataalamu wa lugha ishara pia wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa kuweka mikakati tosha ya kuhakikisha kuwa walemavu wanapata huduma na taarifa muhimu kama Wakenya wengine wote. Kwa mfano, Mweri (2016) anasema kuwa ni muhimu kwa

serikali ya Kenya kuhakikisha kuwa inaweka mikakati ya matumizi ya lugha ishara ili walio na ulemavu wa kusikia na kuongea waweze kuhusishwa katika shughuli za serikali. Mweri anasema kuwa lugha ishara ndio lugha ya kwanza ya watu walio na ulemavu huu. Walemavu wa kusikia na kuongea hawana lugha nyingine wanayojua isipokuwa lugha ishara. Wao huwasiliana na watu wengine kwa kutumia lugha ishara. Hii ndio sababu katiba ya Kenya imeifanya lugha ishara kuwa lugha rasmi na ya taifa kwa watu walio na ulemavu wa kusikia na kuongea. Janga la korona limeathiri kila mtu nchini Kenya. Viongozi wamekuwa mbioni kuhakikisha kuwa wanapunguza maambukizi ya virusi hivi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Utafiti huu utataka kubaini iwapo viongozi walikuwa wakitilia maanani walemavu wa kusikia na kuongea wakati wa uhamasishaji dhidi ya UVIKO-19.

Ni muhimu kwa Wakenya wote kupata taarifa muhimu hasa zile ambazo zinapaswa kushughulikiwa na kila mtu nchini. Tumeangazia namna lugha ishara ya Kenya ni muhimu kwa watu walio na ulemavu wa kusikia na kuongea. Tumeonyesha kuwa katiba ya nchi imeangazia lugha ishara na kuonyesha namna inapaswa kutekelezwa. Sera ya lugha nchini Kenya inajitokeza kuwa yenye inajali maslahi ya watu wa matabaka yote na makabila yote ya Kenya. Hii ndio sababu katiba hiyo hiyo inaangazia lugha rasmi ambayo hutumiwa katika shughuli zote rasmi za nchi, lugha ya taifa ambayo huunganisha Wakenya, lugha ishara ambayo ni muhimu kwa walemavu wa kusikia na kuongea na lugha za asili. Kisehemu kifuatacho kinahusu katiba na utamaduni ambapo tutashughulikia lugha asili za Wakenya.

2.4 Katiba ya 2010 na Lugha za Kiasili

Katiba ya Kenya inatambua utamaduni kama msingi wa utambulisho wa jamii mbalimbali za nchi hii. Kenya ni nchi iliyo na watu wa jamiilugha mbalimbali. Jamiilugha hizi huwana utamaduni ambao huweza kuwatambulisha. Katiba ya Kenya inazitambua tamaduni hizi na kuonyesha umuhimu wa utangamano mzuri bila kubaguana kwa msingi wa tamaduni hizi. Hii ndio maana katiba ya Kenya ya 2010 inaangazia majukumu ya lugha mbalimbali kukiwemo lugha za asili. Katika katiba ya Kenya ya 2010, sura ya 2, Kifungu 11, kinabainishwa mambo yafuatayo kuhusu utamaduni:

1. Katiba inatambua utamaduni kama msingi wa ustaarabu wa Wakenya.

2. Serikali:-

- a. Itakuza aina zote za kujieleza katika utamaduni kupitia kwa fasihi, sanaa, sherehe za kitamaduni, sayansi, mawasiliano, habari, vyombo vya habari, uchapishaji, maktaba na turathi nyingine zinazohusishwa na tamaduni za Wakenya.
- b. Kutambua jukumu la sayansi na teknolojia za kiasili katika maendeleo ya nchi.
- c. Kutambua haki za kiubunifu za Wakenya kupitia kwa lugha zao za asili.

Kifungu hiki cha katiba kinaonyesha wazi kuwa utamaduni wa Wakenya kupitia kwa lugha zao za asili ni muhimu kwao na hata kwa serikali. Hii ndio sababu katiba inautambua kwa kutaja kuwa utamaduni ni msingi wa ustaarabu wa Wakenya katika kipengele cha kwanza. Kipengele cha pili, ni wazi kuwa watu wana uhuru wa kujieleza na kuonyesha utamaduni wao kupitia kwa nyenzo zote za mawasiliano, kukiwemo: vyombo vya habari, uchapishaji na mawasiliano. Hii ina maana pia kuwa Wakenya wako huru kujieleza kwa kutumia lugha zao za asili.

Wakenya wana haki ya kupata taarifa kupitia vyombo vya habari na asasi zingine kwa kutumia lugha ambayo wanaielewa zaidi. Katika hali hii, wapo Wakenya wengine ambao huzungumza na kuelewa tu lugha yao ya kwanza. Hii ina maana kwamba, taarifa za uhamasishaji dhidi ya janga la korona zinapaswa pia kufanywa kwa kutumia lugha hizi za asili. Serikali ya Kenya itafaulu tu katika vita dhidi ya janga la korona iwapo taarifa itamfikia kila Mkenya kupitia kwa lugha iliyomzaa na kumlea. Taarifa ikifika kama inavyostahiki, basi, Wakenya watafuata kanuni na sheria za Wizara ya Afya za namna ya kuzuia maambukizi zaidi ya UVIKO-19.

Kwa wa lugha kikatiba, Kenya, ni wazi kuwa lugha za asili ni muhimu katika kufikisha ujumbe kwa Wakenya wote. Hii ndio maana tunapata vyombo vya habari ambavyo hutangaza kwa kutumia lugha za asili. Vyombo hivi ni kama vile: Egesa, Musyi na Mulembe. Hizi ni stesheni za redio ambazo hutangaza kwa lugha za Ekegusii, Kikamba na Kiluhya mtawalia. Vile vile, zipo stesheni za runinga ambazo hupeperusha matangazo yake kwa lugha za asili kama vile Inooro ambayo hutumia Kikuyu. Hali inaonyesha kuwa serikali ya Kenya inaruhusu kuwepo kwa vyombo vya habari ambavyo hupererusha

matangazo yake kwa lugha asili. Hili lina maana kuwa lugha za asili zinatiliwa maanani kwa kiasi fulani kama zilivyoielezwa katika katiba ya Kenya 2010. Katika sura ya 4, kifungu 44, katiba ya Kenya inasisitiza kuwa:

1. Kila Mkenya ana haki ya kutumia lugha na kushiriki katika maisha ya utamaduni wa chaguo lake.
2. Mkenya anayetoka jamii ya utamaduni au lugha fulani ana haki, pamoja na wanajamii wengine:
 - a. Kufurahia utamaduni wake kwa kutumia lugha yake.
 - b. Kuunda, kujiunga na kudumisha vyama vya kitamaduni na kilugha na miungano mingine ya watu katika jamii.

Utamaduni wa Wakenya umezingatiwa na katiba ya Kenya kama ambavyo tumeonyesha kutoka kwa vifungu vya katiba. Hii ina maana kuwa Wakenya wako huru kutumia lugha zao za asili wanapowasiliana na pia kupata taarifa muhimu kwa kutumia lugha zao za asili. Hali hii itarahisisha mawasiliano kwa kuwa ujumbe utafika kwa kila mtu bila vikwamizi vikubwa. Katiba ya Kenya inaonyesha kuwa kila Mkenya ana uhuru wa kupata taarifa kwa kutumia lugha ambayo anaipendelea. Tumeonyesha kuwa katiba ya Kenya inazitambua lugha rasmi, ya taifa, lugha ishara na lugha za asili. Lugha hizi zimepewa hadhi maalum katika katiba ya Kenya ya 2010. Haya yote yanathibitisha kuwa kila Mkenya ana uhuru wa kupata taarifa muhimu kutoka kwa serikali kwa lugha anayoipendelea. Zipo lugha ambazo hazijaangaziwa kwenye katiba ya Kenya ila ni muhimu katika kufikisha taarifa muhimu kwa kikundi mahsusi cha kijamii. Uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona hukusudiwa kufikia kila Mkenya kwa lugha na namna inayoeleweka vizuri. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa katiba ya Kenya ya 2010 inawapa Wakenya uhuru wa kutumia lugha ambazo wanazipendelea.

Uhuru wa kutumia lugha ambazo zinapendelewa na kueleweka na makundi fulani ya kijamii ni muhimu katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga fulani kama lilivyo korona. Uhuru huu unaruhusu hata makundi mengine ya kijamii ambayo huwa na lugha ambazo hazijaangaziwa katika katiba kupata taarifa kwa namna ambayo wanafurahishwa. Kwa hali hii basi, makundi haya ya kijamii yatakuwa na hamu ya kutaka kusikiliza ujumbe fulani kuanzia mwanzo hadi mwisho. Vijana wa Kenya, hasa wale wa mitaa duni

ya mijini hupendelea kutumia lugha vipindi. Lugha hizi huwa muhimu kwa makundi husika na hivyo basi wao hufurahia kuisikiza na kuizungumza. Katika kishemu kinachofuata tunaangazia lugha vipindi ya Sheng' ambayo inapendelewa na vijana hasa wa mijini nchini Kenya.

2.5 Lugha Vipindi ya Sheng'

Sheng' ni mojawapo wa lugha vipindi maarufu ambayo inatumiwa katika miji mingi humu nchini. Njoroge (2014) anasema kuwa Sheng' hutumiwa manyumbani, mitaani na hata shuleni jambo ambalo limeifanya lugha hii kukua na kuongezeka kwa watumiaji wake. Maoni haya ya Njoroge yanaonyesha kuwa Sheng' ni lugha ambayo inatumika kwingi. Kutokana na kusambaa kwa Sheng', basi ni muhimu kwa viongozi kuitilia maanani hasa wakati wanatoa taarifa muhimu kwa Wakenya wote kukiwemo inayohusu virusi vya korona. Tunasema hivi kwa sababu inaelekea kuwa lugha hii imepata watumiaji wengi kama ilivyotajwa hapo juu. Kwa hali hii basi, ni muhimu viongozi kufanya uhamasishaji wa umma dhidi ya UVIKO-19 wakitumia lugha hii maarufu hasa katika kuwahasisha vijana kwa kuwa ndio wengi Kenya.

Sheng' ni lugha ambayo inapendelewa na vijana. Vijana hawa huwasiliana kwa kutumia lugha hii. Lugha inayopendelewa na vijana inapaswa pia kutumiwa katika uhamasishaji wao kuhusu masuala ibuka kama vile virusi vya korona ili ujumbe uwafikie kikamilifu. Wasomi kama vile Githiora (2002), Iribemwangi na Mukhwana (2011) na Abdulaziz na Osinde (1997) wanahusisha Sheng' na vijana. Wasomi hawawanasema kuwa vijana wengi mitaani wanatumia Sheng' katika mawasiliano yao na ndio lugha ambayo wanaipendelea zaidi. Ni kwa misingi hii basi ambapo tunasema kuwa serikali inafaa kuwahasisha umma kwa kutumia Sheng' pia. Hii ni kutokana na ukweli kuwa hii ndio lugha ambayo vijana hasa wa mijini wanaienzi. Hivyo basi, kwa kutumia lugha hii ya vipindi vijana wataweza kupata hali halisi kuhusu UVIKO-19 kwa kuwa uhamasishaji unafanywa kwa lugha wanayoipendelea zaidi.

Hata hivyo, Sheng' hutumika kama kitambulisho cha kikundi fulani cha kijamii (Githiora, 2002). Anasema kuwa Sheng' inakuwa lugha muhimu ya mawasiliano ya wanakundi. Wanakundi hutumia Sheng' kuonyesha umoja na kuonyesha wao hufurahia matumizi ya lugha hii. Hii ina maana kuwa Sheng' huenziwa na watu wa kundi husika.

Kwa hali hii basi, ni muhimu kwa serikali kuitilia maanani wanapowahamasisha watu dhidi ya janga la korona. Hii ni muhimu kwa kuwa watu hupenda kusikiza vipindi ambavyo vinatangazwa kwa kutumia lugha wanayoipendelea. Hii inadhihirika kutokana na namna nyimbo zilizoimbwa na Sheng' (Githiora, 2002). Kutokana na maoni ya msomi huyu, ni wazi kuwa Sheng' inapaswa kuzingatiwa katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya virusi vya korona ili kila mtu aweze kuupata ujumbe kupitia kwa lugha anayoipendelea.

Sheng' ni lugha vipindi ambayo msamiati wake hubadilika kila mara. Hii ina maana kuwa lugha hii sio imara kimsamiati. Hii ndio maana inakuwa vigumu kupewa majukumu ya kimawasiliano katika nchi ya Kenya. Bosire (2006) anaiona Sheng' kama lugha chotara na ambayo watumizi wake wamejikita katika mapisi fulani. Watumizi wa Sheng' wanajikita kwa mapisi haya ili kuasi mpangilio wa kijamii katika ngazi kama vile za kiuchumi, kihadhi na kimaeneo. Hii ndio sababu wanatumia lugha ambayo inapinga hali za kiusawa na kwa hali hii basi huwa wamejitenga na wanajamii wengine. Maoni haya ya Bosire yanaonyesha kuwa vijana hupendelea Sheng' katika mawasiliano yao ili kujitenga na jamii pana ya Wakenya. Kwa upande wetu, tunaiona Sheng' kama lugha ambayo huwaunganisha vijana na vile vile huwasaidia katika kuficha siri zao. Kwa hali hii basi, njia pekee ya kuwafikia vijana wanaotumia Sheng' ni kuwahamasisha kuhusu virusi vya korona kwa kutumia lugha wanayoishabikia. Kwa hali hii, serikali itatimiza malengo yake ya kuhakikisha kuwa ujumbe umewafikia vijana pia. Hata hivyo, viongozi wa serikali ya Kenya watabidiika kuwa kama vijana hawa katika matumizi yao ya lugha ya uhamasishaji dhidi ya UVIKO-19.

Isitoshe, wasomi wengine wanadai kuwa Sheng' hutumiwa hata na wazazi. Momanyi (2009) anasema kuwa kutokana na mabadiliko ya katiba, Sheng' inatumiwa na watu wengi Kenya. Anaonyesha kuwa lugha hii inatumiwa na vijana, watoto na hata wazazi ambao wanataka kutumia lugha ambayo watoto wao wanaielewa. Wazazi wanatumia Sheng' ili kuwasiliana na watoto wao kwa kutumia lugha hii wanayoielewa. Hali hii inaonyesha kuwa ni muhimu kutumia lugha ambayo inapendelewa na kundi husika ili kutimiza malengo yao. Matumizi ya lugha inayopendelewa na watu wa kundi fulani ni muhimu katika kufikisha ujumbe ipasavyo. Ni kwa hali hii basi tunasema kuwa ni

vigumu kuepuka kutumia Sheng' katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Suala la matumizi ya Sheng' linafaa kufikiriwa hasa katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Hii ni kwa sababu lugha hii pia ina watumizi wake na ambao wanaienzi. Kwa hali hii basi, serikali itakuwa imefikia makundi yote ya kijamii nchini kama inavyoelezwa katika katiba ya Kenya ya 2010.

Iribemwangi (2020) anasema kuwa Sheng' inatumika katika nyanja mbalimbali za maisha. Anaendelea kusema kuwa Sheng' hutumiwa katika mawasiliano ya watu wa umri mbalimbali kukiwemo wazee hasa jijini Nairobi. Msomi huyu anarejelea lugha ya Sheng' kama mto mkubwa ambao unapata maji yake kutoka kwa mito mingine midogo. Hii inaonyesha kuwa Sheng' imeundwa kutokana na lugha mbalimbali za humu nchini. Anaonyesha kuwa Sheng' hutumiwa na watu wengi nchini katika mawasiliano yao. Sheng' hutumiwa kama mbinu ya mawasiliano ya watu mbalimbali Kenya. Kwa hali hii basi, Iribemwangi anasema kuwa ni vigumu kupuuza Sheng' kama msimbo wa mijini. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa ni muhimu kwa viongozi na vyombo vya habari kuzingatia matumizi yake katika utangaziaji na uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya ugonjwa wa korona.

Tumeshughulikia umuhimu wa lugha mbalimbali katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya korona. Tumeangazia lugha ambazo zimeshughulikiwa katika katiba kama vile Kiswahili na lugha ishara. Vile vile tumeshughulikia Sheng' kwa kuwa ni lugha ambayo pia ina wazungumzaji wengi nchini Kenya. Lugha hizi hutumiwa na viongozi katika uhamasishaji wa Wakenya. Uhamasishaji huu hufanywa kupitia kwa vyombo vya habari na hili ni jambo ambalo huwezesha usambazaji wa ujumbe kwa haraka na kwa watu wengi. Katiba ya Kenya ya 2010 pia imekipa Kiingereza hadhi ya kuwa lugha rasmi. Hii ndio sababu tutaishughulikia lugha hii na zingine za kigeni katika sehemu ifuatayo kwa kuwa ni muhimu kwa wageni kupata ujumbe kwa lugha wanayoielewa.

2.6 Kiingereza na Lugha za Kigeni

Dhima ya lugha yoyote ile ni kukidhi mahitaji ya kimawasiliano katika jamii husika. Zipo lugha ambazo zimevuka mipaka ya kijamii na kuwa lugha inayotumiwa katika mawasiliano ya kimataifa. Kiingereza ni lugha ambayo imevuka mipaka ya kijamii na kuwa ya kimataifa. Kwa mujibu wa Johnson (2013) Kiingereza ndio lugha ambayo

imepewa hadhi ya kuwa lugha rasmi katika mataifa 67. Vile vile, Kiingereza ndio lugha ambayo hutumika katika biashara nyingi za kimataifa na pia hutumiwa kama lugha rasmi ya asasi mbalimbali kama vile Muungano wa Kimataifa. Kiingereza ni lugha rasmi ya pili katika taifa la Kenya ambalo ni miongoni mwa mataifa yaliyo katika Muungano wa Kimataifa. Kwa hali hii basi, serikali inapaswa Kukizingatia katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la korona. Lugha za Kiarabu, Kifaransa na Kihispania pia hutumiwa na mataifa mengi kama lugha rasmi. Ni kwa sababu hii ambapo tunasema kuwa Kiingereza ni lugha ya mawasiliano mapana ulimwenguni. Nchi ya Kenya ina wageni kutoka mataifa mbalimbali kukiwemo China, Uingereza, Korea na Ujerumani. Janga la korona lina athari hasi kwa kila Mkenya bila kuwasaza wageni hawa. Kwa hali hii basi, serikali ya Kenya inapaswa kutilia maanani matumizi ya lugha za kigeni katika uhamasishaji wake dhidi ya janga la korona.

Kiingereza kimekuwa kikitumika kama lugha rasmi ya nchi ya Kenya tangu kupata uhuru hadi wakati ambapo katiba mpya ilizinduliwa. Kiingereza ndicho hutumika katika ufunzaji na utahini wa masomo mengi ikilinganishwa na Kiswahili na lugha zingine za kigeni. Hali hii inaonyesha kuwa Kiingereza ni lugha ambayo imepewa hadhi katika mtaala wa elimu ikilinganishwa na lugha zingine za kigeni. Kiingereza pia kinachukuliwa kuwa lugha ya watu ambao wamesoma huku Kiswahili kikinasibishwa na watu ambao hawajasoma. Maoni yetu ni kuwa Kiingereza kinachukuliwa kuwa lugha bora kutokana na athari za ukoloni nchini Kenya. Hata hivyo, matumizi ya Kiingereza ni muhimu katika uhamasishaji wa umma dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 ili watu wanaoipendelea lugha hii waweze kufikiwa na ujumbe muhimu. Ni muhimu kutaja hapa kuwa idadi kubwa ya viongozi wa Kenya hutumia Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Hali hii hudhihirika zaidi katika mawasiliano ya bungeni ambapo mijadala hujadiliwa kwa lugha ya Kiingereza. Viongozi hawa wa Kenya pia wanatakiwa kuelewa janga la korona kwa kuwa wao ni wawakilishi wa Wakenya walio katika maeneo bunge yao au kaunti zao. Kwa hivyo basi, ni muhimu kwa serikali kutumia lugha ya Kiingereza pia katika uhamasishaji dhidi ya janga la korona ili viongozi pia wawaeleze watu wa jamiilugha zao kwa lugha zao za asili.

Katiba mpya ya 2010 ilikipa Kiswahili hadhi ya kuwa lugha rasmi ya kwanza kikifuatiwa na Kiingereza. Hii ina maana kuwa Wakenya wanapaswa kutumia Kiswahili zaidi katika mawasiliano yao ikilinganishwa na Kiingereza. Ingawa hivyo, nchi ya Kenya ina wageni wa mataifa mengine yasiyotumia Kiswahili katika mawasiliano yao. Kwa hali hii basi, ni muhimu kwa viongozi kutilia maanani lugha za kigeni kukiwemo Kiingereza katika uhamasishaji wa umma dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19. Kwa mujibu wa katiba ya Kenya ya 2010, sura ya 4, kifungu cha 44, kila mtu ana haki ya kutumia lugha katika utamaduni anaoupendelea. Katiba hii ya Kenya ya 2010 inaashiria kuwa inazitambua lugha mbalimbali na kuruhusu matumizi yake katika muktadha faafu. Hii ndio maana tunasema kuwa katiba ya Kenya ya 2010 imeruhusu matumizi ya lugha zingine za kigeni kukiwemo Kichina na Kijerumani. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa viongozi wa Kenya wanapaswa kutilia maanani lugha hizi za kigeni katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la korona. Ingawa hivyo, hali ni tofauti katika uhamasishaji dhidi ya UVIKO-19 nchini Kenya. Tunasema hivi kwa sababu utafiti huu umebaini kuwa lugha za kigeni kama vile Kifaransa hazitumiwi katika uhamasishaji dhidi ya janga la korona.

Lugha za kigeni kama vile Kifaransa na Kijerumani hufunzwa katika baadhi ya shule na vyuo humu nchini. Hii inamaanisha kuwa lugha hizi zinatambulika katika mtaala wa elimu na bila shaka katika nchi ya Kenya. Kwa hali hii basi, lugha za kigeni ni muhimu kama zilivyo lugha za asili, Kiswahili na Kiingereza katika uhamasishaji wa ugonjwa wa korona. Hii ni kwa sababu ugonjwa wa korona ni janga la kimataifa na hivyo basi kila mtu anapaswa kuchukua jukumu la kuzuia maambukizi na vifo zaidi. Hii ndio maana tunasema kuwa ni muhimu kwa serikali kutilia maanani lugha mbalimbali kukiwemo za kigeni katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la korona. Ingekuwa muhimu kwa vyombo vya habari kutilia maanani matumizi ya lugha za kigeni kama vile Kichina katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la korona. Hii ni kwa sababu vyombo vya habari ni muhimu katika usambazaji wa ujumbe. Hii ndio maana tunashughulikia uhamasishaji na utangazaji katika kishemu kifuatacho ili kuonyesha umuhimu wake katika kupambana na janga la korona kwa nia ya kuonyesha mchango wake katika uhamasishaji wa ugonjwa huu.

2.7 Uhamasishaji na Utangazaji Kuhusiana na UVIKO-19 Kenya

Utangazaji hufanywa kupitia vyombo vya habari. Vyombo vya habari ni muhimu katika uhamasishaji wa Wakenya. Hii ni kwa sababu vyombo vya habari huwafikia watu wengi nchini Kenya na ulimwenguni kote kwa jumla. Uhamasishaji umelezwa na Bowen (2006) kama mbinu ya kuwafanya watu wa kundi fulani au umma kuelewa jambo fulani. Anasema kuwa uhamasishaji ni muhimu katika kuwafanya watu kupata hali halisi kuhusu jambo fulani. Kulingana na Bowen. Uhamasishaji hufanywa kwa nia ya: kupata taarifa kamili na sahihi, kubadilisha mtazamo wa watu kuhusu jambo fulani, kuwapa watu mbinu za kubadilisha hali fulani waliyokuwa wameizoea na vile vile kujua namna ya kusaidia au mahali pa kupata msaada wakati wa janga fulani. Madai ya Bowen yanaonyesha kuwa uhamasishaji ni muhimu hasa wakati wa janga ambalo linaathiri watu wengi kama hili la UVIKO-19. Kwa hali hii, uhamasishaji hufanywa ili kuwafanya watu kupata uelewa wa uhalisia wa mambo. Uhamasishaji pia huhusisha kuwaeleza watu namna ya kupambana na janga husika na katika muktadha wa utafiti huu janga la virusi vya korona.

Utafiti huu unahusu sera ya lugha na utangazaji kuhusu janga la korona nchini Kenya nia ikiwa ni kuwahamasisha umma dhidi yake. Serikali ina jukumu la kuwahamasisha Wakenya dhidi ya UVIKO-19 ili kupunguza maambukizi na vifo zaidi. Janga la korona limeathiri sekta mbalimbali kama vile uchukuzi, biashara na elimu. Hali hii inarudisha uchumi wa nchi nyuma. Hii ndio sababu ni muhimu kwa serikali kuwahamasisha Wakenya kwa kuwaeleza athari za ugonjwa huu na namna ya kuzuia maambukizi na vifo zaidi. Uhamasishaji unafanywa ili kujumuisha watu wote katika vita dhidi ya janga hili. Lugha itakayotumiwa katika uhamasishaji ni muhimu na ndio maana serikali inafaa kuzingatia majukumu ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya nchi ili ujumbe uweze kuwafikia Wakenya wote.

Matumizi ya lugha kikatiba nchini isipozingatiwa ipasavyo basi juhudi za serikali za kuhamasisha Wakenya dhidi ya majanga kama korona zitapata vikwazo. Watu wengine hawatafikiwa na ujumbe sahihi kwa kutoelewa lugha inayotumiwa. Vyombo vya habari pia vinapaswa kutilia maanani majukumu ya lugha kikatiba katika utangazaji wake kufuatia hali hii. Kandagor (2012) anasema kuwa vyombo vya habari hutoa huduma

mbalimbali kukiwemo, kujuza, kufundisha, kuburudisha na kuelimisha. Kwa hali hii basi, vyombo vya habari ni muhimu katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Njia ya kufikisha ujumbe ni kupitia kwa matumizi ya lugha ambayo inaeleweka na Wakenya wote. Hapa basi, lugha ya taifa, lugha rasmi, lugha ishara, lugha za asili na Sheng' mbali na lugha za kigeni ambazo wageni walio Kenya watapendelea kimawasiliano zinapaswa kutumiwa. Matumizi ya lugha hizi katika utangazaji kuhusu janga la korona yatahakikisha kuwa ujumbe umewafikia Wakenya wote kwa kuwa taarifa itakuwa imetolewa kwa lugha wanayoielewa.

Kutoa na kupokea habari kwa lugha anayoipendelea mhusika kunatambuliwa duniani kote kama moja ya haki za binadamu. Vyombo vya habari huchangia katika kuinusuru jamii kutokana na majanga kama vile magonjwa na vita. Hata hivyo, baadhi ya wananchi hawapati habari kupitia kwa vyombo vya habari kwa kuwa maeneo mengine nchini hayana miundombinu ya mawasiliano (Musau, 2001). Hii ina maana kuwa wapo Wakenya wasiofikiwa na taarifa za habari. Kwa hali hii basi, haki yao ya binadamu inakiukwa. Utangazaji kuhusu janga la korona umekuwa ukifanywa na viongozi kupitia kwa vyombo mbalimbali vya habari. Hata hivyo, ukosefu wa miundombinu ya mawasiliano katika baadhi ya maeneo basi unaonyesha kuwa wapo watu ambao hawatapata habari kuhusu janga hili la korona. Kwa hivyo wapo Wakenya ambao hawatajua kuhusu virusi vya korona, athari zake wala namna ya kujikinga. Hii inaashiria kuwa utangazaji kuhusu janga fulani unapaswa kufanywa kwa namna ambayo habari itawafikia Wakenya wote kupitia lugha wanazozichangamkia ili kupambana nalo kwa pamoja.

2.8 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangazia majukumu ya lugha mbalimbali kama yalivyoelezwa katika katiba ya Kenya ya 2010. Tumeshughulikia sera ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010. Tumeonyesha kuwa serikali inafaa kuzingatia majukumu ya lugha kwa mujibu wa katiba ya nchi katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la korona. Tumeonyesha kuwa katiba ya Kenya inazitambua lugha ya Kiswahili, Kiingereza, lugha za asili, lugha ishara, lugha vipindi na hata lugha za kigeni. Vile vile tumeonyesha kuwa ni muhimu kwa uhamasishaji kufanywa pia kwa kutumia lugha

vipindi ya Sheng' kwa kuwa inashabikiwa sana na vijana hasa wa mitaa mbalimbali mijini.

Viongozi basi wanapaswa kutekeleza katiba ya Kenya katika utangazaji wa uhamasishaji dhidi ya janga la korona. Hili litapelekea Wakenya wengi kupata habari muhinu kuhusu virusi vya korona na athari zake na hatimaye kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi hivi. Kwa kufanya hivi, maambukizi yatapungua. Hii ni kwa sababu watu watapata habari kupitia kwa lugha ambayo wanaishabikia. Hali hii inatuwezesha kushughulikia nafasi ya lugha hizi na athari zake katika utangazaji na uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya virusi vya korona katika sura inayofuatia.

SURA YA TATU

LUGHA YA UTANGAZIAJI NA UHAMASISHAJI DHIDI YA UVIKO-19

3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili ya utafiti huu, tumeshughulikia majukumu ya lugha mbalimbali zipatikanazo Kenya kwa mujibu wa katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010. Tumeonyesha kuwa Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi Kenya ikifuatiwa na Kiingereza kama lugha rasmi ya pili. Kiswahili pia ni lugha ya taifa nchini Kenya. Vile vile, tumeonyesha kuwa katiba ya Kenya ya 2010 inazitambua lugha ishara na lugha za asili nchini humo. Tumeonyesha pia kuwa Sheng' ni lugha inayochangamkiwa na vijana wa humu nchini. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa viongozi wa Kenya wanapaswa kutilia maanani matumizi ya lugha hizi zote wanapohamasisha umma dhidi ya janga la corona. Katika sura hii, tunashughulikia athari za lugha ya utangazaji na uhamasishaji dhidi ya UVIKO-19 kwa umma wa Kenya.

Ujumbe unaotolewa na viongozi katika kuwahamasisha Wakenya dhidi ya UVIKO-19 wanapotumia lugha inaweza kuleta athari hasi au chanya na kuchangia upokeaji wa ujumbe ulio sahihi au usiokuwa sahihi. Katika hali kama hii, lugha itakuwa imetumika kama chombo cha kusahilisha au kutosahilisha mawasiliano yahasuyo virusi vya korona kwa umma wa Kenya. Nadharia ya uhusiano na ile ya utekelezaji inatuwezesha kuainisha athari za lugha tumizi katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Ni vyema kusema hapa kuwa kanuni za uhusiano ambazo zinahusisha matumizi ya lugha kutegemea muktadha ni muhimu katika kuwawezesha viongozi na vyombo vya habari kuzingatia mihimili ya nadharia ya utekelezaji kwa kuzingatia majukumu ya lugha kulingana na katiba ya Kenya. Mihimili ya nadharia hizi itatuongoza katika kuchanganua athari za lugha ya utangazaji na uhamasishaji dhidi ya janga la korona katika sehemu ifuatayo.

3.2 Tathmini Ya Lugha Ya Utangazaji Na Uhamasishaji Dhidi Ya UVIKO-19

Kwa mujibu wa nadharia ya utekelezaji, lugha mbalimbali huwa na uamilifu mahsusi katika jamii. Hivyo basi, lugha chini Kenya zinapaswa kutumiwa kulingana na majukumu yake kutegemea katiba ya nchi hiyo. Uteuzi na matumizi ya lugha ya

utangazaji ni muhimu katika kufanikisha uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la korona nchini Kenya. Kikabila, watu hupenda kusikiza matangazo na taarifa zinazopeperushwa kutumia lugha wanayoienzi. Ili kufanikisha uhamasishaji kuhusu jambo fulani katika jamii basi, ni muhimu kutilia maanani matumizi ya lugha hizi na katika muktadha huu lugha za Kenya. Katika sehemu hii, tunashughulikia tathmini ya lugha za utangazaji katika uhamasishaji wa umma wa Kenya dhidi ya janga la korona. Tunashughulikia athari hasi na chanya zitokanazo na lugha za uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya virusi vya korona katika sehemu hii. Athari hizi tunazishughulikia kwa kuangazia mazungumzo ya viongozi kuhusu janga la korona nchini humo. Tutajikita kwa lugha wanazozitumia viongozi na namna wanavyozitumia wanapowahamasisha Wakenya dhidi ya janga la korona.

3.2.1 Kufasiri Ujumbe Visivyo

Wasemaji wanapotoa ujumbe, hutaka kueleweka na wasikilizaji ambao hupaswa kuchukua hatua mwafaka. Hii ina maana kuwa wasemaji wanapaswa kutumia lugha ambayo itaeleweka na wasikilizaji ili waweze kuchukua hatua iliyokusudiwa. Wakati mwingine, wasikilizaji hufasiri ujumbe wa wasemaji visivyo na hivyo basi kuchukua hatua kinyume na ilivyokusudiwa na wasemaji. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa wasemaji wanapaswa kuzingatia mawasiliano mema kwa kutumia lugha ambayo itaeleweka na ambayo haina utata wowote. Katika mawasiliano mema, msemaji anapaswa kutoa maelezo zaidi kwa usemi ambao una utata ili wasemewa waweze kuuelewa ujumbe ipasavyo (Franco na Galvis, 2013). Hii ina maana kuwa msemaji anapaswa kutoa maelezo ya ziada ili kuondoa utata husika. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa maelezo ya ziada ni muhimu kwa kuwa ujumbe hufasiriwa ipasavyo.

Kufasiri ujumbe visivyo ni hali ya kuelewa ujumbe kwa namna tofauti na alichokusudia msemaji. Hii ni athari hasi inayotokana na matumizi ya lugha bila kuzingatia makundi yote ya kijamii. Tulibaini kuwa viongozi wa Kenya hupendelea kutumia Kiingereza wanapozungumzia suala la virusi vya korona. Hii ni kinyume na majukumu ya lugha mbalimbali kama inavyodhihirika katika katiba ya Kenya. Ikumbukwe kuwa ugonjwa wa korona ni janga la kitaifa na kimataifa na hivyo basi ni muhimu kwa viongozi kuzingatia matumizi ya lugha kikatiba nchini Kenya ili Wakenya wapate ujumbe na kuufasiri

ipasavyo. Kesi ya kwanza ya mwathiriwa wa virusi vya korona nchini Kenya iliripotiwa tarehe 13, Machi, 2020. Waziri wa afya Mutahi Kagwe ndiye aliyezungumzia kuzuka kwa korona nchini Kenya. Waziri Kagwe alitumia Kiingereza alipokuwa akitoa hotuba kwa taifa kuhusiana na virusi vya korona. Hotuba yake ilinuia kuelezea kuhusu virusi vya korona kwa kuwaeleza Wakenya namna virusi hivi husambaa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Virusi hivi vilikuwa vipya na hivyo Wizara ya Afya chini ya uongozi wa Waziri Kagwe, walitakiwa kuwahamasisha Wakenya. Uhamasishaji huu ulihusu namna ya kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya maambukizi zaidi ya virusi vya korona. Hivyo basi, Waziri Kagwe alipaswa kutumia lugha ambayo ingeeleweka na Wakenya wote. Ingawa hivyo, Kagwe alitumia Kiingereza katika hotuba yake na hili ni jambo ambalo linaweza kusababisha Wakenya kufasiri ujumbe visivyo hasa kwa wale ambao hawajasoma. Kwa hali hii, Kiongozi huyu alikiuka katiba ya Kenya hasa mwanzoni mwa msambao wa virusi hivi kwa kutotumia lugha ya taifa. Tunasema hivi kwa sababu Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi kulingana na katiba ya Kenya na vile vile lugha ya taifa. Hii ndio lugha inaunganisha Wakenya wote bila kujali hali zao za elimu, tabaka au masiala mengine ya kijamii.

Athari hasi za lugha inayotumiwa katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona ilijitokeza katika hotuba ya kwanza ya Waziri wa Afya, Bwana Kagwe. Athari hii ni kufasiri ujumbe visivyo. Hotuba ya Waziri Kagwe ya tarehe 13, Machi 2020 ilitolewa kwa Kiingereza katika vyombo mbalimbali vya habari. Hotuba hii ilinuia kuelezea hali ya ugonjwa wa UVIKO-19 nchini na kuwahamasisha Wakenya kwa kuwaelezea athari na msambao wake. Siku hiyo Waziri wa Afya alisema yafuatao kwa Kiingereza:

“First corona virus case in Kenya was confirmed as at 12th night since the outbreak in China. Kenyan Citizen to Nairobi from U.S.A via London on 5th March, 2020 has been confirmed by National Influenza Laboratory M.O.H. However the patient is stable, the temperatures are normal, she is eating but has not been released until the test continues till the test becomes negative. The lady is okay. Therefore there is no need for alarm. The government through the Ministry of Health will strengthen the measures to ensure no more transmission. The health response committee took the strategies on governments approach and implementation of this measure to increase capacity on facilities and how to respond.Observe the following: regular wash hands or use a sanitizer, maintain 1.5 metre distance between

yourself and others, maintain good respiratory hygiene, cough with a tissue, handkerchief or flexed elbow and suspend all public gatherings.”Hapa chini

ni tafsiri yake kwa Kiswahili:

(Kisa cha kwanza cha virusi vya korona kiliripotiwa usiku wa tarehe 12 tangu kuzuka kwa virusi hivi nchini Uchina. Mkenya mmoja alisafiri kutoka U.S.A kupitia London tarehe 5 Machi, 2020 amethibitishwa kuwa na virusi hivyo na maabara ya kitaifa ya magonjwa ya kuambukizana. Ingawa hivyo, mgonjwa yuko sawa, kiwango joto ni sawa, anakula hataruhusiwa kutoka hadi vipimo vionyeshe kuwa hana virusi vya corona. Mwanadada yuko sawa hivyo msiwe na hofu sana. Serikali kupitia kwa Wizara ya Afya itachukua jukumu la kupunguza maambukizi zaidi. Kamati ya Afya inayoshughulikia mikakati ya kukabiliana na kutekeleza mikakati iliyowekwa na serikali inapania kuongeza asasi za afya na namna ya kukabiliana na janga hili..... zingatia yafuatayo: nawa mikono kila wakati au tumia sanitiza, kaa umbali wa 1.5 na mwenzako, kohoa kwa kutumia shashi na pia hakuna mikutano).

Waziri wa Afya anaelezea hali ya janga la korona nchini Kenya kwa kutumia lugha ya Kiingereza ambayo ni lugha ya pili rasmi kwa mujibu wa katiba ya Kenya. Hii ni baada ya kisa cha kwanza kuripotiwa nchini. Waziri alinua kuwahamasisha Wakenya dhidi ya virusi vya korona ambavyo husambaa kwa haraka miongoni mwa watu. Waziri alikuwa na jukumu la kuwaelezea Wakenya kuhusu virusi vya korona ili waweze kujua athari na namna ya kupunguza maambukizi zaidi. Hii ni baada ya kujua namna ugonjwa huu uliwahangaisha Wachina na watu wa mataifa mengine yenye uwezo mkubwa wa kiuchumi. Ni kwa misingi hii ambapo Waziri alitaka Wakenya kufuata masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya ili wasijipate katika hali sawa na ile ya Uchina na mataifa mengine. Waziri ametumia Kiingereza (ambacho ni lugha ya pili rasmi kulingana na katiba) katika hotuba yake ya kwanza ya kuwaeleza Wakenya kuhusiana na janga la korona. Ni muhimu kutaja hapa kuwa hii ilikuwa hotuba muhimu kwa Wakenya ambao walikuwa na hofu kuhusiana na janga hili na hivyo walitakiwa kuelewa kila kitu kuhusu virusi hivi vya korona. Kwa maoni yetu, ingekuwa bora kama Waziri wa Afya angezingatia hadhi ya lugha kulingana na katiba ya Kenya katika hotuba yake ya kwanza ya uhamasishaji dhidi ya janga la korona. Tunasema hivi kwa sababu Wakenya walitakiwa kuchukua hatua na kufuata masharti mapya yaliyoniwa kupunguza msambao zaidi wa virusi vya korona. Kwa hali hii basi, Waziri alitakiwa kuzingatia lugha ambayo

ingeeleweka na Wakenya wa matabaka yote. Hili lingewezekana kama angezingatia matumizi ya lugha kwa mujibu wa katiba ya nchi ya Kenya.

Kiswahili kingekuwa lugha mwafaka ya kutoa hotuba hii ya kwanza kwani ilikuwa muhimu kwa Wakenya ambao walitakiwa kutimiza masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya. Hii ni kwa sababu Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi kwa mujibu wa katiba na vile vile ni lugha ya taifa. Tunasema kuwa Kiswahili kingekuwa mwafaka kwa kuwa ni muhimu kwa umma kuelewa uzito wa jambo fulani ili kuchukua hatua zifaazo. Tuliwahoji Wakenya kwa kutaka kujua walichoelewa kutokana na hotuba ya kwanza ya Waziri Kagwe ili kujua athari ya kutoa hotuba kwa kutumia Kiingereza kwa Wakenya. Tuliwahoji Wakenya namna walivyopokea ujumbe wa Kagwe kutokana na kipengele hiki cha hotuba yake, **“However the patient is stable, the temperatures are normal, she is eating but has not been released until the test continues till the test becomes negative. The lady is okay. Therefore there is no need for alarm.”** Tuliwahoji Wakenya watatu wa Utawala, eneo la Lexo walisema yafuatayo:

1. M1: **Mi chenye najua, hiyo time alikuwa anamaanisha kuwa korona sio mbaya sana Kenya.**
2. Mtafiti: **Mbona unasema hivyo?**
3. M1: **Si alisema no cause for alarm** (*tusiwe na wasiwasi*).
4. M2: **Hiyo kitu alisema ilimaanisha kuwa hii ugonjwa iko na dawa. Kaa huyo mtu wa kwanza alipona, basi hata mwenye atashikwa nayo atapona tu.**
5. M3: **Hiyo tu inamaanisha kuwa tusijali as in** (*kwa kuwa*) **hii ugonjwa si hatari sana.**

Katika mazungumzo haya, ni wazi kuwa Watafitiwa hawajachukulia janga la korona kwa uzito unaofaa. Kutokana na maoni ya watafitiwa hawa ni wazi kuwa walifasiri kipengele hiki cha hotuba ya Waziri Kagwe visivyo. Hii inajitokeza kwa kuwa Waziri alitumia Kiingereza na hili ni jambo ambalo liliwafanya Wakenya kudhani kuwa ugonjwa wa korona haukuwa hatari sana. Hii ni athari hasi kwa kuwa Wakenya wanakosa kuuchukulia ugonjwa wa UVIKO-19 kwa uzito unaofaa. Hali hii inasababishwa na ukiukaji wa majukumu ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya. Hii ilikuwa hotuba ya kwanza na ambayo ilinuiwa kuwaeleza Wakenya kuwa virusi vya korona vilikuwa

vimefika nchini na hivyo walipaswa kuchukua tahadhari kama taifa. Waziri Kagwe anatumia Kiingereza ambacho ni lugha ya pili rasmi kulingana na katiba ya nchi. Kiongozi huyu anakipuuza Kiswahili ambacho ni lugha ya taifa nchini na vile vile ni lugha rasmi ya kwanza kwa mujibu wa katiba. Hivyo basi, Kiswahili kingekuwa lugha mwafaka kwa kuwa kingeleweka na Wakenya zaidi ikilinganishwa na Kiingereza.

Ukiukaji huu wa katiba ya Kenya kilugha unawaathiri Wakenya kwa njia hasi na ndio sababu wanafasiri ujumbe visivyo. Kwa hali hii, Wakenya wanaelekea kuamini kuwa virusi vya korona sio hatari kutokana na yale aliyoyasema Kagwe. Viongozi wanatumia lugha ya Kiingereza ambayo kwa mujibu wa Githiora (2002) ni lugha inayotumiwa katika biashara kubwa kubwa, elimu ya juu na vile vile bungeni. Hii inaonyesha kuwa Kiingereza kinaeleweka na watu waliosoma na walio na kazi au biashara kubwa. Kwa hali hii basi, Wakenya wengine walio na kisomo kidogo na biashara ndogo ndogo huwa hawatumii Kiingereza katika mawasiliano yao. Hii vile vile inaashiria kuwa basi hawapendelei kutumia au kusikiliza watu wanaozungumza kwa Kiingereza. Tulibaini hili pia kutokana na mazungumzo ya watafitiwa wa eneo la Utawala ambao wanasema kuwa Kiingereza kinachukuliwa kuwa lugha ya watu waliosoma huku Kiswahili kikidunishwa na hawa wasomi kuwa lugha ya watu ambao hawajasoma.

Githiora (2002) anasema kuwa Kiswahili ni lugha sambazi nchini Kenya. Hii ina maana kuwa Kiswahili ndio lugha inayotumika kwingi na watu wa matabaka mbalimbali. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa Kiswahili kingekuwa mwafaka katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Hii ni kwa sababu virusi hivi huathiri watu wote bila kubagua kwa misingi ya kiwango cha elimu au uwezo wa kiuchumi. Hali ya kufasiri ujumbe visivyo ilidhihirika pia katika hotuba ifuatayo ya Rais Kenyatta ya tarehe 15, Machi, 2020:

“.....The government has set containment protocols in the country resulting from 2 additional cases and thus directing additional protocols. The government suspends travel from outside countries with cases,.....Where possible, government offices, businesses, companies allow people to work from home except in critical services. To avoid risk of transmission through physical handling of money use cashless transfers, take note of such situations to reduce cost of transactions....”Tafsiri ya

ujumbe huu ni kama ifuatavyo: *(Serikali imeweka mikakati ya kupunguza maambukizi zaidi baada ya visa vingine viwili vya korona kuripotiwa na hivyo tutaongeza mikakati zaidi. Serikali imesitisha safari zote kutoka kwa mataifa ya nje ambayo tayari yameripoti korona. Ikiwezekana, ofisi za serikali, biashara na makampuni waruhusu watu wafanyie kazi nyumbani isipokuwa kwa huduma za dharura. Ili kupunguza maambukizi yatokanoyo na kubadilishana pesa, asasi husika wazia namna ya kupunguza ada).*

Rais ametumia Kiingereza anapowaeleza Wakenya kuhusiana na mikakati ambayo imewekwa na serikali kwa nia ya kupunguza maambukizi zaidi baina ya watu. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa Rais alikiuka katiba ya Kenya ambayo imekiorodhesha Kiswahili kama lugha ya kwanza rasmi kikifuatiwa na Kiingereza. Mtafiti alitaka kujua namna Wakenya waliupokea ujumbe wa Rais kwa kuwahoji wakaazi wa eneo la Pipeline, Embakasi. Wakaazi wa Pipeline walidhihirisha kuwa matumizi ya Kiingereza katika kuwahamasisha Wakenya dhidi ya janga la korona huweza kufasiriwa visivyo. Mtafiti aliteua kipengele kifuatacho cha mazungumzo ya Rais kwa nia ya kujua namna watu wa Pipeline walivyofasiri ujumbe wake: “.....**Where possible, government offices, businesses, companies allow people to work from home except in critical services. To avoid risk of transmission through physical handling of money use cashless transfers, take note of such situations to reduce cost of transactions....**”

1. Mtafiti: **Rais amesema kuwa watu wafanye kazi wakiwa nyumbani ili kuzuia maambukizi, kutokana na kipengele hiki wewe umelewa nini?**
2. M1: **Sasa anasema tufanyie kazi home aje sasa hivo?**
3. M2: **Ati critical services ni gani tena? Hata hii yangu ya kuuza matunda ni critical ala.**
4. M1: **Imagine hii kitu ya kuwork from home haiwes make kwa mahustler kama sisi. Juu ni lazima tukatafutie familia kila siku.**
5. Mtafiti: **Na wewe mama umelewa nini kutokana na hii mambo ya kukaa nyumbani isipokuwa tu watu wa critical services?**
6. M3: **Sasa wee ukiona tutakula nini tukikaa nyumbani au watatupea food sisi wote? Hii serikali ina mambo haki.**

Mazungumzo ya Wakenya hawa wa Pipeline yanaonyesha kuwa hawajaelewa maana ya usemi ‘*critical services*’. Watafitiwa hawa wa eneo la Pipeline ni wauzaji wa matunda na mboga. Katika hali halisi mboga na matunda ni miongoni mwa bidhaa muhimu ambazo haziwezi kusitishwa. Kutokana na usemi wa watafitiwa hawa ni wazi kuwa hawaelewi kuwa biashara waifanyayo pia ni muhimu kwa kuwa chakula pia ni bidhaa muhimu. Hali hii inajitokeza katika usemi wa M3 ambaye anasema kuwa “**Sasa wee ukiona tutakula nini tukikaa nyumbani au watatupea food sisi wote? Hii serikali ina mambo haki.**” Usemi wa mtafitiwa huu unaonyesha kuwa hajui kuwa biashara yake ya kuuza mboga ni muhimu na hivyo haiwezi kusitishwa. Kwa upande mwingine, M2 anaashiria kuwa anaelewa kuwa biashara yake pia ni huduma muhimu na hivyo haifai kusitishwa. Ingawa hivyo, anasema hili kimzaha kama inavyojitokeza katika usemi wake anaposema kuwa “**Ati critical services ni gani tena? Hata hii yangu ya kuuza matunda ni critical ala.**” Maneno yake yanaonyesha kuwa anafanya mzaha anaposema kuwa hata biashara yake ni huduma muhimu hali inayoonyesha kuwa amefasiri usemi wa Rais visivyo.

Usemi wa watafitiwa hawa pia unaonyesha kuwa hawajaelewa uzito wa janga hili la korona. Kwao, wanaona kuwa ni muhimu kuendelea na biashara zao kama kawaida. Hii ni kinyume na mikakati iliyowekwa na Wizara ya Afya ambayo inawataka Wakenya kuzuia maambukizi zaidi ya korona kwa kupunguza usafiri kutoka kwa eneo moja au lingine. Kwao, wanaonyesha kuwa kazi kwanza kwa kuwa hawana pengine pa kutoa kipato. Haya yanadhihirika katika usemi wa M1 anaposema kuwa “**Juu ni lazima tukatafutie familia kila siku.**” Usemi huu unadhihirisha kuwa hawakubaliani na maoni ya serikali ya kuwataka kukaa nyumbani ili kupunguza maambukizi zaidi. Ufasiri huu unatokana na ukweli kuwa Rais alikiuka katiba ya Kenya kilugha kwa kutumia Kiingereza katika mawasiliano yake badala ya kutumia Kiswahili ambacho ni lugha ya taifa na sambazi nchini Kenya. Rais angetumia neno la Kiswahili kurejelea *critical services*, angeeleweka maana angesema huduma muhimu na angelazimika kutoa mifano ili kueleweka zaidi.

Nadharia ya uhusiano inadai kuwa msemaji anapaswa kutoa maelezo zaidi iwapo ujumbe hauieleweki vyema. Kwa mfano, viongozi walipaswa kuelezea huduma ambazo wanazirejelea kama *critical services* na ambazo zinahusisha vyakula na dawa. Hivi basi, watafitiwa wetu wangeelewa kuwa biashara yao pia ni huduma muhimu. Watafitiwa

wanakosa kuchukua hatua faafu kwa kuufasiri ujumbe wa Rais visivyo. Athari hasi inajitokeza kwa kuwa Rais anakosa kutoa maelezo zaidi kuhusiana na huduma anazoziita za muhimu. Athari hii hasi ndio inawafanya watafitiwa kuchukulia kuwa wanapewa adhabu na serikali ilhali viongozi wanataka kuokoa maisha ya Wakenya dhidi ya ugonjwa wa korona. Hali hii inawafanya watafitiwa kutofuata masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya ya kupunguza msambao wa virusi vya korona.

Usemi wa watafitiwa hawa unaonyesha kuwa serikali haijafaulu katika kuwahamasisha Wakenya dhidi ya janga. Hii ni kwa sababu viongozi wamepuza lugha kikatiba na hili ni jambo ambalo linazua athari hasi kutokana na hali ya kukiuka masharti ya kuzuia msambao zaidi wa virusi vya korona. Tumeonyesha kuwa viongozi wanatumia Kiingereza kuwahamasisha Wakenya jambo ambalo linawafanya kufasiri ujumbe visivyo. Kulingana na nadharia ya uhusiano, msemaji anapaswa kusema ujumbe kwa namna inayoeleweka na ambao ni rahisi kufasiriwa na wasemewa. Hali hii haijitokezi katika mazungumzo ya viongozi ambao wanawahamasisha Wakenya dhidi ya janga la korona. Usemi wa Katibu wa kudumu, bwana Kibicho wa Machi tarehe 22, 2020 pia ulifasiriwa visivyo na Wakenya wa Katani, kaunti ndogo ya Athi River. Kibicho alisema,

“.... Measures may be inconvenient but are necessary but can meet the objective of keeping Kenyans safe.... This is not a joke, in the coming weeks, its important to enforce government measures like no gathering within the streets..... Stay at home.....People are getting sick through contacts with tourists who have been to bars and hotels. We don’t know who is sick, this is not business as usual.”*(Mikakati ambayo imewekwa na serikali sio faafu kwa Wakenya ila itatuwezesha kutimiza malengo ya kuwakinga. Ugonjwa huu sio mchezo, majuma yajayo serikali itahakikisha kuwa Wakenya wamefuata kanuni zilizowekwa kama vile hamna mikutano. Kaa nyumbani, watu wanaupata huu ugonjwa kupitia maingiliano baina yao na watalii ambao huenda kwenye mabaa na mikahawa. Hatujui ambaye ana virusi hivi, hali sio kama kawaida.)*

Mtafiti aliwahoji wakaazi wa Katani kuhusiana na usemi huu wa Katibu wa kudumu, bwana Kibicho na walikuwa na haya ya kusema:

1. M1: **Mzee anamaanisha kuwa matourist ndio wako na hii virusi. So mimi hata siwezi pata nikiwa hapa mashamba.**

2. M2: **Hata yeye anajua kuwa hii ugonjwa ni ya masos, kwani sisi huenda hizo bar na mahoteli wanaenda, hapana sisi hapa katani hakuna hiyo ugonjwa.**
3. M3: **Kwanza wewe nikuulize, umeona corona kweli, au kuna mtu wenu ako na korona? Serikali inatuchesa tu ipate doo kutoka ng'ambo.**
4. M4: **Mi najua hakuna korona na hata hiyo stori hainibambi juu tunacheswa kaa watoi wakubwa wakiunda pesa.**

Usemi wa Watafitiwa hawa unaonyesha wazi kuwa wamefasiri ujumbe wa Bwana Kibicho visivyo. Kibicho alinua kuwahakikishia Wakenya kuwa virusi vya korona vipo na vinasambaa kwa haraka. Alitaka kuonyesha umuhimu wa kukaa nyumbani iwapo mtu hana shughuli ya lazima itakayomfanya aende mjini au mtaani. Kibicho alitaka Wakenya wajue kuwa huwezi kujua yule ambaye ni mgonjwa. Haya yanadhihirika katika usemi wake anaposema kuwa **“We don’t know who is sick, this is not business as usual.”** Usemi huu ni wazi kuwa ni vigumu kujua mtu aliye na virusi hivi na akataka kuwahamasisha watu dhidi ya kutangamana ovyo ili kupunguza maambukizi. Hata hivyo, Wanakatani wanakuwa na maoni tofauti kabisa na usemi wa Kibicho. Kibicho anasema kuwa hata watalii wako na virusi hivi. Anasema hivi kuonyesha kuwa virusi hivi vinaathiri kila mtu na wala hakuna anayesazwa hata watalii. Ingawa hivyo, M2 anafasiri usemi huu visivyo kwa kusema kuwa ugonjwa wa korona ni wa matajiri. Hili linadhihirika anaposema kuwa **“Hata yeye anajua kuwa hii ugonjwa ni ya masos.”** Hali hii ni mfano wa athari hasi inayotokana na kupuuza sera ya lugha ya Kenya jambo ambalo ni hatari kwa kuwa masharti yatapuuzwa na Wakenya wanaoufasiri ujumbe visivyo.

Kibicho anatumia Kiingereza katika kuwaeleza Wakenya kuhusu janga la korona. Kulingana na nadharia ya Uhusiano, msemaji anapaswa kutoa maelezo zaidi kwa usemi ambao unahitaji maelezo haya ili wasikilizaji waweze kuuelewa ujumbe kama alivyokusudia. Kanuni nyingine ya nadharia ya uhusiano ni kuwa msemaji atoe ujumbe ambao ni rahisi kufasiri. Haya ndio mambo yanayokosekana katika usemi wa Kibicho ambao unalenga kuwahamasisha Wakenya dhidi ya janga la korona. Ukiukaji wa kanuni hizi, unawafanya Wakenya kufasiri ujumbe visivyo kama inavyojitokeza katika usemi wa M3 na M4 ambao hawaamini kuwa kuna ugonjwa wa korona. Kulingana nao, serikali

inatumia janga la korona kupata msaada kutoka mataifa ya nje. Matumizi ya lugha ya Kiingereza yanawafanya Wakenya kufasiri ujumbe visivyo na hata kuchukulia kuwa hakuna ugonjwa wa korona kama inavyotangazwa na vyombo vya habari na viongozi. Haya yanadhihirika M3 anaposema kuwa “**Kwanza wewe nikuulize, umeona korona kweli, au kuna mtu wenu ako na corona? Serikali inatuchesa tu ipate doo kutoka ng’ambo.**” Hali hii ni hatari kwa kuwa Wakenya wataendelea na shughuli zao za kawaida bila kujali kwa kuwa wanaamini kuwa hakuna virusi vya korona. Msambao wa virusi vya korona utaongezeka na kusababisha vifo zaidi kutokana na hali ya kupuuza katiba ya Kenya kilugha.

Watafitiwa hawa wanaonyesha wazi kuwa wanafasiri ujumbe wa Kibicho visivyo. Sababu kuu inayowafanya Wakenya kufasiri ujumbe visivyo ni viongozi kukosa kuzingatia majukumu ya lugha kikatiba. Pia viongozi hawa hawatoi maelezo zaidi kuhusu yale wanayoyasema. Badala yake, wanabana ujumbe jambo ambalo linawafanya Wakenya kufasiri ujumbe visivyo. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa viongozi wanakosa kuzingatia kanuni za nadharia ya uhusiano kukiwemo kutoa maelezo zaidi kwa baadhi ya semi au kutoa usemi ambao ni rahisi kufasiriwa. Hali hii inawafanya Wakenya kutofuata masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya na hivyo basi nia ya uhamasishaji dhidi ya janga la korona inakosa kuafikiwa.

Tumeonyesha namna Wakenya wanafasiri usemi wa viongozi visivyo kwa kuwa wanakosa kuzingatia katiba ya Kenya, hali inayozua athari hasi na kupelekea Wakenya kupuuza masharti ya kuzuia msambao wa virusi vya korona. Vile vile, tumeonyesha kuwa viongozi hawatoi maelezo ya ziada kuhusu virusi vya korona ambayo yatawafanya Wakenya kuuelewa ujumbe kama inavyokusudiwa. Huu ni ukiukaji wa kanuni za nadharia ya uhusiano ambazo zinawahitaji watu kutoa maelezo zaidi panapohitajika. Tuligundua kuwa pia Wakenya hupuuza yanayosemwa na viongozi au yale yanayotangazwa katika vyombo vya habari kuhusu virusi vya korona. Hii ndio maana tunaangazia upuuzaji wa yanayosemwa katika kishemu kifuatacho.

3.1.3 Upuuzaji Wa Yanayosemwa

Upuuzaji wa yanayosemwa na viongozi au vyombo vya habari ni athari hasi inayotokana na kupuuza majukumu ya lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya, 2010. Katiba ya Kenya

inakitambua Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha ya kwanza rasmi kikifuatiwa na Kiingereza kama lugha ya pili rasmi, inazitambua lugha ishara na lugha asili. Kwa hali hii basi, viongozi na vyombo vya habari vinapaswa kutilia maanani matumizi ya lugha hizi katika uhamasishaji dhidi ya janga la korona kwenye ngazi ya kitaifa. Kutokana na upuuzaji huu wa katiba ya Kenya kilugha, Wakenya wanapuuzwa yanayosemwa na viongozi hawa. Hali hii inawafanya kupuuzwa mikakati iliyowekwa na serikali kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya kuambukizana virusi vya korona. Kutokana na watafitiwa wetu tuligundua kuwa asilimia kubwa ya Wakenya wanapuuzwa masharti yaliyowekwa na serikali kwa kutotaka kusikiliza hotuba za viongozi kwa kuwa wao hutumia Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili.

Vyombo vya habari vimekuwa msitari wa mbele katika uhamasishaji dhidi ya virusi vya korona. Vyombo vya habari vimekuwa vikiwapasha Wakenya kuhusu janga la korona na vile vile kuwahamasisha dhidi yake. Vyombo vya habari kama vile televisheni ya Citizen imekuwa ikiandika ujumbe kuhusu namna ya kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona. Nia kuu ikiwa ni kuwafanya watazamaji wauone ujumbe huo ili waweze kuchukua tahadhari ifaayo na kufuata masharti yaliyowekwa na serikali. Ujumbe ambao umekuwa kwenye runinga ya citizen kuanzia mwezi Machi-Disemba 2020 ni:

“The corona virus disease (COVID-19) is a communicable respiratory disease caused by a new strain of coronavirus that causes illness. Most people infected will develop mild to moderate illness. Most common symptoms are: fever, dry cough, tiredness. Less common symptoms are: body ache, sore throat, diarrhoea, conjunctivitis, headache, loss of taste or smell, a rash on skin or discolouration of fingers or toes.”*(Ugonjwa wa korona (COVID-19) ni wa kuambukizwa ambao unasababishwa na virusi vya korona ambavyo huwafanya watu kuugua. Dalili za watu walioambukizwa ni kama vile, joto mwilini, kikohozi kikavu, kuchoka, kuumwa mwili, koo inaumia, kuharisha, kuumwa kichwa, kupoteza hisia za kunusa, na vidole vya miguu na mikono kubadilisha rangi.)*

Ujumbe huu wa televisheni ni muhimu kwa kuwa unawaeleza Wakenya kuhusu ugonjwa wa korona. Vyombo vya habari vinaelezea dalili ambazo zinahusishwa na ugonjwa usababishwao na virusi vya korona ili watu wajue na watafute matibabu haraka. Hii ni muhimu kwa kuwa watu watajua wakati watapatwa na virusi hivi, kisha

watajitenga na watu wengine kwa nia ya kupunguza maambukizi kwa watu wengine. Tuliwahoji wakaazi wa eneo la Ruai kutaka kujua namna wao huchukulia ujumbe huu wa televisheni kuhusu ugonjwa wa korona. Tuligundua kuwa wengi wao husoma ujumbe huu na kila wakati huwa wanakuwa makini kwa nia ya kutaka kujua iwapo ni dalili za virusi vya korona kama inavyoelezwa na vyombo vya habari. Tuliwahoji vijana ambao huwa na mashamba yao ya kuuza miti na mboga za kupanda kando kando ya barabara ya Kangundo. Mazungumzo yao yalikuwa kama ifuatavyo:

1. M1: **Mi chenye nimepata ni hizo symptoms. Nakuwa keen hata nikisikia kukohoa naogopa.**
2. M2: **Hata juzi nimeenda soko kubuy minji, wacha jamaa akohoe, kila mtu alienda mbio.**
3. M3: **Hiyo TV inatumia kizungu ngumu hata sielewangi mimi walahi.**
4. M4: **Hiyo ujumbe hunikumbusha tu kuwa kuna corona na hivyo natake caution.**
5. M5: **Hizo vitu hazielewekangi saa hata sisomangi.**

Kutokana na mazungumzo haya, tunaweza kusema kuwa wapo Wakenya ambao wamesaidika na jumbe hizi ambazo huwa kwenye televisheni kila mara. Hawa ni wale, kutokana na utafiti wetu, wamekwenda skuli na kupata kisomo cha haja kinachowawezesha kufahamu jumbe zitolewazo kuhusu korona kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Ingawa hivyo, wapo wanaosema kuwa lugha inayotumika ni ngumu na hivyo huwa hawaelewi kilichoandikwa. M1, M2 na M4 wanaonyesha kuwa wamefaidika na jumbe hizi. Ni kwa sababu hii ambapo baadhi ya watafitiwa wanasema kuwa jumbe hizo ni muhimu kwa kuwa zinawajuza kuhusu ugonjwa wa korona. Ingawa hivyo, M3 na M5 wanaashiria kuwa wao hupuuza jumbe hizi kwa kuwa huwa zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Semi zao zinadhihirisha kuwa huwa hawapendi kusoma jumbe hizi kwa kuwa zimeandikwa kwa lugha ngumu. Haya yanadhihirika katika vipengele vifuatavyo vya usemi wao:

4. M3: **Hiyo TV inatumia kizungu ngumu hata sielewangi mimi walahi.**
6. M5: **Hizo vitu hazielewekangi saa hata sisomangi.**

Kutokana na vipengele hivi vya mazungumzo ni wazi kuwa upuuzaji wa katiba kilugha ya Kenya unawafanya watu kupuuzia yale yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kwa hivyo kukosa kupata jumbe za uhamasishaji dhidi ya maenezi ya virusi vya korona. Vyombo vya habari vimedhihirisha kuwa vinapendelea Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Runinga ya Citizen huweka ujumbe huu wa Kiingereza kwa muda mwingi. Hii ni changamoto kwa kuwa Wakenya wengine hupuuza kusoma jumbe hizi kwa kudai kuwa zimeandikwa kwa lugha ngumu. Hili huwafanya kupuuzia masharti yaliyowekwa na serikali ya Kenya na hivyo basi kuwa katika hatari ya kuambukizwa au kuwaambukiza watu wengine virusi vya korona.

Katika kisehemu hiki cha kazi yetu ya utafiti, tumeonyesha vile upuuzaji wa katiba ya Kenya kilugha huwa na athari hasi katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya ugonjwa wa korona. Ingawa hivyo, uhamasishaji huu una athari chanya kwa Wakenya. Hii ni kwa sababu, Wakenya hawakujua kimbele kuhusu ugonjwa huu na hivyo basi walipaswa kupata maarifa yake kutoka kwa viongozi kupitia kwa vyombo vya habari. Ndio maana tunashughulikia athari chanya za matumizi ya lugha katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya ugonjwa wa korona katika sehemu ifuatayo.

3.2.2 Athari Chanya Za Lugha Ya Utangazaji Katika Uhamasishaji Wa UVIKO-19

Hapo juu tumeonyesha namna lugha ya viongozi na ile ya utangazaji na uhamasishaji dhidi ya janga la korona huwaathiri Wakenya kwa njia hasi. Katika sehemu hii, tunaangazia namna matumizi ya lugha mbalimbali huwaathiri Wakenya kwa njia chanya ili kujua vile walivyofaidika kutokana na uhamasishaji dhidi ya ugonjwa wa korona. Katika kisehemu hiki, tunaangazia athari chanya ambazo zinatokana na matumizi ya lugha fulani katika uhamasishaji dhidi ya janga la korona. Tunashughulikia uongezaji maarifa ya kujikinga dhidi ya virusi hivi na uboreshaji mitazamo kuhusu ugonjwa huu.

3.2.3 Kuongeza Maarifa

Uhamasishaji dhidi ya jambo fulani hufanywa ili kuongeza maarifa kuhusiana na jambo hilo husika. Uhamasishaji dhidi ya janga la korona umekuwa ukifanywa nchini Kenya na viongozi na vyombo vya habari. Uhamasishaji huu umekuwa ukifanywa ili Wakenya waweze kuuelewa ugonjwa wa korona vyema na kisha kuchukua hatua zifaazo ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi yake. Ugonjwa wa korona uliripotiwa mwanzo

katika nchi ya Uchina na kusambaa haraka kwa mataifa mengine jambo ambalo liliwafanya viongozi wa Afrika pia kuchukua jukumu la kuwahamasisha raia zao. Uhamasishaji ulifanywa na viongozi na vyombo vya habari kupitia kwa wataalamu wanaoshughulikia magonjwa ambayo husambaa haraka. Kwa kuwa sio kila Mkenya angeweza kuzungumza na wataalamu hawa, vyombo vya habari viliwahoji wataalamu hawa na Wakenya wamepata kujua mengi kuhusiana na virusi vya korona.

Waziri wa Afya, Bwana Kagwe amekuwa akiwaeleza Wakenya kuhusu namna hali ilivyo nchini kuhusiana na maambukizi na vifo ambavyo vinatokana na ugonjwa wa COVID-19. Katika hotuba zake, Bwana Kagwe amekuwa akiwaambia Wakenya wawe makini na wachukue tahadhari ili kuzuia maambukizi zaidi. Amekuwa akiwahamasisha Wakenya namna ya kujikinga dhidi ya kuambukizwa virusi hivi vya korona. Baadhi ya mikakati iliyowekwa na serikali kuzuia maambukizi ya virusi vya korona ni kudumisha usafi kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka, kutohudhuria mikutano ya hadhara na kupunguza kutoka nyumbani hasa ikiwa mtu hana shughuli muhimu mjini au mtaani. Pia Wakenya wametakiwa kuvaa barakoa wanapokuwa na watu wengine ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona. Hotuba ya Bwana Kagwe ya tarehe 22, Machi, 2020 ilikuwa ya kuwaeleza Wakenya kuwa virusi vya korona ni hatari kwa kuwa vinaathiri hata mataifa yaliyoendelea. Baadhi ya vipengele vya hotuba hiyo ni muhimu kwa kuwafanya Wakenya kupata maarifa kuhusu ugonjwa wa korona kama ifuatavyo:

“.....Fellow Kenyans, the virus disease has affected world statistics, global infection is at 266,073..... The health centre has shifted from China to Europe. In Africa, 572 case with 12 deaths as at 21st March..... Second week is critical as we contain the outbreak. Maintain high hygiene, keep social distance, wear your mask while in public The government in the past few weeks announced various containment measures. We are disappointed because majority ignore them, they behave as if its business as usual. Caution, this disease is not a joke, give it the seriousness it deserves. Change lifestyle. If we continue to behave normally, this disease will treat us abnormally..... wash your hands, its just hygiene, just soap and water.”Tafsiri yake kwa Kiswahili ni kama ifuatavyo: (*....Wakenya wenzangu, virusi vya korona vimeathiri ulimwengu mzima, walioambukizwa ulimwenguni ni watu 266,073. Afrika ina visa 572 na vifo 12 kufikia tarehe 21 Machi. Juma la pili ni hatari zaidi na hivyo tuendele kuzuia maambukizi zaidi. Dumisha usafi wa hali ya juu, kaa mbali na mwenzako, vaa barakoa unapokuwa*

na watu wengine..... Serikali ilitangaza mikakati ya kufuatwa katika majuma machache yaliyopita. Tunasikitika kwa kuwa watu wengi hawatilii maanani mikakati hii na kuchukulia mambo kama kawaida. Ugonjwa huu sio mchezo, upe uzito unaostahiki. Badilisha mitindo ya maisha. Tukiendelea kuishi kama kawaida, ugonjwa huu utatuhangaisha. Ni usafi tu, nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka.)

Usemi wa Waziri wa Afya, Bwana Kagwe unaonyesha yale ambayo Wakenya wanapaswa kufanya ili kupunguza maambukizi miongoni mwa watu. Kutokana na hotuba hii, Waziri anataka Wakenya wachukulie janga la korona kwa uzito unaofaa kwa kufuata masharti yaliyowekwa na serikali kwa lengo la kupunguza maambukizi zaidi. Kagwe anatumia Kiingereza hali inayoashiria ukiukaji wa katiba ya Kenya kilugha. Ingawa hivyo, Kagwe alitoa hotuba kwa kutumia maneno ya Kiingereza ambayo yaliyoonyesha madhara ya janga la korona. Hali hii inajitokeza Kagwe anaposema kuwa **“Caution, this disease is not a joke, give it the seriousness it deserves.”** Maneno haya ya Kagwe ni onyo au tahadhari kwa Wakenya ambao hawaamini kuwa ugonjwa wa korona uko. Onyo hili limetolewa ili kuwashawishi Wakenya kufuata masharti yaliyotolewa na serikali kwa nia ya kuzuia msambao wa virusi vya korona. Maneno haya yalionyesha kuwa ugonjwa wa korona unapaswa kuchukuliwa kama janga ambalo ni hatari. Hii ndio maana anawatahadharisha Wakenya kwa kuwaambia kuwa wachukulie ugonjwa huu kwa uzito unaofaa. Kagwe aliongezea kwa kusema kuwa **“...If we continue to behave normally, this disease will treat us abnormally...”** Kwamba Wakenya wanapaswa kubadilisha tabia na mienendo na kuacha kuishi kama ilivyo kwa kawaida. Waziri Kagwe anatumia mbinu ya tahadhari ili kuwashawishi Wakenya kufuata masharti na kuzuia msambao zaidi ya virusi vya korona. Tahadhari hii inawaonya Wakenya dhidi ya kuendelea kuishi kama kawaida, na kuonyesha kuwa kinyume chake kitasababisha ugonjwa huu kusambaa kwingi na itakuwa vigumu kwa taifa kuuthibiti.

Waziri ametumia Kiingereza kuwatahadharisha Wakenya kuwa wanapaswa kubadilisha mienendo yao ili kuweza kushinda vita dhidi ya janga la korona. Tuliwahoji Wakenya, vijana waliofanya kazi barabarani hali maarufu ‘kazi kwa vijana’ katika mji wa Nairobi, eneo la Shooters kwa kutaka kujua namna walivyochukulia tahadhari ya Bwana Kagwe kutokana na semi tulizoziangazia katika aya hii. Mazungumzo yao yalikuwa ifuatavyo:

1. M1: **Mi vile nimeelewa ni kwamba waziri anataka watu wajikinge kabisa na hii korona juu inatembea mbio sana.**
2. M2: **Kwa upande wangu, mimi naona Waziri anatumieleza vile hii ugonjwa ni mbaya. Juu haki watu wa Amerika wamekufa tu sana. Sasa Waziri ametueleza tu vile tunafaa kuzuia hii ugonjwa.**
3. Mtafiti: **Wewe unajua njia zipi?**
4. M2: **Kulingana na vile nimemsikia akisema mara kadhaa ni kuwa ugonjwa hii inaletwa na uchafu, na pia inasambazika kupitia kusalimiana. Saa hiyo ni rahisi juu tumeshaacha hata kusalimiana na kutembeleana.**
5. M3: **Ndio maana hata hakuna mwenye ako na hiyo korona hii Kisii.**
6. M4: **Mask ndio ngumu tu juu hata huwezi pumua lakini tunavaa kwanza tukikuja huku tao.**
7. M5: **Mi chenye nilielewa ni kuwa hii ugonjwa sio normal aki na tunatakiwa kuwa serious vile anasema juu unajua yeye ni Minister for Health so ni kumaanisha kuwa anajua juu ya korona kutuliko.**

Semi za watafitiwa hawa zinadhirisha kuwa Wakenya wanapata maarifa kuhusu virusi vinavyosababisha ugonjwa wa korona kutoka kwa viongozi wao. Viongozi wanakiuka katiba ya Kenya kilugha ila watu wanapata ujumbe na hivyo basi wanajua kuwa wanapaswa kufuata mikakati iliyowekwa na serikali ya kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona. Semi za watafitiwa hawa zinaonyesha kuwa Wakenya wanapata ujumbe kuwa virusi vya korona ni hatari. Kutokana na tahadhari ya Kagwe kuwa “...**this disease is not a joke, give it the seriousness it deserves.**” Wakenya wamedhihirisha kuwa usemi huu uliwafanya wao kuwa makini zaidi ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona. M1 anathibitisha hili anaposema kuwa “...**waziri anataka watu wajikinge kabisa na hii korona juu inatembea mbio sana.**” Usemi wake unathibitisha kuwa kutokana na tahadhari ya Kagwe, M1 aligundua kuwa huu ugonjwa unasambaa kwa haraka na hivyo hawana budi kujikinga kwa kufuata kanuni zilizotolewa na Wizara ya Afya. Uhamasishaji unaofanywa kwa kutumia mbinu ya tahadhari unakuwa na athari chanya kwa kuwa Wakenya wanachukua tahadhari dhidi ya virusi vya korona. Mbinu hii ya tahadhari inawafanya kuchukulia janga la korona kwa uzito unaofaa.

Kwa upande mwingine, M2 anathibitisha kuwa kutokana na tahadhari ya Kagwe, amepata kujua kuwa ugonjwa wa korona unawasumbua watu hata wa mataifa ambayo yameendelea. M2 anatambua kuwa ugonjwa wa korona unaua na hivyo ni muhimu kujikinga na kuwakinga wengine dhidi yake. Tahadhari aliyoitoa Bwana Kagwe inazua hofu kwa Wakenya. Hofu hii ni nzuri kwani itawafanya watu kufuata mikakati iliyowekwa na Wizara ya Afya ili kujikinga na kuwakinga watu wengine dhidi ya maambukizi ya virusi hivi. Hofu ya M2 inadhihirika zaidi anaposema kuwa “**Waziri anatueleza vile huu ugonjwa ni mbaya. Juu haki watu wa Amerika wamekufa tu sana.**” Matumizi ya maneno *juu haki* yanaonyesha kuwa ameshajua kuwa virusi vya korona ni hatari. Tahadhari ya Bwana Kagwe inaashiria kuwa Wakenya ambao ni watu wa taifa ambalo bado ni miongoni mwa mataifa yanayoendelea wataweza kumalizwa na virusi vya korona iwapo hawatakuwa makini. Tahadhari ya Kagwe pia inamtia M5 hofu kama inavyobainika anaposema kuwa “**Mi chenye nilielewa ni kuwa hii ugonjwa sio normal aki na tunatakiwa kuwa serious vile anasema juu unajua yeye ni Minister for Health so ni kumaanisha kuwa anajua juu ya korona kutuliko.**” Usemi wake unaonyesha kuwa pia yeye ana hofu ya virusi vya korona kutokana na tahadhari ya Waziri wa Afya, Bwana Kagwe.

M2 anathibitisha kuwa ameelewa masharti ya kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya korona yaliyotolewa na Wizara ya Afya anaposema kuwa “**Saa hiyo ni rahisi juu tumeshaacha hata kusalimiana na kutembeleana.**” Usemi huu uanonyesha kuwa M2 ameelewa mikakati iliyowekwa na serikali katika kukabiliana na janga la korona. Mtafitiwa anasema kuwa wameacha kusalimiana na hata kutembeleana kutokana na uhamasishaji wa Kagwe kuwa watu wakae nyumbani. Hii inaonyesha kuwa tahadhari ya Kagwe iliwaathiri watafitiwa hawa kwa njia chanya na hili ni jambo ambalo linawafanya kuwa na hofu na kwa hali hiyo basi, kufuata maagizo yaliyotolewa na Wizara ya Afya ya namna ya kujikinga dhidi ya virusi vya korona.

Kutokana na semi za watafitiwa tuliowashughulikia katika kishemu hiki, ni wazi kuwa Waziri Kagwe alizingatia kanuni mojawapo ya nadharia ya uhusiano ya kuwataka wasemaji kutoa ujumbe kwa namna ambayo utafasirika kwa urahisi. Waziri Kagwe ametumia Kiingereza na hili ni jambo ambalo linakiuka majukumu ya lugha mbalimbali kwa mujibu wa katiba ya Kenya ila anaeleweka kutokana na kutumia mbinu ya tahadhari

ambayo inaibua athari chanya kwao. Athari hii chanya inawafanya Wakenya kuuogopa ugonjwa wa korona na kwa hali hiyo, wanachukua hatua madhubuti kuzuia maambukizi zaidi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kama inavyodhihirika katika mazungumzo ya watafitiwa hapo juu. Kwa baadhi ya Wakenya wengine, maagizo yaliyotolewa na Wizara ya Afya ni kikwazo kwao ila wanalazimika kuyafuata ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona. Wakenya wanatakiwa kuvaa barakoa kila wakati wanapokuwa hadharani. Barakoa ni muhimu kwa kuwa huzuia mtu kumwambukiza mwingine virusi vya korona kupitia kwa mate au kamasi. Kwa hali hiyo basi, ni muhimu kwa Wakenya kuvaa barakoa ingawa hawapendezwi nayo. Usemi wa M4 unadhihirisha hili anaposema kuwa **“Mask ndio ngumu tu juu hata huwezi pumua lakini tunavaa kwanza tukikuja huku tao.”** Usemi huu unaonyesha kuwa Wakenya hawapendezwi na kuvalia barakoa ila wanafuata masharti ya serikali yatolewayo kwa Kiingereza ili kuwakinga watu wengine na kujikinga pia dhidi ya virusi vya korona.

Kutokana na mazungumzo yaliyo hapo juu, ni wazi kuwa Wakenya wameweza kuuelewa ugonjwa wa korona kupitia kwa viongozi na vyombo vya habari. Semi za watafitiwa tuliowaangazia hapo juu zinaonyesha kuwa Wakenya wamepata maarifa kuhusu virusi vya korona na kwa hali hii wanafuata masharti yaliyotolewa na Wizara ya Afya kwa lengo la kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona. Tunasema hivi kwa sababu, asilimia kubwa ya Wakenya hawana ujuzi wa magonjwa ambayo yanazuka na hivyo basi, viongozi huwa na jukumu la kuwahamasisha ili kuwapa mwanga na kuwaeleza namna ya kujikinga.

3.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumeonyesha namna lugha itumiwayo na viongozi na kwenye vyombo vya habari huathiri Wakenya katika uhamasishaji dhidi ya ugonjwa wa korona. Tumeonyesha kuwa ni muhimu kwa viongozi na vyombo vya habari kuzingatia katiba ya Kenya kilugha kama inavyojitokeza katika katiba ya mwaka wa 2010. Katiba ya Kenya inaonyesha kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa na ya kwanza rasmi katika taifa la Kenya. Kiingereza vile vile ni lugha rasmi. Katiba hiyo pia imeangazia lugha ishara na lugha za asili. Kwa hali hii basi, tumeonyesha kuwa upuuzaji wa katiba ya Kenya kilugha huwa na athari hasi na chanya katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona.

Tumegundua kuwa athari hasi ni kama vile kufasiri ujumbe visivyo au kupuuza ujumbe ulioandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Vile vile, tumeonyesha kuwa Wakenya walipata maarifa kuuhusu ugonjwa wa korona kutokana na hotuba za viongozi na matangazo ya vyombo vya habari. Hii ni athari chanya kwa kuwa Wakenya waliweza kuelewa ugonjwa wa korona na kisha kujua namna ya kujikinga kupitia kwa uhamasishaji uliofanywa na viongozi na kupitia kwa vyombo vya habari. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa ni muhimu kwa viongozi kufuata majukumu ya lugha mbalimbali kikatiba ili wasije wakawafungia wengine nje katika uhamasishaji dhidi ya janga la korona. Ni vyema kukumbuka kuwajanga hili linaathiri kila mtu bila kubagua kwa misingi ya uwezo wa kiuchumi wala kiwango cha elimu. Hivyo basi, ni vyema kutilia maanani katiba ya Kenya kilugha ili ujumbe uweze kumfikia kila mmoja kwa lugha anayoipendelea.

SURA YA NNE

NAFASI YA KISWAHILI KATIKA UHAMASISHAJI WA WAKENYA DHIDI UVIKO-19

4.1 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia , tumeangazia athari za lugha ya utangazaji na uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Tumeonyesha kuwa lugha ya Kiingereza ilitumika zaidi katika uhamasishaji uliofanywa na viongozi na vyombo vya habari kuliko Kiswahili. Hali hii iliwafanya watu kupuuza au kufasiri ujumbe uliotolewa visivyo. Hii ni kutokana na athari ya kupuuza katiba ya Kenya kilugha. Tumeonyesha pia kuwa kunazo athari chanya za matumizi ya Kiingereza kwa kuwa ugonjwa huu ni mpya na hivyo Wakenya hawakuwa wanauelewa. Ni kwa sababu hii basi ambapo lugha ya Kiingereza ambayo ni ya kimataifa ikatumika kuwahamasisha Wakenya.

Katika sura hii, tutashughulikia nafasi ya Kiswahili katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Tutashughulikia matangazo ya vyombo vya habari na semi ambazo hutolewa na viongozi kwa lugha ya Kiswahili. Hatimaye tutaonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika uhamasishaji kwa kuangalia namna ujumbe uliotolewa kwa Kiswahili unavyopokelewa na Wakenya. Katika sura hii, tunaonyesha namna vyombo vya habari na viongozi wanatumia Kiswahili katika kuwahamasisha Wakenya dhidi ya janga la korona. Tutaongozwa na mhimili unaoshughulikia uzingativu wa uhusiano baina ya mahitaji, uwezo na mazingira yanayooana na mkabala husika. Hii ni kwa sababu tumegundua kuwa viongozi hutumia Kiswahili wanapokuwa katika maeneo ya pwani ambapo lugha ya mawasiliano ni lahaja mbalimbali za Kiswahili. Hii ni kinyume na hotuba zinazokuwa zinatolewa jijini Nairobi ambapo viongozi wanatumia Kiingereza. Hii inaonyesha kuwa viongozi wanazingatia mazingira wanapokuwa wakitoa hotuba zao. Tutazingatia hotuba zinazotolewa kwa Kiswahili kuhusu virusi vya korona katika sura hii.

4.2 Kiswahili Kama Chombo Imara Cha Uhamasishaji Dhidi Ya UVIKO-19

Kiswahili ni lugha ya taifa na imepewa hadhi pia ya kuwa lugha ya kwanza rasmi kulingana na katiba ya Kenya ya 2010. Kiswahili kinakuwa mwafaka katika uhamasishaji

wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Janga hili linahitaji ushirikiano wa idara zote za serikali na watu wote katika kupunguza maambukizi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Lugha itakayotumiwa katika uhamasishaji huu ni muhimu. Kutokana na hali hii basi, lugha ya Kiswahili inaweza kuwa faafu katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Matangazo kuhusiana na korona yanapaswa kutolewa kwa Kiswahili. Maandishi yanayohusiana na janga la korona, kwenye kuta, mavazi, barakoa na kwenye mitungi ya maji ya kunawa yanapaswa kuwa katika Kiswahili. Hili litahakikisha kuwa Wakenya wanaelezwa kuhusu kuzuka kwa virusi vya korona, maambukizi na suluhisho lake kwa lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili. Hili litawawezesha Wakenya kuchukua hatua zilizotolewa na Wizara ya Afya za kudumisha usafi na kuvaa barakoa. Hii ndio maana tunashughulikia nafasi ya Kiswahili katika sura hii ambapo tutaanza na Kiswahili kama kitambulisho na kiunganishi cha Wakenya.

4.3 Kiswahili Kama Kitambulisho na Kiunganishi Cha Wakenya

Katika nchi ya Kenya, Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi kwa mujibu wa katiba ya 2010. Kwa hali hii basi, Kiswahili kinapaswa kutumika katika shughuli za serikali na bunge, lugha ya mawasiliano mapana kama vile inayotumika katika vyombo vya habari nchini Kenya. Vile vile, Kiswahili kinapaswa kuwa lugha ya mawasiliano baina ya watu wa makabila mbalimbali nchini Kenya. Hii inaonyesha kuwa Kiswahili ni lugha unganishi ya Wakenya wote, wadogo kwa wakubwa na wasomi na wasio wasomi. Hii ni kwa sababu, Kiswahili ndio lugha inayotumika na watu zaidi ya asilimia 80 huku Kiingereza kikitumiwa na asilimia 20 tu ya Wakenya (Kiango, 2002). Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa Kiswahili ni lugha sambazi. Hivyo basi Kiswahili ni lugha mwafaka katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya virusi vya korona kwa kuwa ndio lugha inayozungumzwa na asilimia kubwa ya Wakenya ikilinganishwa na Kiingereza.

Mbali na lugha, taifa laweza kutambuliwa kutokana na bendera ya nchi husika na mambo mbalimbali kama vile michezo, elimu na vyakula. Hata hivyo, lugha ni chombo muhimu zaidi cha utambulisho wa taifa fulani. Lugha ya taifa ya nchi fulani huwa kitambulisho cha taifa husika. Kiswahili ndio lugha ya taifa nchini Kenya. Hivyo basi, Kiswahili ni kitambulisho cha Wakenya. Hii ndio maana tunasema kuwa ni muhimu kwa viongozi na vyombo vya habari kutumia Kiswahili zaidi katika mawasiliano yao. Nchini Kenya,

Kiswahili hutumika kama kiunganishi katika mawasiliano miongoni mwa watu wa makabila tofauti tofauti. Wanasiasa pia hutumia Kiswahili wanapofanya siasa zao, hasa wakati wa kampeni. Wao hutumia Kiswahili ili kuonyesha kuwa wanawaenzi Wakenya na lugha yao tukufu. Tunasema hivi kwa sababu wanasiasa wawa hawa hupendelea kutumia Kiingereza katika mawasiliano yao hasa wanapokuwa bungeni kwa kuamini kuwa ndio lugha ya wasomi nchini Kenya. Hali hii inaonyesha kuwa wanasiasa wanajua kuwa Kiswahili ndio lugha unganishi nchini Kenya na ndio maana wao hukitumia wanapofanya kampeni zao wakati wa uchaguzi.

Katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19, wapo viongozi ambao wanatumia Kiswahili. Viongozi hawa wanatumia Kiswahili ili kuweza kuelewika na Wakenya wengi. Waziri wa Afya, Kagwe alikuwa na mazoea ya kutumia Kiingereza wakati wa mwanzo mwanzo kutoa hotuba inayohusiana na janga la korona kwa taifa. Ingawa hivyo, hotuba yake ya baadaye Machi, 27, 2020, akiwa kaunti ya Mombasa alitumia Kiswahili katika baadhi ya sentensi. Aliteua maneno ya Kiswahili ambayo aliyatumia kuwaeleza watu wa Mombasa hatua ambazo serikali ilikuwa imechukua ili kuhakikisha kuwa maambukizi ya virusi vya korona yamepunguzwa. Waziri aliisoma hotuba yake kwa Kiingereza ila akachanganya na Kiswahili kama ifuatavyo:

“.... Kulingana na hotuba ya Rais, alisema kaunti za Nairobi, Kwale, Kilifi na Marsabit watu wakae ndani. Wageni mtangoja 21 days kabla kuingia Nairobi, Nairobi tukae Nairobi hakuna kutoka sababu tukitembea tutapeleka virusi huko tunaenda. Tujikinge, tujitayarisha sio kitu inapita harakaharaka. Tutafanya chochote ndio watu wasiumie au kufa vile nchi zingine tuwe tayari. Kenya tunaona vile kunafanyika hata ng’ambo. Tunawasihi tufanye vile serikali inasema usijaribu eti wewe ni mwerevu. Usicheze sio uerevu ni ujinga.”

Waziri wa Afya, Kagwe ametumia Kiswahili katika hotuba hii ila ametumia maneno matatu ya kiingereza, *days* katika kipengele hiki cha mazungumzo. Maneno matatu ya Kiingereza yametumika hapa tofauti na ambavyo Kagwe amekuwa akitumia Kiingereza katika hotuba zake kwa taifa zima. Kiswahili kimetumika hapa kwa kuwa mazingira ya pwani ni ya Waswahili. Hili linajitokeza hapa kwa kuwa mazingira ni muhimu katika matumizi ya lugha fulani. Hotuba hii ya Waziri Kagwe ni ya kuwahamasisha watu na

kuwaeleza sababu ya kuweka vikwazo vya kutosafiri kutoka kaunti moja hadi nyingine. Waziri anasema hivi kwa kuwa anajua kuwa watu hawajafurahishwa na vikwazo vya kutosafiri kwenda kaunti zingine. Matumizi ya Kiswahili ni muhimu katika mazingira haya kwa kuwa waziri alikuwa na nia ya kuwataka Wakenya kuelewa sababu ya kuweka vikwazo vya usafiri.

Mazungumzo ya Bwana Kagwe yanaonyesha sababu za kuweka vikwazo hivi ila pia anaonyesha kuwa haitachukua muda mrefu. Hili linajitokeza anaposema kuwa “**Wageni mtangoja 21 days kabla kuingia Nairobi, Nairobi tukae Nairobi hakuna kutoka sababu tukitembea tutapeleka virusi huko tunaenda.**” Bwana Kagwe ametumia mbinu ya takriri katika usemi huu. Neno *Nairobi* limetajwa mara tatu kwa nia ya kuisitiza. Takriri ni muhimu kwa kuwa huwawezesha watu kuelewa zaidi. Kagwe ametumia msisitizo kama mbinu ya kutoa maelezo zaidi kwa Wakenya. Takriri imetumiwa katika uhamasishaji ambao umefanywa kwa lugha ya Kiswahili ili Wakenya waweze kuelewa sababu ya serikali kuwawekea vikwazo vya kutosafiri kutoka na kwenda kaunti kama vile Nairobi na Mombasa. Mbinu ya kurudia maneno ya miji ambayo imefungwa ni kuashiria kuwa kaunti husika zilikuwa zimerekodi idadi kubwa ya maambukizi ya ugonjwa wa korona na hivyo kufungwa kwao kulinuia kupunguza msambao kwa kaunti zingine.

Vikwazo vya kutosafiri kutoka kaunti kama vile Mombasa hadi Kwale huathiri watu kiuchumi. Hii ni kwa sababu watu hufanya kazi katika kaunti mbalimbali kwa mfano, watu wanawezakuwa wanaishi Kwale ila wanafanya kazi Mombasa. Ingawa hivyo, Waziri Kagwe anatumia lugha shawishi pia katika hotuba yake kuwaeleza Wakenya kinagaubaga sababu za kuweka vikwazo vya usafiri kutoka kaunti moja hadi nyingine. Vile vile, Waziri huyu anatumia lugha ya ahadi kwa nia ya kuwapa Wakenya matumaini dhidi ya athari hasi za kiuchumi zinazosababishwa na janga la korona. Hili linabainika anaposema kuwa “**Tutafanya chochote ndio watu wasiumie au kufa vile nchi zingine tuwe tayari. Kenya tunaona vile kunafanyika hata ng’ambo.**” Pia tunaweza kusema kuwa Waziri ametumia mbinu ya ulinganisho katika usemi huu. Waziri analinganisha nchi ya Kenya na mataifa mengine yaliyoathiriwa na ugonjwa wa korona kama mbinu ya kuwashawishi Wakenya kuamini kuwa virusi vya korona ni hatari.

Waziri wa Afya anatoa hotuba yake lugha ya Kiswahili kwa kutumia mbinu ya urudiaji, lugha shawishi na vile vile ulinganisho kwa nia ya kuwashawishi Wakenya kuzingatia masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya. Bwana Kagwe pia anawasuta wale wanaopitia njia mbadala kuingia na kutoka kaunti zilizofungwa. Anatumia lugha ya kurai pamoja na ya kuwasuta Wakenya wanaokaidi kanuni za serikali na kuwataka wafuate masharti kwa kutumia neno *tunawasihi* na *ujinga* anaposema kuwa “**Tunawasihi tufanye vile serikali inasema usijaribu eti wewe ni mwerevu. Usicheze sio uerevu ni ujinga.**” Katika usemi huu, Waziri Kagwe anatumia lugha ya kurai na kusuta vile vile kwa nia ya kutaka kueleweka vizuri na Wakenya. Tuliwahoji Wakenya wa eneo la Mlolongo kuhusiana na hotuba hii ya Waziri ya Mombasa. Watafitiwa wa Mlolongo walikuwa mwafaka kwa kuwa eneo hili linapatikana katika kaunti ya Machakos ila wakati wa kufunga Nairobi, hawakuruhusiwa kwenda Machakos. Kwa hali hii waliathirika kwa kuwa wengine hufanya kazi katika kampuni za simiti na mafuta zilizo katika eneo la Athi River. Maoni yao yalikuwa ifuatavyo:

1. Mtafiti: **Waziri Kagwe akiwa Mombasa alisema hivi** “*Tujikinge, tujitayarishe sio kitu inapita harakaharaka. Tutafanya chochote ndio watu wasiumie au kufa vile nchi zingine tuwe tayari. Kenya tunaona vile kunafanyika hata ng’ambo. Tunawasihi tufanye vile serikali inasema usijaribu eti wewe ni mwerevu. Usicheze sio uerevu ni ujinga.*” **Je, wewe uliuelewa aje huu ujumbe?**
2. M1: **Huyo mtu wa korona aliongea poa. Kaa watatupea msaada tutatulia tu tusiende job Macha.**
3. M2: **Mutahi anajaribu kutueleza tutulie, juu hii kitu kama imetesa watu wa Amerika wenye wako na uwezo mwingi wa kila kitu, na sisi? Afadhali tutulie tu hadi hii korona iishe.**
4. M3: **Yenyewe ni ujinga mtu kupitia panya route afike kwao ushago halafu apelekee mamathee wenye wamezeeka korona na wakufe tu. Mi nakubaliana na Waziri, wacha watu wakae mahali wako ndio hii kitu iishe haraka haki. Lakini Wakenya tuko wajinga haki, hata maski watu hawataki kuvaa walahi.**

5. **M2: Ujinga ndio inatumaliza haki, sa mtu hajapima halafu anakimbia ushago mahali hata tuhosi hatuwezi kutibu malaria. Na sasa akiwa na korona, si watu watakufa tu na waambukizane kijiji yote?**

Maoni ya watafitiwa hawa yanaonyesha kuwa walielewa alichosema Waziri wa Afya, Kagwe. Kutokana na hali hii, tunaweza kusema kuwa Waziri Kagwe alifaulu kuwahamasisha Wakenya dhidi ya kupitia njia mbadala kuingia mashinani kwa kutumia lugha ya kurai na kusuta vile vile. Usemi wa watafitiwa hawa unaonyesha kuwa wameridhika na hotuba ya Waziri na ndio maana wanaamua kushirikiana na serikali kama inavyobainika M2 anaposema kuwa “**Mutahi anajaribu kutueleza tutulie,..... Afadhali tutulie tu hadi hii korona iishe.**” M2 anaonelea kuwa ni muhimu kufuata masharti yaliyotolewa na Wizara ya Afya ili kupunguza msambao wa virusi vya korona, hii ikiwa ndio nia kuu ya uhamasishaji. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa lugha tumizi na namna ya kuitumia ni muhimu katika kutimiza malengo ya wazungumzaji. Vile vile tumegundua kuwa Wakenya huelewa hotuba zinazotolewa kwa Kiswahili zaidi ikilinganishwa na Kiingereza.

Matumizi ya Kiswahili kwa kutumia lugha ya kurai na kusuta yameweza kuwafanya Wakenya kuelewa masharti ya kupunguza msambao wa virusi vya korona na hivyo basi kuzingatia vikwazo vilivyowekwa. Hili linabainika M3 anaposema kuwa “**Yenyewe ni ujinga mtu kupitia panya route afike kwao ushago halafu apelekee mamathee wenye wamezeeka corona na wakufe tu. Mi nakubaliana na Waziri, wacha watu wakae mahali wako ndio hii kitu iishe haraka haki. Lakini Wakenya tuko wajinga haki, hata maski watu hawataki kuvaa walahi.**” Usemi huu unadhihirisha kuwa hotuba ya Waziri wa Afya iliyotolewa kwa Kiswahili iliweza kupokelewa vilivyo kama alivyokusudia. Vile vile, Wakenya wanaashiria kuwa wako tayari kufuata masharti ya serikali na mtindo mpya wa maisha kama inavyojitokeza katika sehemu ifuatayo.

4.4 Kujenga Na Kuendeleza Mtindo Mpya Wa Maisha

Kiswahili kimetumiwa na viongozi na vyombo vya habari kuwahamasisha watu ili wazoe mtindo mpya wa maisha. Mtindo huo mpya unahusisha kunawa mikono kila wakati, kuvaa barakoa, kutotembeleana nyumbani, kupenga kamasi kwa kutumia sashi na wala sio kitambaa kama ilivyokuwa hapo awali na vile vile kutowatembelea wagonjwa

mahospitalini na kutotembelea mahabusu gerezani na hakuna ruhusa ya watu kutoka nje baada ya saa moja usiku na kabla ya saa kumi na moja asubuhi. Vile vile, magari ya uchukuzi wa umma yamelazimika kupunguza idadi ya abiria. Masharti haya ni mtindo mpya wa maisha kwa Wakenya kwa nia ya kupunguza msambao wa virusi vya korona. Hii ndio sababu serikali ilichukua hatua ya kuwahamasisha watu wakumbatie masharti haya na wala wasichukulie kuwa ni mateso. Hotuba ya Waziri wa Afya, Kagwe, ya Machi, 27, 2020 huko Mombasa inaonyesha mtindo mwingine mpya ambao Wakenya wanaotumia vileo na mihadarati wanapaswa kuufuata. Mtindo huo ni kutokana na masharti yaliyomo katika hotuba ifuatayo:

“... sio lazima uwe karibu na miraa, itaingia hata ukiwa mbali. Ukiingia matatu, usiingie kama imejaa, it’s a choice. Watu wako usiku wanacheza muziki kwa baa, the curfew is still on. Police will be vigilant, don’t be out in the street at night..... Kwa sasa jameni tujikinge na tukimbie sana kutoka kwa hii virusi, tufanye vile tumesema. Kama mimi mzee nina watoto, mama, jirani. Ingawa nina watoto mimi pia ni mtoto, ninaweza kupelekea mama yangu virusi. Vaa maski ukitembelea mama, beba sanitizer na maski usimpatie. Tufanye vile Wizara ya Afya inasema. Tuchungane. Am grateful to the people of Mombasa. Tunawaombea mema.”

Katika hotuba hii, Waziri Kagwe ametumia mbinu ya kuchanganya ndimi na lugha ya kutania ili kuhamasisha Wakenya dhidi ya virusi vya korona. Waziri Kagwe amechanganya ndimi kwa kutumia Kiswahili (ambacho kimetawala) na Kiingereza. Kagwe anatumia Kiingereza kwa nia ya kujieleza ipasavyo kutokana na misingi yake ya uanaafisa na mahusiano katika muktadha wa taifa la Kenya. Utani unajitokeza Waziri Kagwe anaposema kuwa **“.....sio lazima uwe karibu na miraa, itaingia hata ukiwa mbali.”** Matumizi ya utani yametumika ili kuondoa ukinaifu kutokana na lugha ya ukali ambayo imekuwa ikitumika. Matumizi haya ya utani yanaeleweka zaidi hasa kwa waraibu wa mihadarati kinyume na lugha ya ukali. Matumizi ya lugha katika hotuba hii ya Waziri yanalenga kuwataka Wakenya kuchukua jukumu la kibinafsi kwa kufuata masharti na hili ni jambo ambalo litapunguza msambao wa virusi vya korona. Waziri anatumia umoja kuonyesha kuwa mtu binafsi ndiye anapaswa kuchukua hatua madhubuti kupunguza maambukizi ya virusi vya korona. Hili limebainika anaposema kuwa **“Ukiingia matatu, usiingie kama imejaa...”** Jambo lingine linalojitokeza hapa ni kuwa Waziri anawataka Wakenya wawe msitari wa mbele katika kuhakikisha kuwa

wanapunguza maambukizi ya virusi vya korona kwa kujirejelea kama mfano unaopaswa kuigwa. Kujirejelea huku kunaashiria kuwa hakuna ambaye amesazwa katika masharti yaliyowekwa na serikali. Hii ni kutokana na usemi wa Waziri Kagwe kuwa “**Kama mimi mzee nina watoto, mama, jirani. Ingawa nina watoto mimi pia ni mtoto, ninaweza kupelekea mama yangu virusi. Vaa maski ukitembelea mama, beba sanitizer na maski usimpatie. Tufanye vile Wizara ya Afya inasema. Tuchungane.**”

Kutokana na hotuba hii ya Waziri Kagwe, tuliwahoji watu ambao hutumia miraa katika eneo la Shooters, Utawala. Watafitiwa walitueleza kuwa idadi yao imepungua katika kibanda chao kwa sababu watu wanahofia kukamatwa na maafisa wa polisi ambao wanahakikisha kuwa watu wanakaa umbali wa mita moja baina yao. Mazungumzo ya watafitiwa waliokuwa katika kibanda husika wakati wa utafiti wetu yanaonyesha kuwa wanajua umuhimu wa kuzingatia masharti yaliyotolewa na Wizara ya Afya kama ifuatavyo:

1. Mtafiti: **Waziri amesema kuwa mkulie jaba nyumbani, yaani mkae tu nyumbani juu itaingia tu. Maoni yenu ni yapi kuhusiana na hali hii mpya?**
2. M1: **Aaah, si mbaya kama hiyo itatuliza korona sisi ni nani tukatae?**
3. M2: **Hiyo itasaidia lakini saa hii bizna iko down manze. But ni sawa wacha tuchungane.**
4. Mtafiti: **Bizna iko down kwa nini na bado watu wanatumia bado?**
5. M2: **Wee huoni vile wateja wamereduce, hapa kungejaa saa hii kama ni before korona.**
6. M2: **Saa hii ni kaa nyumbani, wewe huoni. Hii korona inaua watu sana.**

Matumizi ya lugha katika mazungumzo ya watafitiwa hawa yanadhihirisha kuwa wameuelewa ujumbe wa Waziri wa Afya. Watafitiwa hawa wanatumia Kiswahili huku wakichanganya na maneno ya Kiingereza hapa na pale. Hii inadhihirisha kuwa Kiswahili ni lugha sambazi hasa katika mitaa mbalimbali ya jiji la Nairobi na ndio maana wanakuwa na mtazamo chanya kuhusiana na hotuba ya Kagwe iliyotolewa kwa Kiswahili. Tunasema hivi kwa kutokana na diskosi ya watafitiwa wetu ambayo inaonyesha kuwa wameridhika na masharti yaliyotolewa na Wizara ya Afya ya kuzuia

msambao wa virusi vya korona. Hili linadhihirika M1 anaposema kuwa **“Aaah, si mbaya kama hiyo itatuliza korona sisi ni nani tukatae?”** Hii inaonyesha kuwa uhamasishaji uliofanywa na Bwana Kagwe ulichukuliwa kwa mtazamo chanya na watumizi hawa wa miraa.

M2 pia anatumia lugha inayoashiria kujali maslahi yake na ya wenzake. Matumizi ya lugha ya M2 anaposema kuwa biashara imekuwa mbaya ila halimfanyi kuishutumu serikali kwa kuweka masharti ambayo yatawakosesha wateja. Usemi wake unaonyesha kuwa anakubaliana na vikwazo vilivyowekwa na serikali ili kuzuia maambukizi zaidi ya ugonjwa wa korona. Hili linadhihirika anaposema kuwa **“Hiyo itasaidia lakini saa hii bizna iko down manze. But ni sawa wacha tuchungane.”** Usemi wa watafitiwa hawa unaonyesha kuwa uhamasishaji uliofanywa na serikali umefaulu kwa kuwa watu wamejua athari za ugonjwa huu na ndio maana wanafuata masharti ya serikali. Tunasema hivi kwa sababu, M2 ambaye ni muuza miraa anatumia lugha inayodhihirisha hali ya kujali na vile vile kuashiria kuwa anajua madhara ya virusi vya korona. Hivyo basi, inaelekea kuwa Wakenya wamekubali mtindo mpya wa maisha.

Kutokana na utafiti huu, tulibaini kuwa wapo viongozi ambao walitumia Kiswahili kuwajua Wakenya kuhusu mtindo mpya wa maisha baada ya kuzuka kwa ugonjwa wa korona. Raila, Waziri Mkuu wa zamani alitumia Kiswahili katika kuwahamasisha watu dhidi ya janga la korona. Hotuba za Raila zinaonyesha kuwa ni muhimu kukumbatia mtindo mpya wa maisha ili kupiga vita virusi vya korona. Raila anatumia Kiswahili kwa kuwa ni lugha sambazi nchini Kenya. Kwa hivyo, Kiswahili ni mwafaka kwa kuwa janga la korona huathiri kila mtu na ndio maana ni muhimu kuzingatia sera ya lugha ya Kenya. Raila anazingatia sera ya lugha ya Kenya anapotoa hotuba yake ya tarehe 25, Machi alipozungumza na Wakenya kupitia kwa mtandao wa Youtube kwa kutumia Kiswahili kama ifuatavyo:

“Wakenya wenzangu, tunaongea juu ya janga la COVID-19. Korona ni kweli na ni hatari kwa wanadamu, umesababisha vifo 16000 duniani. Tujilinde, tusafishe mikono, tutumie sanitizer, tujiepushe kwenda matanga, tusingie kwenye kundi la watu, tushishikane mikono kwa kusalimiana, tukae mbali na atu wengine, tutimize yale tunaelezwa mara kwa mara, tujiepushe kwenda hapa na pale, kaa nyumbani na familia yako.”

Katika hotuba hii, Raila anatumia lugha ya uhamasishaji na ya kuwarai Wakenya kufuata masharti ili kuzuia msambao wa ugonjwa wa korona. Nchini Kenya, Kiswahili kinachukuliwa kuwa duni na ndio maana viongozi wengi hutumia Kiingereza katika mazungumzo yao. Hii ndio maana viongozi wanatumia Kiingereza zaidi ambacho kinanasibishwa na watu waliosoma katika mazungumzo yao. Ingawa hivyo, Raila ambaye ni kiongozi pia anawahamasisha Wakenya kupitia kwa mtandao wa Youtube kwa kutumia Kiswahili. Raila anawataka Wakenya kuzoea mtindo mpya wa maisha wa kutosalimiana kwa kutumia mikono na kutohudhuria matanga kama hapo awali. Jamii kama ya Waluo, atokako Raila, maombolezi huwa sherehe kubwa sana ambayo huhudhuriwa na watu wengi na vyakula vya kila aina huandaliwa. Hata hivyo, Raila anachukua jukumu la kuwaeleza Wakenya, wakiwemo watu wa kabila lake kuwa wajiepushe kwenda kwa matanga.

Lugha ya Kiswahili pia inaweza kutumika katika maandishi mbalimbali kuwahamasisha watu dhidi ya ugonjwa wa korona. Kutokana na kuwepo kwa virusi vya korona nchini Kenya, watu wanatakiwa kunawa mikono kabla ya kuingia kwa magari. Hii ni kwa kuwa Wizara ya Afya inawaeleza watu namna ya kupata virusi vya korona. Njia mojawapo ni kutokana na kushika mahali ambapo mtu aliye na virusi hivi ameshika. Mitungi ya maji inawekwa kwenye vituo vya mabasi na katika milango ya hospitali na hata shule mbalimbali. Tuligundua kuwa ujumbe wa kunawa mikono ili kuzua ugonjwa wa korona umeandikwa kwa lugha mbalimbali kutegemea mazingira. Lugha hizi ni kama vile za Kikamba na Kiingereza. Lugha ya Kiswahili inatumika na watu wa kabila mbalimbali maeneo kama vile vituo vya mabasi na mashule. Maandishi kwenye mitungi ya maji yanadhihirisha umuhimu wa kunawa mikono. Katika eneo la Kincar, Utawala, kwenye kituo cha mabasi, mtungi wa maji ya kunawa kabla ya kuingia kwa gari umeandikwa kuwa:

“Osha mikono kwanza, corona yaua.”

Maandishi haya yameandikwa kwa lugha ya kurai na kwa namna inayoeleweka kwa urahisi. Tunasema hivi kwa kuwa Kiswahili sanifu ni kunawa mikono na wala sio kuosha mikono. Neno kunawa linaeleweka zaidi na wasomi wa Kiswahili na ndio maana halitumiki zaidi katika maandishi ya uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya virusi vya

korona. Maneno “**Osha mikono.....**” ni rahisi kueleweka na Wakenya wengi na ndio sababu yanatumika katika mitungi ya maji ya kunawa iliyo kwenye vituo vya magari ya kubeba abiria.

Vile vile, Oktoba 12, 2020, tulikutana na maandishi ya Kiswahili katika shule ya upili ya Muhuri Muchiri ilioko eneo la Ruai. Maandishi haya yalikuwa kwenye lango kuu la shule na yaliandikwa kwa Kiingereza na Kiswahili. Maandishi hayo yalisema kuwa “**Safisha mikono hapa, sote tumalize corona**” Ni muhimu kukumbuka kwamba hapa ni shuleni na ni baada ya wanafunzi kurudi shuleni baada ya kufunga Machi, 2020 kulipozuka ugonjwa wa korona nchini Kenya. Tahadhari inatakiwa kuwekwa shuleni ili kuzuia maambukizi kwa wanafunzi. Hii ndio sababu wanatumia neno *safisha* kwa maana ya kuosha kwa makini ili kumaliza virusi iwapo vipo mikononi. Neno hili linatumika shuleni kama tahadhari kwa kuwa idadi ya wanafunzi ni kubwa na iwapo basi virusi vya korona vitaingia basi madhara yake ni hatari zaidi.

Kaunti ya Mombasa ilikuwa miongoni mwa kaunti ambazo ziliathirika zaidi na virusi vya korona. Kwa hali hii basi, gavana Joho alichukua hatua kuhakikisha kuwa virusi hivyo havisambai sana. Aliwataka watu wa Mombasa kupimwa ili kuwatenga wale ambao walikuwa wameathiriwa jambo ambalo lingepunguza msambao wa virusi hivi. Ingawa hivyo idadi ndogo ya watu ilijitokeza kupimwa. Joho alichukua fursa hiyo kuwahamasisha kuhusu mtindo mpya wa maisha ambao ulinuia kulinda maisha ya Wakenya. Gavana Joho alitumia Kiingereza kutoa hotuba yake ila alianza kutumia Kiswahili ili aweze kujieleza ipasavyo na kuwashawishi Wakenya kupimwa. Hotuba yake ya Mei, tarehe 2, 2020 ilinuia kuwahamasisha watu juu ya mtindo mpya wa maisha. Alitumia Kiingereza na Kiswahili ila tutaangazia sehemu ambayo alitumia Kiswahili pekee kama ifuatavyo:

“...Hizo ndizo fitina hatutaki kwa kuwa jamani haturuhusiwi kuswali msikitini. Unafungua msikiti. Watu wanaanza kuswali, baadaye polisi waingie muanze fitina na ni nyinyi mnayaanzisha. Ukifuata sheria polisi hawawezi kuja. Kwa nini uingie msikitini? Huko ni kuhatarisha maisha ya watu. Akili yako iko wapi? Ni uzembe kiasi gani, unaingia mitandaoni, facebook, whatsapp, na Instagram kupinga na kuponda kila kitu. Mimi hunilindi..... Nimevaa maski yangu..... tuangalie jamii, watu wangapi mmezika? Lakini bado mnaongea sijui ooh, sijui hili lile, ooh

tufanyie hivi. Jiulize wewe wajifanyia nini? Jiulize watu wangapi wamekufa ulimwenguni..... Watu wamekufa wengi hata Afrika. Mnaletewa matibabu barabarani upimwe, wasuasua, hatutaki tujulikane, ni uzembe kiasi gani..... Kupimwa waletewa kwa nyumba yako, ni uzembe kiasi gani? Watu watafuta hii nafasi ya kupimwa na hawapati. Wacheni mchezo, kama mnataka kukasirika..... waweza kufa au kuua. Angalia pwani, tumezika watu 6, Mombasa yote watu 11..... bado mnalalamika. Mna kasumba ya kibiashara, mfiche rafiki, mswali pamoja, tufungue mwadhini pamoja....”

Gavana Joho anatumia lugha ya ukali na inayoashiria machungu kwa kuwa watu anaowaongoza wamekataa kufuata mtindo mpya wa maisha. Kutokana na ongezeko la visa vya virusi vya korona, serikali kupitia kwa Wizara ya Afya iliwashauri Wakenya kukaa nyumbani na wasiende hata kanisani wala msikitini. Watu wa pwani walikuwa wamepuuza ushauri huu na wakawa wanajumuika pamoja kuswali kama inavyojitokeza kwa hotuba ya Gavana Joho anaposema kuwa “**Mna kasumba ya kibiashara, mfiche rafiki, mswali pamoja, tufungue mwadhini pamoja....**” Joho anatumia lugha ya ukali hapa kwa kuwa watu wa pwani walikuwa wamekaidi masharti ya serikali ya kutoenda msikitini kuswali hadi hali itakapobadilika. Anatumia Kiswahili na kutumia ukali kuashiria kugadhabishwa kwake. Pia, lugha ya ukali imetumika kuashiria onyo kwa wanaokiuka masharti ya serikali ya kupunguza msambao wa virusi vya korona. Hizi kanuni zifaazo kufuatwa ndio mtindo mpya wa maisha. Joho anatumia lugha ya kujirejelea ili kudhihirisha kuwa watu wanatakiwa kuiga viongozi wao katika vita dhidi ya virusi vya korona. Hili linajitokeza anaposema kuwa “**Mimi hunilindi..... Nimevaa maski yangu...**” Kuvalia barakoa ni mtindo mpya na ni muhimu kwa lengo la kujikinga na kuwakinga wengine.”

Katika kisehemu hiki tumeonyesha namna viongozi na vyombo mbalimbali vya habari walivyotumia Kiswahili kuwahamasisha watu kuhusu kuukubali mtindo mpya wa maisha. Tumeonyesha kuwa viongozi wanatumia lugha ya ukali, ya kurai na vile vile kutoa onyo kama njia moja ya kuhakikisha kuwa Wakenya wamezingatia mtindo mpya wa maisha. Tumegundua kuwa Kiswahili ni lugha mwafaka katika uhamasishaji huu. Hii ni kwa sababu, Kiswahili ni lugha rasmi ya kwanza nchini na vile vile ni lugha ya taifa kwa mujibu wa katika ya 2010. Kiswahili ni lugha sambazi na hivyo basi ndio lugha

faafu katika kuwaeleza watu kuhusu mtindo mpya wa maisha ambao Wakenya wanapaswa kuukumbatia kutokana na janga la korona. Kando na kuwahamasisha Wakenya kuhusu mtindo mpya wa maisha, tuligundua pia kuwa Kiswahili kilitumika katika kuwaelimisha Wakenya kuhusu ugonjwa wa korona na hatua zinazopaswa kufuatwa ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi yake. Hii ndio maana tunashughulikia ujenzi wa elimu bora kupitia kwa matumizi ya Kiswahili katika kishemu kifuatacho.

4.5 Kujenga Elimu Bora

Wakati wa janga la korona, Kiswahili kimetumika kuanzisha na kuendeleza uzoefu unaoana na misingi ya maadili katika jamii. Katika vyombo vya habari, viongozi walizoea kusema kuwa “**kaa nyumbani**” baada ya matangazo ya biashara. Ujumbe huu umebadilisha mitindo ya maisha ya Wakenya. Wazazi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiwaacha watoto wao na walezi. Akina baba ambao hutumia pombe walikuwa wanakaa katika baa wengine hadi usiku wa manane. Wakifika nyumbani, watoto wanakuwa wamelala. Kwa hali hii, mshikamano wa jamii haukuwepo ila hali ilibadilika wakati watu walilazimika kukaa nyumbani kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona.

Vyombo vya habari vilichukua jukumu la kuwahoji madaktari wakati wa kutoa taarifa za habari ili kuwaeleza wasikilizaji na watazamaji kuhusu virusi vya korona. Kwa mfano, runinga ya Citizen ilimhoji Daktari Yubrine Moraa tarehe 22 Aprili ambaye alitumia Kiswahili kuwaelimisha watu namna ya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa korona. Matumizi ya lugha ya Daktari Moraa ni ya kuwapa Wakenya matumaini kuwa inawezekana kupunguza msambao wa virusi vya korona. Daktari aliwataka Wakenya kunawa mikono au kutumia sanitaiza pia. Moraa anawaelimisha Wakenya kuhusu njia bora za kunawa mikono na kuwataka Wakenya kuenda hospitalini bila wasiwasi wa kuambukizwa virusi vya korona. Haya yanajitokeza katika usemi wa Moraa aliposema kuwa:

“.....Watu wasiwe na uoga wa kwenda hosipitalini. Muhimu ni kufuata masharti kama kukaa umbali na mtu mwingine, ukiingia kwa matatu fungua madirisha. Tumia sanitizer ya kutosha, ipitishie ndani ya viganja na pande zote za mikono, sugua vidole vizuri kwamikono hadi ikauke.... Ukiosha

mikono, paka sabuni ya kutosha na utumie maji ya kutiririka, viini vitiririke, uweke maji kwanza na uoshe na sekunde 20.”

Daktari Moraa anatumia lugha ya kuashiria matumaini kwa kuwaelimisha Wakenya kuhusiana na njia za kujikinga dhidi ya korona. Watu walikuwa wameacha kwenda hospitalini kwa kuhofia kuwa wataambukizwa virusi vya korona. Moraa anawaeleza kuwa ni muhimu kwenda kutibiwa iwapo mtu ni mgonjwa ila wazingatie masharti ya afya. Matumizi yake ya lugha ni funzo kuu la afya hasa kuhusiana na magonjwa ya kuambukiza yatokanayo na uchafu kama vile UVIKO-19. Usemi huu wa Daktari umetolewa kwa Kiswahili kwa nia ya kuwapa watu elimu bora ya kunawa mikono. Huu ni uhamasishaji muhimu kwa kuwa Wakenya wanapaswa kubadilisha mtindo wa kunawa waliouzoa ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona.

Katika mawasiliano mema ni muhimu kwa wasemaji kuzingatia uhusiano na mazingira ya mazungumzo husika. Hili litawawezesha wasemaji kutumia lugha itakayoeleweka na walengwa wote. Viongozi wanachukua jukumu la kuwahamasisha wananchi kwa kuwaeleza kuhusu ugonjwa wa korona. Vyombo vya habari pia viliwaalika wataalamu mbalimbali ili watazamaji na wasikilizaji wao waweze kuelewa mbinu na mikakati ya kujikinga na kuwakinga wengine. Tumbaine kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yameweza kufaulu katika kuwahamasisha watu dhidi ya janga la korona.

Mitandao ya kijamii pia imehusika pakubwa katika kuwahamasisha watu dhidi ya ugonjwa wa korona. Wakati wa janga la korona, watu walitakiwa kukaa nyumbani. Hili liliwaacha watu bila shughuli nyingi za kufanya. Kwa sababu hii basi, Wakenya waliingia kwenye mtandao kujifurahisha. Asilimia kubwa zaidi ya waandishi Wakenya mtandaoni waliandika kwa kutumia Kiingereza. Ingawa hivyo, wapo wachache waliotumia Kiswahili ili kuwaeleza Wakenya kuhusu janga la korona. Kwenye facebook, katika sehemu ya Valley Wise Health Group mmoja wao kwa jina, Deborah aliandika kuwa:

“Tunazungumzia COVID-19 jinsi ya kujilinda na kulinda afya vizuri. Ukiwa na homa au kohozi au kifua kinachozidi kuongezeka, upungufu wa kupumua, kaa nyumbani. Pigia daktari wako simu kabla ya kuenda kliniki. Muulize rafiki au jamaa yako au kiongozi wa jamii akusaidie kupata daktari. Ni sawa kuwa na wasiwasi na vyema kusema ukweli ili daktari akusaidie. Atakusaidia kufanya vipimo vya COVID-19 kwa kutia pamba

kwa pua yako ambayo ni njia moja ya kujua kama una corona. Dalili za wagonjwa wanaweza kupona wakiwa nyumbani, fuata mapendekezo ya daktari, kunywa vinywaji au dawa ya homa na maumivu. Usitumie awa au kitu kisichopendekezwa na daktari, muulize daktari wako kwanza. Unaweza kujikinga ili jamaa yako wasiwe wagonjwa pia. Usiondoke nyumbani tu kwenda kutibiwa ukisikia dalili hizi ila ikiwa unataka huduma za dharura. Kaa nyumbani kwa chumba chako tu, usitembelewe na jamaa zako, ukitaka kitu piga simu, ambia mtu alete chakula aache mbele ya mlango wako. Asishike mlango, msikumbatiane au kubusu, funika mdomo unapokohoa ili kuzuia kueneza. Ukiona hauna nyumba ya kutosha kaa katika nyumba iko kando na usitoke ndani, tumia choo tofauti, safisha pande zote umegusa, usitumie vitu vya watu wengine, safisha mikono baada ya kukohoa. Jiepushe na ujumbe wowote usiotoka kwa daktari.”

Mwandishi wa ujumbe huu ametumia lugha sahili ili aweze kueleweka ipasavyo. Hii ni lugha ya maelezo na ambayo ni muhimu katika kuwaelimisha Wakenya dhidi ya virusi vya korona. Ujumbe huu kwenye mtandao umeandikwa kwa Kiswahili na ni lugha shawishi na ya kuelimisha. Ni ujumbe wa kuwaelimisha Wakenya kuhusu yale wanayopaswa kufanya ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya janga la korona. Vile vile, unaelimisha kuhusu mambo ambayo mtu anatakiwa kuyafanya iwapo atapatwa na dalili za virusi vya korona. Hii ni elimu bora kwa kuwa usemi wa Deborah unawaeleza watu jambo ambalo wanatakiwa kulifanya baada ya kupata virusi vya korona. Anawaelimisha watu namna wanapaswa kujitenga anaposema kuwa “...**ukitaka kitu piga simu, ambia mtu alete chakula aache mbele ya mlango wako. Asishike mlango, msikumbatiane au kubusu, funika mdomo unapokohoa ili kuzuia kueneza...**” Usemi huu wa Deborah ni wa kimaelezo na unaelimisha watu umuhimu wa kujitenga kabisa mtu anaposhuku kuwa ana virusi vya korona. Elimu hii ni muhimu kwa kuwa Wakenya wanapaswa kuhamasishwa kwa lugha wanayoielewa vizuri. Hii ni lugha ambayo maelezo yake hujitokeza wazi bila kuhitaji maelezo ya ziada.

Kiswahili kimetumika kuwaelimisha Wakenya na kuwafanya kufuata kanuni zilizowekwa na Wizara ya Afya. Tarehe 2, Aprili, Waziri wa Afya, Kagwe alianza kwa kutumia Kiingereza ila alipofika mahali alitaka Wakenya wajue kuwa ugonjwa wa korona uko, alianza kutumia Kiswahili. Hii ni kwa sababu alitaka aeleweke ipasavyo. Huu ni wakati ambao Wakenya walitumia lugha inayoashiria kutoamini viongozi na

kudai kuwa serikali inasema kuwa kuna virusi vya korona ili iweze kupata msaada kutoka nje. Jambo hili lilimuudhi Waziri Kagwe ambaye aliwataka Wakenya kufuata sheria zilizowekwa ili kupunguza msambao zaidi. Kwake basi Kiswahili kikawa lugha mwafaka ya kutoa maelezo kwa Wakenya. Alitoa hotuba yake kwa Kiingereza na Kiswahili ila tutaangazia sehemu aliyotumia lugha ya taifa tu ifuatavyo:

“.....Leo hii watu wameambukizwa ni 110 kumaanisha virusi iko kila pahali. Nawasihi wanaozungumza mtaani hakuna virusi hawajui yoyote amepatwa na virusi au amekufa. Wewe hujui watu, ndugu yako au rafiki ni kwa sababu hatutaki ujue yeyote ndio maana tunawahimiza kufanya vile serikali inasema usipate mtu wako wa karibu ako nayo. Jikinge wewe mwenyewe. Wale wanahudumu manduka, matatu na bodaboda tumia vitambaa vya uso. Watu wengi wamepata virusi huwezi wacha kusema huwezi kupata. Abiria wameambukizwa. Siku mbili tutawaletea hizi vitambaa zingine zinazoundwa vijijini na serikali ifuatilie kuona hakuna mtu atabebwa bila kutumia kitambaa. Msiseme tumekuwa wakali eti tunawasukuma, tunataka Wakenya waishi.....”

Waziri Kagwe anatumia lugha ya kuonya Wakenya ambao hawaamini kuwa ugonjwa wa korona uko. Lugha hii ya kuonya ni muhimu kwa Wakenya ambao walikuwa wanakaidi masharti ya serikali hasa baada ya kuwahamasisha dhidi ya virusi vya korona. Vile vile, Waziri anafichua kuwa Wakenya hawajui waathiriwa wa ugonjwa wa korona kwa kuwa serikali imefanya kuwa siri kwa sababu za kiusalama. Hili linadhihirika anaposema kuwa **“...Wewe hujui watu, ndugu yako au rafiki ni kwa sababu hatutaki ujue yeyote ndio maana tunawahimiza kufanya vile serikali inasema usipate mtu wako wa karibu ako nayo.”** Waziri Kagwe anatumia Kiswahili anapowaelimisha Wakenya ili kuweza kueleweka zaidi na hivyo anazingatia hadhi za lugha kwa mujibu wa katiba ya Kenya. Hii inaonyesha kuwa Kiswahili kina nafasi muhimu katika kuwaelimisha Wakenya kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19.

Waziri Kagwe anawataka Wakenya kuwa anatumia lugha inayoashiria kuwa virusi vya korona huweza kuwaathiri bila kubagua kwa misingi ya kazi wazifanyazo. Waziri Kagwe anatumia lugha ya kuwarejelea watu mahsusi kuashiria kuwa hakuna anayesazwa na virusi vya korona. Haya yanadhihirika anaposema kuwa **“Jikinge wewe mwenyewe.**

Wale wanahudumu maduka, matatu na bodaboda tumia vitambaa vya uso. Watu wengi wamepata virusi huwezi wacha kusema huwezi kupata.”

Kisa cha kwanza cha mwathiriwa wa ugonjwa wa korona kiliripotiwa mwezi Machi tarehe 12. Serikali iliwataka Wakenya kuchukua tahadhari ili kuzuia janga hili kusambaa kama ilivyokuwa katika nchi kama vile Uchina. Ilipofika mwezi wa Aprili, visa vya waathiriwa viliendelea kuongezeka na ndio maana serikali iliwataka Wakenya kuvalia barakoa. Wakenya walidhihirisha kuwa hawakutaka kuzivalia na ndio sababu Wizara ya Afya ilichukua jukumu la kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kuvalia barakoa. Hotuba ya waziri kagwe inaonyesha kuwa Wakenya watalazimika kuvaa barakoa kwa kuwa serikali itachukua hatua dhidi ya watu wanaokiuka agizo hili. Hili linadhihirika Kagwe anaposema kuwa “...**serikali ifuatilie kuona hakuna mtu atabebwa bila kutumia kitambaa.**” Waziri anatumia lugha ya kuonya kwa nia ya kuwashawishi Wakenya. Lugha ya kuonya ilikuwa mwafaka baada ya Wakenya kukosa kufuata masharti Waziri alipotumia lugha ya kurai.

Tumeonyesha kuwa viongozi na Wakenya wengine walitumia lugha ya kushawishi, ya kuonya na vile vile ya kurai kama njia ya kuwataka watu kufuata masharti yaliyotolewa na Wizara ya Afya. Tumbaini pia kuwa wasanii wa nyimbo waliwahamasisha watu dhidi ya virusi vya korona kupitia kwa uimbaji wao kama inavyojitokeza katika sehemu ifuatayo.

4.6 Kiswahili Kama Lugha Ya Uhamasishaji Dhidi Ya Janga La Korona Kupitia Kwa Muziki

Uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona ulifanywa na watu mbalimbali kukiwemo viongozi. Baada ya kuzuka kwa virusi vya korona na kuthibitishwa kuwa vimeingia nchini Kenya mwezi wa Machi, 2020, Wizara ya Afya ilichukua jukumu la kuwahamasisha Wakenya dhidi yake. Kando na serikali, tumbaini pia kuwa muziki ni nyenzo muhimu katika kuhamasisha raia. Hili linajitokeza katika nyimbo ambazo zinazungumzia masharti yanayopaswa kufuatwa ili kuzuia maambukizi zaidi ya ugonjwa wa korona.

Wanamuziki mbalimbali walichukua fursa hiyo na kutunga nyimbo za kuwahamasisha raia. Wapo wanamuziki waliotumia lugha ya Kiingereza katika nyimbo zao za hamasisho

dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 kama vile wimbo wa Bobi Wine ambaye ni mwanamuziki na mwanasiasa nchini Uganda. Mwanamuziki huyu ametumia Kiingereza katika wimbo wake unaohusu janga la korona na ambao unachezwa hata nchini Kenya. Kwa upande mwingine, wanamuziki Diamond na Koffi Olomide wameimba wimbo unaowahamasisha watu kuzingatia masharti Wizara ya Afya kwa lugha ya Kiswahili. Wimbo wao unachezwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari nchini Kenya pia. Wimbo huu una nafasi muhimu katika kuhamasisha watu kuhusu namna ya kupunguza maambukizi zaidi ya virusi vya korona. Yaliyomo katika muziki huu yanathaminiwa ili kuona ni kwa kiasi gani athari zake zaweza kuwa ama chanya au hasi kwa suala zima la vita dhidi ya kuenea kwa virusi vya korona. Yaliyomo katika muziki huu yamepatikana kwa Youtube na yametufaa katika utafiti huu. Tutazingatia sehemu ya wimbo huu ambapo Kiswahili kimetumika na kuonyesha athari zake kwa Wakenya. Wimbo huo ni kama ifuatavyo:

Usiniguse, usinitouch

Tusalimiane kwa miguu

Usiniguse usinitouch

Tusalimiane kwa miguu

Ooh nasema usiniguse, usinitouch

Salamu iwe kwa miguu

Tusigusane, usiniguse, usinitouch

Salamu iwe kwa miguu

Ooh kwanza kaa mbali

Corona coro

Corona coro

Mwenzako naogopa

Corona coro.....

Corona coro

Tena vaa maski

Corona coro

Corona coro

Mikono yako kuosha

Corona coro....

Corona coro.....

Wimbo wa wanamuziki Olomide na Diamond unaangazia masharti yanayopaswa kufuatwa ili kujikinga na kuzuia maambukizi zaidi ya virusi vya korona. Katika wimbo huu, Olomide na Diamond wametumia mitindo mbalimbali ya lugha kuwasilisha ujumbe kwa raia. Mbinu hizi ni kama vile urudiaji, kufupisha maneno na kuchanganya ndimi. Mbinu ya urudiaji hutumiwa kwa nia kusisitiza jambo. Katika wimbo huu, maneno **usiniguse** na **corona** yamerudiwa. Kutokana na urudiaji wa maneno haya, tunaweza kusema kuwa waimbaji wanawataka watu wasisalimiane kama ilivyokuwa kawaida. Waimbaji hawa wanarudia maneno kwa nia ya kusisitiza na kuonyesha kuwa ni muhimu kufuata masharti yaliyowekwa ili kupunguza maambukizi zaidi ya virusi za korona. Tunaweza kusema kuwa urudiaji wa maneno haya katika wimbo huu ni muhimu kwa kuwa wasikilizaji wataelewa zaidi sehemu ambazo hurudiwarudiwa. Kwa hali hii basi, wasikilizaji wa wimbo husika wataweza kujua mambo wanayopaswa kufanya ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona. Neno korona limetajwa mara 8 katika wimbo huu na hili ni jambo linalodhihirisha kuwa wimbo huu unahusu janga la korona. Tunasema hivi kwa sababu ndio neno ambalo limetajwa kwingi zaidi ikilinganishwa na maneno mengine katika wimbo huu. Urudiaji huu unaashiria kuwa msisitizo uko kwenye kudhihirishia watu kuwa virusi vya korona ni hatari na hivyo basi ni muhimu kujikinga.

Waimbaji wa wimbo huu pia wametumia mbinu ya kufupisha maneno kwa nia ya kujieleza ipasavyo. Neno **coro** limefupishwa kutoka kwa neno corona. Katika wimbo huu, neno hili linafuatana na neno corona. Hali hii inajitokeza katika misitari mbalimbali kukiwemo wa 10 na 11 waimbaji wanapoimba **corona coro**. Tunaweza kusema kuwa waimbaji wanafupisha neno korona ili kumuacha msikilizaji kujikamilishia wimbo

unapoimbwa. Mtindo huu ni muhimu kwa kuwa wasikilizaji wataweza kuhusika kikamilifu wimbo unapoimbwa na hivyo basi ataelewa ujumbe ipasavyo. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa mtindo wa ufupishaji umesaidia katika uhamasishaji wa raia dhidi ya janga la korona kwa kuhusishwa kikamilifu. Mtindo huu basi ni muhimu katika kuwahamasisha raia kuhusu njia za kupunguza maambukizi zaidi ya virusi vya korona miongoni mwao.

Olomide na Diamond pia wametumia mtindo wa kuchanganya ndimi katika wimbo uliopo hapo juu. Neno **usinitouch** limetokana na muungano wa viambishi vya Kiswahili **usini-** na mzizi **touch** wa Kiingereza. Mbinu hii ya kuchanganya ndimi ni muhimu katika wimbo huu. Matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi katika wimbo huu yanaashiria pia hali ya msisitizo. Tunasema hivi kwa sababu neno **usinitouch** linatokea baada ya neno **usiniguse**. Maneno haya mawili yana maana sawa ingawa wanayatumia katika sentensi moja. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa wanamuziki Olomide na Diamond wanachanganya ndimi kwa nia ya kusisitiza kuwa watu wasisalimiane na vile vile wanapaswa kukaa mbali na mwingine. Uhamasisho huu kutoka kwa wanamuziki hawa ni muhimu katika kusaidia kupunguza maambukizi zaidi. Kwa hali hii. Tunaweza kusema kuwa nyimbo zilizoandikwa kwa Kiswahili ni muhimu katika kuwahamasisha Wakenya dhidi ya janga la korona.

4.7 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia nafasi ya Kiswahili katika uhamasishaji dhidi ya janga la korona. Tumeonyesha kuwa Kiswahili ni lugha unganishi na kitambulishi cha taifa la Kenya. Kwa hali hii basi, Kiswahili ni lugha mwafaka katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya virusi vya korona. Tumethibitisha hili kwa kuangazia mahojiano baina yetu na Wakenya wa maeneo mbalimbali. Kutokana na maoni yao, tunaweza kusema kuwa Wakenya wengi walielewa ujumbe uliotolewa kwa lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na ule unaotolewa kwa Kiingereza na lugha zingine. Hii ina maana kuwa Kiswahili kina nafasi muhimu katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona.

Tumegundua kuwa Wakenya huuelewa zaidi ujumbe unaotolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu ni lugha yao ya taifa. Viongozi ambao hutumia Kiswahili katika kuwahamasisha watu dhidi ya virusi vya korona walieleweka kwa urahisi na hili ni jambo

ambalo liliwafanya watu kufuata masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya. Kwa hali hii uhusiano na mazingira ni muhimu katika kuteua na kutumia lugha ambayo hueleweka na walengwa na katika muktadha wa utafiti huu wa Wakenya. Mbinu ambazo zimetumiwa na viongozi na wanamuziki ni kama vile urudiaji, ufupishaji wa maneno, matumizi ya lugha ya maelezo na vile vile ya kuonya. Katika sura ifuatayo, tunatoa muhtasari wa utafiti wetu pamoja na mahitimisho na vile vile mapendekezo kwa tafiti za baadaye kuhusiana na mada yetu ya utafiti.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

5.1 Utangulizi

Sura hii, ndio ya mwisho katika tasnifu hii na tunashughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti huu. Tumeangazia maswali ya utafiti wetu na kubaini kama yanaafikiana au kukinzana na matokeo ya utafiti wetu. Hatimaye tumetoa mapendekezo kwa tafiti za baadaye kuhusiana na mada ya utafiti huu na vile vile tumeorodhesha changamoto ambazo tulikumbana nazo wakati wa kukusanyaji data kwa ajili ya utafiti wetu.

5.2 Muhtasari

Katika sura ya kwanza, tumeangazia utangulizi wa tasnifu hii kwa jumla ambapo tumeonyesha suala kuu la utafiti huu. Katika utafiti huu, tumeongozwa na malengo matatu katika kushughulikia tatizo la utafiti wetu. Malengo hayo ni: kwanza, kubaini athari za lugha ya utangazaji na uhamasishaji wa wananchi wa Kenya kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 kwa kurejelea vibadala mbalimbali vya kijamii, pili, kujadili nafasi ya Kiswahili, Kiingereza, lugha za asili, lugha ishara na Sheng' katika utangazaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya janga la UVIKO-19, tatu ni kubaini changamoto za kijamii na zile za kimatibabu ambazo hudhihirika baada ya kupuuza katiba ya Kenya kilugha katika kuwahamasisha raia wake kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19.

Tuliongozwa na nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Wilson (1995) na ile ya utekelezaji kama ilivyoelezwa na Spencer (1971). Kutokana na data ya utafiti huu, tunaweza kusema kuwa ni kweli kwamba mawasiliano huongozwa na kanuni ya uhusiano. Hali hii imejitokeza pale ambapo Wakenya walikuwa na tafsiri tofauti tofauti kuhusu jambo fulani ambalo lilikuwa limesemwa na viongozi kuhusu namna ya kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya virusi vya korona. Tafsiri hizi tofauti zilitokana na matumizi ya lugha ya viongozi na wadau wengine katika sekta ya afya. Tumeonyesha kuwa viongozi, hasa Waziri wa Afya Bw. Mutahi Kagwe walipendelea Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Huu ni ukiukaji wa katiba ya Kenya ya 2010 ambayo ilikifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa na vile vile lugha ya kwanza rasmi na Kiingereza kuwa ya pili. Hali hii imethibitisha kuwa suala la utekelezaji wa katiba kwa misingi ya hadhi ya lugha

mbalimbali halijatiliwa maanani. Tumeonyesha pia umuhimu wa vyombo vya habari katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Nyimbo za wanamuziki zilizohusu virusi vya korona pia zilichezwa katika vyombo vya habari. Hata hivyo, tumebaini kuwa nyingi ya nyimbo hizo zimetungwa kwa lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, tunaweza kusema kuwa nadharia ya uhusiano na ile ya utekelezaji zinaakisi mada ya utafiti huu ambayo ni lugha katika katiba ya Kenya na ujitokezaji wake katika utangaziaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya UVIKO-19.

Utafiti huu ni wa uchambuzi ubora na hivyo basi, tulitumia data ambayo ilituwezesha kutimiza malengo yetu bila kuzingatia idadi ya watafitiwa. Hii ndio maana tulizingatia hotuba za viongozi wachache nchini Kenya hata ingawa wengi walihusika katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19. Vile vile, tumeangazia wimbo wa wanamuziki wachache na hasa ulioimbwa kwa Kiswahili. Tulikusanya data yetu kwa kusikiliza hotuba za viongozi mbalimbali katika vyombo vya habari kama vile redio na runinga. Vile vile, tulipata data katika mtandao wa You tube na hatimaye tumechanganua data yetu kwa njia ya kinadhari.

5.3 Mahitimisho Ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kuchanganua lugha katika katiba ya Kenya na ujitokezaji wake katika utangaziaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19. Ugonjwa huu ulikuwa ukisambaa kwa haraka na ndiposa serikali ilichukua jukumu la kuwahamasisha Wakenya dhiki yake kwa nia ya kupunguza maambukizi zaidi. Katika utafiti huu, tuliongozwa na malengo matatu na ambayo tutayatolea mahitimisho katika visehemu vifuatavyo:

5.3.1 Athari Za lugha Ya Utangaziaji Na Uhamasishaji Wa Wananchi Wa Kenya Kuhusu Ugonjwa Wa UVIKO-19

Tumeonyesha kuwa katiba ya Kenya imezipa lugha mbalimbali hadhi. Kulingana na katiba ya 2010, Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile ni lugha ya kwanza rasmi ikifuatwa na Kiingereza. Hii ina maana kuwa Kiswahili kimepewa hadhi kuu ikilinganishwa na Kiingereza. Ingawa hivyo, tumeonyesha kuwa viongozi wengi walikuwa wanatumia Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Vile vile, katiba ya

2010 inazitambua lugha za asili na lugha ishara. Hii ina maana kuwa lugha hizi zinapaswa kutumiwa katika uhamasishaji wa umma dhidi ya virusi vya korona. Kwa kufanya hivi, Wakenya wataweza kuuelewa ujumbe kwa kusikiza lugha anayoipendelea zaidi. Ni kwa misingi hii basi ambapo tunasema kuwa lugha ya utangaziaji na uhamasishaji dhidi ya UVIKO-19 huweza kuwafanya baadhi ya Wakenya kuufasiri ujumbe visivyo. Ufasiri wa ujumbe kwa namna tofauti na ilivyokusudiwa na viongozi huwafanya Wakenya kupuuza kanuni zinazowekwa na Wizara ya Afya kwa nia ya kupunguza maambukizi zaidi. Vile vile, matumizi ya lugha moja badala ya nyingine na bila kuzingatia katiba ya Kenya ya 2010 huweza kuwafanya watu kukosa kusikiza hotuba za uhamasishaji dhidi ya UVIKO-19. Kwa hivyo basi, juhudi za serikali za kuhamasisha umma dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 zinarudishwa nyuma kwa kukosa kutekeleza katiba ya Kenya kilugha.

5.3.2 Nafasi Ya Kiswahili, Kiingereza, Lugha Za Asili, Lugha Ishara Na Sheng’ Katika Utangaziaji Na Uhamasishaji Wa Umma Dhidi Ya Janga La COVID-19

Kutokana na data ya utafiti huu, tunaweza kusema kuwa Kiswahili, Kiingereza, lugha za asili, lugha ishara na Sheng’ zina umuhimu mkubwa katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Tumeonyesha kuwa Wakenya walielewa zaidi ujumbe uliotolewa kwa lugha ya Kiswahili zaidi ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza. Vile vile, tunaweza kusema kuwa viongozi walipaswa kutilia maanani matumizi ya lugha ya Sheng’ kwa vile ndio inayopendelewa zaidi na vijana hasa wale wa mijini. Hii ina maana kuwa vijana hawa hupendelea kusikiza hotuba na matangazo katika Sheng’. Lugha ishara ndio lugha ya taifa na vile vile rasmi kwa walemavu wa kusikia na kuongea nchini Kenya. Watu hawa hupata ujumbe kupitia kwa ishara zinazotolewa na wala sio mazungumzo. Kwa hivyo basi, wao wanaelewa ujumbe unaotolewa kwa ishara na hivyo basi kuchukua hatua mwafaka. Kwa upande mwingine, wapo watu, hasa vijijini ambao hupendelea lugha zao za asili. Wao husikiza matangazo kwa lugha zao za asili na hivyo kuchukua hatua zinazofaa. Hii ina maana kuwa Wakenya ni wanawingilugha ila kila mmoja huwa na lugha anayoipendelea na ndio maana ni muhimu kuzingatiwa katika uhamasishaji dhidi ya janga la korona.

5.3.3. Changamoto Za Kijamii Na Zile Za Kimatibabu Ambazo Hudhihirika Baada Ya Kupuuza Majukumu Ya Lugha Za Kenya Kikatiba Katika Kuwahasisha Raia Wake Kuhusu Ugonjwa Wa UVIKO-19

Katika utafiti huu tulibaini kuwa upuuzaji wa majukumu ya lugha kama inavyojitokeza katika katiba ya mwaka wa 2010 hupelekea Wakenya kufasiri ujumbe visivyo. Hali ya kufasiri ujumbe visivyo hasa kuhusiana na uhamasishaji dhidi ya janga la korona iliwafanya baadhi ya Wakenya kutofuata kanuni zilizotolewa na Wizara ya Afya. Kanuni hizi zilikuwa muhimu kwa kuwa zilikusudiwa kupunguza maambukizi zaidi ya virusi vya korona. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa kupuuza kanuni kulipelekea kusambaa kwa virusi vya korona nchini Kenya.

5.4 Changamoto za Utafiti

Katika kukusanya data ya utafiti huu tulikumbana na changamoto kadhaa na ni muhimu kuzitaja hapa. Ugonjwa wa UVIKO-19 ulikuwa mpya kwetu na kwa taifa nzima. Kwa hali hii basi, ilikuwa vigumu kupata misamiati ya Kiswahili kurejelea dhana fulani fulani. Hivyo basi, tulijipata tukirejelea ugonjwa wenyewe kama ‘korona’ na wakati mwingine ‘corona’. Vile vile, sajili ya matibabu huwa na misamiati maalum na ambayo wakati mwingine inakuwa vigumu kupata dhana faafu kwa Kiswahili. Hali hii ya kufasiri majina kutoka kwa Kiingereza hadi kwa Kiswahili ilituwia changamoto ila tunashukuru kuwa tulijitahidi na kukamilisha tasnifu hii kwa wakati ufaao.

Changamoto nyingine tuliyokumbana nayo ni kuwa idadi kubwa ya viongozi walikuwa wanatumia lugha ya Kiingereza kutoa hotuba zao na kwa hali hii basi tulilazimika kufanya tafsiri. Hili lilitufanya kutumia muda mwingi katika kuwasilisha data ya utafiti wetu. Pia, tulilazimika kupata data kutoka kwa mtandao na hili lilikuwa gharama kubwa kifedha kwa upande wetu. Hata hivyo, licha ya kupitia changamoto tulizozitaja tuliweza kukamilisha tasnifu hii kwa wakati ufaao.

5.5 Mapendekezo

Katika utafiti wetu, tulibanwa na upeo na mipaka yetu na kwa hiyo kuna mambo tuliyoyaacha nje na ambayo yanaweza kutafitiwa kuhusiana na lugha katika katiba ya Kenya na ujitokezaji wake katika utangazaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya janga

fulani. Wakati wa kukusanya data tuligundua kuwa yapo mambo mengine ambayo yanaweza kutafitiwa hasa kuhusiana na umuhimu wa lugha ya uhamasishaji wa umma dhidi ya janga fulani. Kwa hivyo, tungependekeza ifuatavyo:

1. Katika utafiti huu, tulizingatia hotuba za viongozi wa kitaifa na vyombo vya habari ambavyo hutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kupeperusha matangazo yao. Kwa hali hii tungependekeza watafiti wa baadaye wazingatie vyombo vya habari ambavyo hupeperusha matangazo kwa lugha za asili za Kenya ili kuchambua namna viongozi wa mashinani hutumia lugha wakati wa uhamasishaji.
2. Vile vile tungependekeza kuwa watafiti wa baadaye watumie nadharia nyingine kushughulikia lugha katika katiba ya Kenya na ujitokezaji katika uhamasishaji wa umma dhidi ya janga fulani.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M. na Osinde, K. (1997) Sheng' and Engsh: Development of Mixed Codes among the Urban Youth in Kenya. *International Journal of the Sociology of Language* 125 (Sociolinguistic Issues in Sub-Saharan Africa) pp.4 5-63.
- Ali, J.N. (2011) Changamoto Zinazokumba Mawasiliano ya Kiofisi Kwa Kutumia Kiswahili kama Lugha Rasmi. Tasnifu ambayo haijachapishwa ya Chuo Kikuu cha Katoliki cha Afrika Mashariki.
- Amolloh, Sh. (2012) Sera Mpya ya Lugha Nchini Kenya: Changamoto za Utekelezaji wa Matumizi Rasmi ya Kiswahili kama Lugha ya Kufundisha katika Shule za Msingi. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Cha Nairobi ambayo Haijachapishwa.
- Bamgbose, A. (1991) *Language and Nation: The Language Question in Sub-Sahara Africa*. England: Eanglewood University Press.
- Bosire, M. (2009) What Makes a Sheng' Word Uniquelexical Manipulation in Mixed Language? *Selected Proceedings of The 39th Annual Conference on African Linguistic Somerville M.A.*
- Carston, R. (2002) *Thoughts and Utterances: The Pragmatics of Explicit Communication*. Wiley: Blackwell.
- Fink, T.K. (2005) Attitudes Towards Languages in Nairobi. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa ya Chuo Kikuu cha Pittsburg.
- Franco, P.C. na Galvis, A.H. (2013) The Role Of Situational Context And Linguistic Context When Testing EFL Vocabulary Knowledge In A Language Teacher Education Program: A Preliminary Approach. *Colombian Applied Linguistics Journal*. Vol.15 no.1 Bogota Jan./June 2013.
- Githinji, P. (2008) Ambivalent Attitudes: Perceptions of Sheng' and its Speakers. Ohio University: *Nordiac Journal of African Studies*. 17(2), 113-136.

- Githiora, C. (2002) Sheng: Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? *Journal of African Cultural Studies*, Vol. 15, No. 2, (Dec., 2002), pp. 159-181
 Imechapishwa na: Taylor na Amp; Francis, Ltd. Stable URL:
<http://www.jstor.org/stable/3181415>
<https://www.standardmedia.co.ke>
<https://www.unicef.org>
<https://www.who.int/health-topics>.
- Iribemwangi, P. na Mukhwana, A. (2011) *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers.
- Iribemwangi, P. (2020) A River From Rivulets? A Study Of Sheng' Vis-à-vis Indigenous Kenyan Languages And Modern Technology. *Asian Journal Of African Studies* Vol.49/ August 2020.
- Johnson, D.C. (2013) *What is Language Policy? In Language Policy, Research and Practice in Applied Linguistics*. London: Palgrave Macmillan.
- Kiango, J. G (2002) Nafasi Ya Kiswahili Katika Ujenzi Wa Jamii Mpya Ya Afrika Mashariki. *Nordic Journal of African Studies* 11(2): 185-197 (2002).
- Kibui, A.W (2014) Language Policy In Kenya And The New Constitution For Vision 2030. *International Journal Of Educational Science And Research*, Vol.4.
- Kiio, M.M (2017) Utayari wa Wakenya katika Utekelezaji wa Sera ya Lugha ya Kiswahili kama Lugha Rasmi Nchini Kenya, Kaunti ya Nairobi. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Kinoti, T. M. (2019) Dhima Ya Kiswahili Katika Uimarishaji Wa Utamaduni na Mazingira Kwa Mujibu wa katiba Ya Kenya. *East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature*. Vol 2, issue-9, Sept-2019
- Mathooko, P.M. (2007) *Isimujamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njigua Books.
- Mbaabu, I. (1996) *Language Policy in East Africa*. Nairobi: Educational Research Publication

- Mekacha, D.K. (2011) *Isimujamii: Nadharia na Mukstadha wa Kiswahili*. Dar Es Salaam: TUKI
- Mirianga, R.K. (2014) Mielekeo ya Walimu wa Shule za Msingi Kuhusu Suala la Lugha Kama Linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Mohochi, E.S. (2002) Kiswahili na Vyombo vya Habari Nchini Kenya: Matatizo katika Matumizi ya Lugha ya Kiswahili. *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja. Cape Town: CASA. Uk. 147-157.*
- Momanyi, C. (2009) The Effects of Sheng' in Teaching Of Kiswahili in Kenyan Schools. *The Journal of Pan African Studies 2.8 (2009): 127-138.*
- Mweri, J. G. (2016) The Acquisition Of Kenyan Sign Language And Its Significance As A Mother Tongue and Medium Of Instruction In Schools For The Deaf In Kenya. *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics, Vol. 5 (2016), 85-100.*
- Msanjila, Y.P (2012) Nafasi Ya Lugha Za Asili Katika Shirikisho La Afrika Mashariki. *African Journals Online, eISSN: 0023-1886*
- Mukhwana, A. (2008) Language Attitudes in Urban Kenya: The Case Study of Kisumu, Nairobi and Mombasa. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijchapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Musau, P.M. (2001) Freeing the Airwaves or Cultural Enslavement: The Case of Media in Kenya: A Tool for Development. *The Multidisciplinary Approach. Eldoret: Moi University Press. Pp 36-42.*
- Ngige, B.N.(2014) Mielekeo na Changamoto za Maafisa wa Kaunti katika Utekelezaji wa Katiba Kuhusu Sera ya Lugha: Mfano wa Kaunti ya Nakuru. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
- Ngugi, P. na Chacha, L. (2004) *Sociolinguistics*. Nairobi: KUIOL.
- Njoroge, W. F. (2014) Hali, Hadhi Na Majukumu Ya Sheng' Mjini Nakuru. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijchapishwa.

- Ogechi, N. O. (2003) On Language Rights in Kenya. *Nordic Journal of African Study*, 12, 277-295
- Ogola, J.O. (1990) Mielekeo ya Wasomi Kuhsu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Nchini Kenya. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Ontieri, J. (2017) Nafasi ya Kiswahili kama Lugha Rasmi Nchini Kenya: Majukumu na Changamoto. *Journals.udsm.ac.tz/index.php*.
- Shitemi, L.N. (2011) *Kubidhaaisha na Kuwezesha Lugha Kama Sarafu ya Kiuchumi na Kijamii: Kielelezo cha Taaluma za Kiswahili na Tafsiri*. Kenya: Moi University Press.
- Spencer, J. (1971) Colonial Language Policies and Their Legacies. In Sebeok, Thomas (ed). *Current Trends in Linguistics*, vol, 537-547. The Hague: Mouton de Gruyter.
- Sperber, D. na Wilson, D. (1995) *Relevance: Communication and Cognition*. Wiley: Blackwell
- _____ (2002) *Relevance Theory: Psychology and Language Sciences*. Wiley: Blackwell.
- The Constitution Of Kenya, 2010- Kenya Law Reform Commission.
<http://www.klrc.go.ke>.
- Wardhaugh, R. (1986) *An Introduction to Sociolinguistics*. New York: Blackwell Publishers.

DATA YA UCHANGANUZI

Data hii ilikusanywa kutoka kwa mitaa mbalimbali katika Kaunti ya Nairobi na Machakos. Tumeyahifadhi maandishi haya katika hali yake halisi bila kurekebisha makosa ya kisarufi na ya tahajia.

1. Wakaazi wa eneo la Pipeline, Embakasi

Mtafiti: Rais amesema kuwa watu wafanye kazi wakiwa nyumbani ili kuzuia maambukizi, kutokana na kipengele hiki wewe umeelewa nini?

1. M1: Sasa anasema tufanyie kazi home aje sasa hivo?
2. M2: Ati critical services ni gani tena? Hata hii yangu ya kuuza matunda ni critical ala.
3. M1: Imagine hii kitu ya kuwork from home haiwes make kwa mahustler kama sisi. Juu ni lazima tukatafutie familia kila siku.
4. Mtafiti: Na wewe mama umeelewa nini kutokana na hii mambo ya kukaa nyumbani isipokuwa tu watu wa critical services?
5. M3: Sasa wee ukiona tutakula nini tukikaa nyumbani au watatupea food sisi wote? Hii serikali ina mambo haki.
6. Mtafiti: Naelewa, lakini unajua serikal inafanya hivi kwa manufaa yako mwenyewe ndio usiambukizwe korona.
7. M3: Sasa unajua ni kweli lakini pia lazima tumange vizuri ndio hii magonjwa isituweze sana.
8. M2: Hii gava hata haijalingi sisi watu wa chini. Masonko saa hii ndio wanasikia poa tu.
9. M1: Maviongozi wetu ndio mafala tu, saa hii wanafikiria tu vile wataunda doo kutoka kwa hii korona.
10. M3: Wee hii Kenya yetu mwenye ako nayo ndio anaongezewa. Wewe mwenye hauna kakitu ndio unateseka.
11. Mtafiti: Lakini mnajua kuwa COVID-19 haujui tajiri na maskini. Inaffect kila mtu na ndio maana ni vizuri kuzingatia masharti ambayo yamewekwa na Wizara ya Afya.
12. M2: Mimi hata sijasikia mtu mwenye najua amekuwa na hii ugonjwa.

13. M1: By the way, hii inaweza kuwa stori tu za gava za kutafuta msaada si kitu ingine.
14. M3: Shida ni kutuweka hapo ati kaa nyumbani na lock down bila kujua watu wataamanga nini. Hata njaa inauma bwana.
15. M1: Unye ananisinya siku hizi anafikiria kila msee alipata mali kutoka kwa mababa zao kaa yeye. Wengine lazima tuhustle tupate ya Sukuma.
16. Mtafiti: Nawaelewa ila

2. Waendeshaji pikipiki katika eneo la Katani

1. M1: Mzee anamaanisha kuwa matourist ndio wako na hii virusi. So mimi hata siwezi pata nikiwa hapa mashamba.
2. M2: Hata yeye anajua kuwa hii ugonjwa ni ya masos, kwani sisi huenda hizo bar na mahoteli wanaenda, hapana sisi hapa katani hakuna hiyo ugonjwa.
3. M3: Kwanza wewe nikuulize, umeona corona kweli, au kuna mtu wenu ako na korona? Serikali inatuchesa tu ipate doo kutoka ng'ambo.
4. M4: Mi najua hakuna korona na hata hiyo stori hainibambi juu tunacheswa kaa watoi, wakubwa wakiunda pesa.
5. Mtafiti: You mean hamuamini kuwa corona iko?
6. M3: Madam, hii stori haina base juu sisi hapa hakuna msee amewahi kupimwa.
7. M2: Hata bro yangu mwenye anaendeshanga matrela alinishow kuwa wao wanapimangwa before waingie Ug na eti wanaambiwa gava inataka number fulani ya watu ipatikane na korona.
8. M1: Waah so hii vitu ni ya kuunda tu doo na.....
9. M4: Si niliwaambia, nikucheswa tunacheswa tu na hawa wakubwa.
10. M3: Wacha nihustle watoto wangu wasiteseke na njaa.

Mtafiti: Sawa, siku njema.

3. Wakenya wa eneo la Katani, kaunti ndogo ya Athi River

Mtafiti: Bwana Kibicho amesema kuwa "...This is not a joke, in the coming weeks, its important to enforce government measures like no gathering within the streets..... Stay at

home.....People are getting sick through contacts with tourists who have been to bars and hotels. We don't know who is sick, this is not business as usual.” Je, umelewa nini kutokana na usemi huu?

1. M1: Mzee anamaanisha kuwa matourist ndio wako na hii virusi. So mimi hata siwezi pata nikiwa hapa mashamba.
2. M2: Hata yeye anajua kuwa hii ugonjwa ni ya masos, kwani sisi huenda hizo bar na mahoteli wanaenda, hapana sisi hapa katani hakuna hiyo ugonjwa.
3. M3: Kwanza wewe nikuulize, umeona corona kweli, au kuna mtu wenu ako na corona? Serikali inatuchesa tu ipate doo kutoka ng'ambo.
4. M4: Mi najua hakuna korona na hata hiyo stori hainibambi juu tunacheswa kaa watoi wakubwa wakiunda pesa.
5. Mtafiti: Haki nyinyi mnanishangaza, mnawezaje kusema kuwa hakuna corona na kuna watu wamekufa nayo. Ni vi...
6. M1: Wewe nikuulize, kuna mtu unajua mwenye ako nayo?
7. M4: Sema sasa.
8. Mtafiti: Mimi kuna uncle yangu amekufa nayo.
9. M3: Waah, hao ni wale familia zao zimelipwa na gava waseme kuna corona.
10. M2: Hata mimi najua kuna watu wamekanjwa pesa mingi wadanganyie tu.
11. Mtafiti: Nimeona siwezi kuwaconvince eti kuna.....
12. M4: Au na wewe umelipwa ndio uambie watu ati kuna corona?
13. Mtafiti: Mimi sijalipwa na hata sijui mtu yeyote kwa gava, ni hustler tu kama nyinyi. Hata hivyo, bye.

4. Vijana wa eneo la Ruai ambao huwa na mashamba ya kuuza miti na mboga za kupanda kando kando ya barabara ya Kangundo

1. Mtafiti: Huu ujumbe wa TV mnaupokea vipi.
2. M1: Mi chenye nimepata ni hizo symptoms. Nakuwa keen hata nikisikia kukohoa naogopa.
3. Mtafiti: Na wewe mwenzangu?

4. M2: Hata juzi nimeenda soko kubuy minji, wacha jamaa akohoe, kila mtu alienda mbio.
5. Mtafiti: Na wewe kijana?
6. M3: Hiyo TV inatumia kizungu ngumu hata sielewangi mimi walahi.
7. Mtafiti: Mwenzangu unaonaje?
8. M4: Hiyo ujumbe hunikumbusha tu kuwa kuna corona na hivyo natake caution.
9. Mtafiti: Hey, na wewe?
10. M5: Hizo vitu hazielewekangi saa hata sisomangi.
11. Mtafiti: Husomangi, sasa utajuaje ni nini kinaendelea nchini?
12. M5: Sasa vitu wanasema haieleweki, hatujui kama ni ukweli kama kuna corona. Tena..
13. M2: Hata huyo Minister wa Health si anasemanga kuwa hawaelewi hii ugonjwa vizuri.
14. Mtafiti: Unajua anasema hivyo kwa sababu huu ni ugonjwa ambao ni mpya kwa kila mtu na hata madaktari wanaendelea kuujua tu.
15. M4: Hata hizo signs wanashinda wamesema mi nilikuwa nazo 2019 na nikatibiwa pneumonia.
16. M1: Heeeh, hiyo inamaanisha kuwa pneumonia ndio wameanza kuiita corona.
17. Mtafiti: Imagine sio vile mnafikiria na ndio maana ni vizuri mfuate yale Kagwe anasema ndio...
18. M3: Wachana na huyo mtu wa corona, mbona yeye hajaadmitiwa hosi.
19. Mtafiti: Haki fanyeni tu vile serikali inasema ndio tupunguze msambao zaidi. Wacha niwaache mwendelee na kazi yenu. Asanteni.

5. Vijana waliokuwa wakifanya kazi barabarani hali maarufu ‘kazi kwa vijana’ eneo la Shooters, Nairobi

1. Mtafiti: Habari zenu vijana? Mnajua corona iko?
2. Wote: Ndio.
3. Mtafiti: Sasa mlichukuliaje maneno ya Waziri wa Afya aliposema kuwa “...If we continue to behave normally, this disease will treat us abnormally...”

4. M1: Mi vile nimeelewa ni kwamba waziri anataka watu wajikinge kabisa na hii corona juu inatembea mbio sana.
5. M2: Kwa upande wangu, mimi naona Waziri anatueleza vile hii ugonjwa ni mbaya. Juu haki watu wa Amerika wamekufa tu sana. Sasa Waziri ametueleza tu vile tunafaa kuzuia hii ugonjwa.
6. Mtafiti: Wewe unajua njia zipi?
7. M2: Kulingana na vile nimemsikia akisema mara kadhaa ni kuwa ugonjwa hii inaletwa na uchafu, na pia inasambazika kupitia kusalimiana. Saa hiyo ni rahisi juu tumeshaacha hata kusalimiana na kutembeleana.
8. M3: Ndio maana hata hakuna mwenye ako na hiyo corona hii Kisii.
9. M4: Mask ndio ngumu tu juu hata huwezi pumua lakini tunavaa kwanza tukikuja huku tao.
10. M5: Mi chenye nilielewa ni kuwa hii ugonjwa sio normal aki na tunatakiwa kuwa serious vile anasema juu unajua yeye ni Minister for Health so ni kumaanisha kuwa anajua juu ya corona kutuliko.
11. Mtafiti: Atleast nyinyi mnajua vile mnatakiwa kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya corona. Endelea tu kuvaa mask na kuosha mikono au kusanitize kila mara hasa ukishika pesa.
12. M1: Sasa wewe ni mtu wa serikali au ni nani?
13. Mtafiti: Mimi ni raia tu kama nyinyi lakini nimeona niwahamashe ndio tupunguze maambukizi ya ugonjwa wa COVID. Bakini salama.
14. M3: Sawa, wacha tuendeleo kuosha mikono.

6. Wakenya watatu wa Utawala, eneo la mafuta ya magari, Lexo

1. M1: Mi chenye najua, hiyo time alikuwa anamaanisha kuwa corona sio mbaya sana Kenya.
2. Mtafiti: Mbona unasema hivyo?
3. M1: Si alisema no cause for alarm.
4. M2: Hiyo kitu alisema ilimaanisha kuwa hii ugonjwa iko na dawa. Kaa huyo mtu wa kwanza alipona, basi hata mwenye atashikwa nayo atapona tu.

5. Mtafiti: Hawajasema kuna dawa, inategemea tu na immune ya mtu binafsi. Mwenzangu wewe unasemaje?
6. M3: Hiyo tu inamaanisha kuwa tusijali as in hii ugonjwa si hatari sana.
7. M1: Hii kitu ni kaa homa tu ya kawaida, haina haja kuworry sana.
8. Mtafiti: Kwani wewe huogopi mwenzangu?
9. M1: Watu kaa sisi tumepitia maissue mob hadi vitu inakaa homa haitutishi.
10. M3: Mi chenye naogopa ni mtoi wangu apate, ndio maana najaribu tu kufuata hizo masharti za viongozi wa.....
11. M2: Yenyewe hakuna kitu mbaya mtoi akue msick, Walahi hamuwezi kulala.
12. Mtafiti: Ndio maana mnapaswa kuzingatia sheria ambazo zimewekwa na Wizara ya Afya ndio msipelekee watoto corona. Sawa sasa mbaki poa.

7. Watu wanaouza na wanaotumia miraa katika eneo la Shooters, Utawala jijini Nairobi

1. Mtafiti: Saseni?
2. Watafitiwa: Poa.
3. Mtafiti: Waziri amesema kuwa mkulie jaba nyumbani, yaani mkae tu nyumbani juu itaingia tu. Maoni yenu ni yapi kuhusiana na hali hii mpya?
4. M1: Aaah, si mbaya kama hiyo itatuliza corona sisi ni nani tukatae?
5. M2: Hiyo itasaidia lakini saa hii bizna iko down manze. But ni sawa wacha tuchungane.
6. Mtafiti: Bizna iko down kwa nini na bado watu wanatumia bado?
7. M2: Wee huoni vile wateja wamereduce, hapa kungejaa saa hii kama ni before corona.
8. Mtafiti: Walienda wapi?
9. M2: Saa hii ni kaa nyumbani, wewe huoni. Hii corona inaua watu sana.
10. M1: Watu wanaogopa makarao zaidi kuliko hata corona. Huku makarao wanatembeanga kutafuta watu hawafuati vile serikali inasema.
11. Mtafiti: Na unajua hiyo sio poa coz kila mtu anatakiwa afuate sheria za serikali ndio ajikinge na awakinge wengine.

12. M2: Sasa sisi hapa tunavaa mask na tunaoga mikono kila saa lakini huko mtaa watoi wetu wanaruka tu hapa kule kila mahali day yote, hiyo corona itawakosa kweli.
13. M1: Hii kitu ni Sir Jah tu atuepushie, bure sisi hatuna nguvu. Hata saa hii najua msee anaeza genya na chochote hata accident, wengine ni kansa na kadhalika.
14. M2: Uko on point brathe.
15. Mtafiti: Ni hivyo lakini ni heri kujikinga ndio Mungu pia akusaidie. Tutaonana baadaye but keep safe my brothers.

8. Wakaazi wa Mlolongo wanaofanya kazi katika kampuni ya simiti ilioko katika eneo la Athi River

1. Mtafiti: Habari zenu?
2. Watafitiwa: Poa.
3. Mtafiti: Waziri Kagwe akiwa Mombasa alisema hivi “Tujikinge, tujitayarisha sio kitu inapita harakaharaka. Tutafanya chochote ndio watu wasiumie au kufa vile nchi zingine tuwe tayari. Kenya tunaona vile kunafanyika hata ng’ambo. Tunawasihi tufanye vile serikali inasema usijaribu eti wewe ni mwerevu. Usicheze sio uerevu ni ujinga.” Je, wewe uliuelewa aje huu ujumbe?
4. M1: Huyu mtu wa corona aliongea poa. Kaa watatupea msaada tutatulia tu tusiende job Macha. Lakini for now hatuna option juu familia lazima ikule.
5. Mtafiti: Mwenzangu wewe unasemaje?
6. M2: Mutahi anajaribu kutueleza tutulie, juu hii kitu kama imetesa watu wa Amerika wenye wako na uwezo mwingi wa kila kitu, na sisi? Afadhali tutulie tu hadi hii corona iishe.
7. Mtafiti: Wewe unachukulia kuwa alisema poa, hiyo ni mzuri. Ndugu yangu wewe waonaje?
8. M3: Yenyewe ni ujinga mtu kupitia panya route afike kwao ushago halafu apelekee mamathee wenye wamezeeka corona na wakufe tu. Mi nakubaliana na Waziri, wacha watu wakae mahali wako ndio hii kitu iishe haraka haki. Lakini Wakenya tuko wajinga haki, hata maski watu hawataki kuvaa walahi.

9. M2: Ujinga ndio inatumaliza haki, sa mtu hajapima halafu anakimbia ushago mahali hata tuhosi hatuwezi kutibu malaria. Na sasa akiwa na corona, si watu watakufa tu na waambukizane kijiji yote?
10. Mtafiti: Nafurahia vile mnachukulia jambo hili kwa uzito unaofaa. Hii inaonyesha kuwa mko tayari kushirikiana na serikali ili kupunguza maambukizi zaidi hasa kwa wazazi wetu ambao wako mashambani. Shikilia hapo ndio atleast turudie hali yetu ya kawaida. Mbaki mpoa watu wangu.
11. M2: Tuombeane tu madam.
12. Mtafiti: Ni sawa basi, nitafanya.